# UHAMISHAJI WA MAANA KATIKA SAJILI YA MCHEZO WA KANDANDA

ANJEJO MARK ODAWO

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA

2015

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya shahada katika Chuo Kikuu chochote kingine.

Sahihi__________________ Tarehe 2/6/2015

ANJEJO MARK ODAWO

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu Cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi.

Sahihi__________________ Tarehe 02.06.2015

DKT. LEONARD M. CHACHA

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.

Sahihi__________________ Tarehe 02.06.2015

DKT. JACKTONE O. ONYANGO

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mke wangu, mwana wa wakwe zangu, Lucy Atieno, kwa kunitia shime na kunijaza kani hata nikafikisha chombo hiki bandarini. Hakika muhibu, wewe ni wa mtima wangu wa dhati. Nyie mabinti zangu, Marion Treazer, Wendy Jennifer na Cindy Keylla, kipande cha moyo wangu mnachojikita kitadumu daima. Ukamilifu wa maisha yangu unafungamana na nafsi zenu. Stahamala wenu nilipozamia kazi hii hata ikaelekea kuonekana kuwa niliwatelekeza haiwezi kupigiwa mfano.

Muhibu wa mtima Lucy

Marion wa nafsini binty

Kwa dhati ya dhamiri Wendy

Nawe azizi Cindy

*Tangu azali, meonesha kubali,*

*nijitie makali, mpukutikie dhalili,*

*almuradi ya mustakabali, niumbulike ugiligili,*

*nikwelee majabali iso kalili, utashi wa stahamili,*

*nyie amana aali, Jalali akupevusheni jamali.*

**SHUKRANI**

Shukrani zangu za dhati ninamtolea Mwenyezi Mungu kwa kunikirimia na kunifikisha umbali huu. Yakini umenibeba pasi kujikaza. Pili, ninawashukuru na kuwapongeza wasimamizi wangu, Daktari Leonard M. Chacha na Daktari Jacktone O. Onyango kwa mwongozo mpevu uliofanikisha kazi hii. Ninathamini mno ushauri wenu tangu mada ya tasnifu hii ilipotayarishwa. Sitasahau asilani mlivyonikongoja na kunihimiza kuning'inia ukambaa huu hata kunitanabahisha kumakinikia kazi hii. Mlisoma kazi yangu bila kuchoka na kunitaalamisha kwa weledi wenu. Asanteni kwa kuwa dira na kielelezo kwa wasomi limbukeni kama mimi. Daktari Pamela M.Y. Ngugi, asante kwa mchango wako hasa mada ya tasnifu hii ilipojengwa. Hukuchelea kunizindua nilipopayapaya. Mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Daktari Richard M. Wafula, Mwenyekiti wa Shahada za Juu, Daktari Alice N. Mwihaki, na wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, ninawapongeza kwa kuwa mlikuwepo na kunifaa kila nilipohitaji ushauri wenu. Asanteni kwa kunifundisha na kunielekeza kiusomi.

Kwa wanafunzi wenzangu, Iladiva Jesicah, Ashioya Cosnet, Kalekye Beth, Mutie Janet, Sitati Amos, Nyamohanga Paul na Sylvans Mahiandah, ninawakumbuka kwa shinikizo na pandashuka tulizopitia pasi kukubali kutamauka. Hili ni zao la zihi zilizotububujika. Kwa mkutubu wa Maktaba ya Idara, Caroline, unastahili shukrani kwa msaada wako ambao thamani yake haiwezi kupatikana katika fedha.

Mwana wa wakwe zangu, Lucy Atieno, umenifaa mno na kunipiga pambaja kwa mvua na jua. Katu siwezi kusahau hisani jazila, hazina lufufu na mshawasha mzo ulionipa. Mabinti zangu Marion Treazer, Wendy Jennifer na Cindy Keylla, asanteni kwa kuridhia kukoseshwa mengi katika harakati zangu za kujijuza. Haya yote yalijiri kwa kutilia maanani siku zenu za halafu. Kweli pasipo ninyi, kele za nini? Nitakuwa mtovu wa hisani nikisusia kuwashukuru wazazi wangu. Babangu Alois Odawo na mamangu Teresa Adero, ninawapongeza kwa ulezi wenye maadili, maombi na ushauri wenu jalili. Tangu dahari, mmenigutusha kufikia upeo wa juu zaidi katika yote nifanyayo. Hamkusahau kunikumbusha kwamba kila aotaye ana uwezo wa kujukumikia utimiaji wa ndoto zake.

Nicholas Agull, sijamaizi ingeniwiaje kama hungenichagiza kujibwaga na kuogelea katika shumbi hii ambayo sikujua kina chake. Unajua zaidi yangu kuwa ulinifaa kwa hali na mali. Nakushukuru ndugu. Japo ni muhali kumtaja kila yeyote aliyechangia urutubishaji wa kazi hii, mchango wenu utathaminiwa daima.

# IKISIRI

Utafiti huu ulinuia kubainisha jinsi maana inavyohamishwa katika sajili ya mchezo wa kandanda nchini Kenya. Lugha ya mchezo wa kandanda huonyesha namna ya utegemezi wa maneno na kauli za sajili tofauti na istilahi za taaluma nyingine kufuma na kuibua maana. Utafiti huu ulilenga kutimiza malengo matatu yafuatayo: Kutambua mbinu za mawasiliano zinazotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda, kubainisha msimbo wa maana inayoibuliwa kutokana na matumizi ya lugha katika sajili ya mchezo wa kandanda na kubainisha taaluma na sajili zinazotumiwa na sajili ya mchezo wa kandanda ili kujitosheleza. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo iliyoasisiwa na Halliday (1985). Nadharia hii inaeleza kuwa kama tukio la kijamii, lugha iliundwa kwa minajili ya kuwezesha mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. Inaangalia lugha sawa na mtandao wa maana unaowakilishwa kwa maumbo ya kisarufi. Data ya utafiti huu ilikusanywa maktabani na nyanjani. Maandishi yanayohusu mchezo huu kutoka vitabu, makala, tasnifu, magazeti na majarida yalidurusiwa ili kujenga usuli wa utafiti huu na kung'amua yaliyoandikwa kuhusu mada. Matangazo ya moja kwa moja ya mchezo huu na taarifa za mchezo huu katika redio na runinga yalisikilizwa ili kupata data iliyochanganuliwa. Data iliyokusanywa ni msamiati, istilahi, virai, vishazi na sentensi. Data iliainishwa na kuchanganuliwa kwa uzingativu wa maswali na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo yaliyojumuisha matumizi ya majedwali. Ripoti ya utafiti huu imepangwa katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi uliojumuisha usuli wa mada, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, mapitio ya maandishi, misingi ya kinadharia na mbinu za utafiti. Sura ya pili imeangalia mbinu za mawasiliano zinazotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda. Mbinu zilizobainika ni utohozi, uchanganyaji msimbo, ubadilishaji msimbo, takriri, tashbihi, tashihisi, semi, methali, maswali ya balagha na tafsiri sisisi. Sura ya tatu imebainisha msimbo wa maana inayoibuliwa kutokana na matumizi ya lugha katika sajili ya mchezo wa kandanda. uchanganuzi wa data umebainisha kuwa lugha huwa na maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi. Sura ya nne iliangazia taaluma na sajili zinazotumiwa na sajili ya mchezo wa kandanda ili kujitosheleza. Imejitokeza kuwa sajili ya mchezo wa kandanda hutegemea istilahi na vipashio vya sajili ya hoteli, ulinzi, hospitali, biashara na mapenzi. Sura ya tano ni muhtasari wa matokeo ya utafiti, mahitimisho na mapendekezo. Imependekezwa kuwa maandishi na malumbano baina ya mashabiki wa sajili hii yachunguzwe kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika lugha ya uneni inayotumiwa na watangazaji wa mchezo huu. Mbali na kutafiti namna lugha inavyotumiwa katika aina tofauti ya michezo, pana hitaji la kuchunguza lakabu zinazohusu wachezaji, wakufunzi na viwanja mbalimbali ili kubainisha maana zinazotokana nazo. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yanatazamiwa kuwa ya manufaaa kwa wanafunzi, walimu, watafiti na wataalam wengine wa isimu watakaozamia matagaa ya semantiki na pragmatiki, hasa kuhusu maana inavyoibuliwa katika miktadha mbalimbali. Waaidha, yatatoa mchango mkubwa kwa waitifaki wa isimujamii wanaodhamiria kukuza sajili changa.

## ABSTRACT

This research intends to show how meaning is transferred in sports register, particularly the game of football in Kenya. Football language shows to a great extent some form of dependence on terminologies and phrases that are usually associated with other styles and different professions in a bid to give meaning and be understood. The research intends to accomplish this by realizing the following three research objectives: To identify methods and aspects of communication that are used by football commentators, to show how meaning is transferred in football register and to investigate professions and registers that form the basis of language use in football register . This research was based on the theory of Systematic Functional Grammar that was postulated by Halliday (1985). This theory holds an argument that as a product of social life and interaction, language was invented for communication purposes in relation to different contexts. It views language as a network of meaning that is represented by grammatical elements. Data that was used in this research was collected both in the library and in the field. Written texts concerning football in books, theses, newspapers and sports magazines were investigated in order to generate information concerning research topic and literature review. Football commentary on radio and news concerning football on radio and television were investigated in order to generate enough data. Data that was collected includes vocabularies, terminologies, phrases and sentences. Data collected was sorted and analyzed on the basis of the research objectives in conformity with the principles of the research theory. Data presentation has been done through tabulation and written essay. This research has been presented in five chapters. Chapter one includes research topic, research questions and objectives, scope and limitations of the study, literature review, theoretical framework and research methods. The second chapter identified methods and aspects of communication that are used by football commentators. They include, code mixing, code switching, repetition, similies, personification, proverbs, rhetorical questions and direct translation. The third chapter examined how meaning is transferred in football register. Forms of meaning identified include conceptual meaning, social meaning and textual meaning. The forth chapter investigated professions and registers that form the basis of language use in football register. Terminologies associated with the field of medicine, defense, hotel and hospitality, business and love relationships were identified. The fifth chapter will include summary, conclusions and recommendations. Further research in relation to language use in written texts, among football fans and other sports is recommended. The findings of this research are therefore expected to be of great benefit to students, teachers, researchers and other linguistic scholars who intend to dig deeper into semantics and pragmatics, especially on how meaning is transferred in different contexts and registers. The findings shall also give enormous contribution to researchers who would be keen to develop new styles in sociolinguistics.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI NA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| Kandanda | : | Mchezo unaochezwa kwa miguu wenye timu mbili zinazoshindana. |
| Kirai | : | Kipashio cha kisarufi kinachoundwa na neno moja au fungu la maneno na hakina muundo wa kiima-kiarifa. |
| Kusawiri | : | Kufanya kitu au jambo lieleweke bayana kutokana na lilivyoelezwa. |
| Mashabiki | : | Watu wanaopenda sana na kuushangilia mchezo wa kandanda. |
| Matini | : | Mfululizo wa usemi unaowasilisha ujumbe dhahiri. |
| Uhamishaji | : | Utumizi wa vipashio vya kisarufi kuibua maana tofauti. |
| SAM | : | Sarufi Amilifu Mfumo. |
| T.y | : | Tafsiri yangu. |

## YALIYOMO

Ukurasa

**Mada**....................i

Ungamo....................ii

Tabaruku....................iii

Shukrani....................iv

Ikisiri....................vi

Abstract....................vii

Ufafanuzi wa Istilahi na Vifupisho....................viii

Yaliyomo....................ix

Orodha ya Majedwali....................xiii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**

1.0 Usuli wa Mada....................1

1.1 Suala la Utafiti....................5

1.2 Maswali ya Utafiti....................6

1.3 Malengo ya Utafiti....................6

1.4 Sababu za Kuchagua Mada....................7

1.5 Upeo na Mipaka....................8

1.6.0 Yaliyoandikwa kuhusu Mada....................9

1.6.1 Maandishi ya Jumla kuhusu Mada....................9

1.6.2 Tafiti Mahsusi kuhusu Sajili....................12

1.7 Misingi ya Kinadharia....................18

1.8.0 Mbinu za Utafiti....................23

1.8.1 Uteuzi wa Sampuli....................23

1.8.2 Mbinu za Ukusanyaji wa Data....................25

1.8.3 Mbinu za Uchanganuzi wa Data....25
1.8.4 Uwasilishaji wa Matokeo....26
1.9 Hitimisho....26

## SURA YA PILI: MBINU ZA MAWASILIANO KATIKA SAJILI YA MCHEZO WA KANDANDA

2.0 Utangulizi....27
2.1 Utohozi....29
2.2 Uchanganyaji Msimbo na Ubadilishaji Msimbo....38
2.2.1 Uchanganyaji Msimbo....38
2.2.1.1 Uambatishaji wa Kiungo....40
2.2.1.2 Uchopekaji wa Maneno ya Kigeni Kati ya Sentensi....42
2.2.1.3 Uchopekaji wa Maneno ya Kigeni Mwishoni mwa Sentensi.45
2.2.2 Ubadilishaji Msimbo....46
2.2.2.1 Kurejelea....50
2.2.2.2 Kufafanua....51
2.2.2.3 Kupendeza na Kujitambulisha....52
2.2.2.4 Kuonyesha Hisia....52
2.2.2.5 Kusisitiza....54
2.3 Tamathali za Semi....56
2.3.1 Takriri/Urudiaji....57
2.3.1.1 Takriri-Vitenzi....58
2.3.1.2 Takriri-Nomino....59
2.3.2 Tashbihi....61
2.3.3 Tashihisi....63
2.3.4 Misemo/Nahau....67

2.3.5 Misimu/Simo....71

2.3.6 Methali....79

2.4 Maswali ya Balagha....84

2.5 Tafsiri Sisisi....89

2.6 Hitimisho....93

**SURA YA TATU: MAANA KATIKA MATINI.**

3.0 Utangulizi....96

3.1 Maana Dhanishi....96

3.1.1 Matumizi ya Vitenzi....97

3.1.2 Matumizi ya Nomino....105

3.1.3 Matumizi ya Vivumishi....109

3.2 Maana Tagusani....114

3.2.1 Maagizo/Amri....116

3.2.2 Kurai....117

3.2.3 Maswali....119

3.2.4 Maelezo....122

3.3 Maana Matinishi....125

3.3.1 Ugeuzi....126

3.3.1.1 Upanguaji....127

3.3.1.2 Uchopekaji....129

3.3.1.3 Udondoshaji....130

3.3.2 Uwakilishaji/Urejeshi....133

3.3.3 Uunganishi/Uhusishi....135

3.4 Hitimisho....139

**SURA YA NNE: UFUMAJI WA SAJILI YA MCHEZO WA KANDANDA**

4.0 Utangulizi....142

4.1 Taaluma ya Ulinzi....143

4.1.1 Vitenzi katika Taaluma ya Ulinzi....144

4.1.2 Nomino katika Taaluma ya Ulinzi....146

4.1.3 Vivumishi katika Taaluma ya Ulinzi....151

4.1.4 Semi katika Taaluma ya Ulinzi....153

4.2 Sajili ya Biashara....155

4.3 Sajili ya Utabibu/Hospitali....157

4.4 Sajili ya Hoteli/Taaluma ya Upishi....160

4.5 Sajili ya Mapenzi....162

4.6 Hitimisho....167

**SURA YA TANO: HITIMISHO**

5.0 Utangulizi....168

5.1 Matokeo ya Utafiti....169

5.2 Mahitimisho ya Utafiti....177

5.3 Mapendekezo ya Utafiti....179

MAREJELEO....180

VIAMBATISHO....190

Kiambatisho 1: Matini za Misimu....190

Kiambatisho 2: Matini za Vitenzi....192

Kiambatisho 3: Matini za Nomino....194

Kiambatisho 4: Matini za Kauli za Maelezo....196

Kiambatisho 5: Matini za Udondoshaji....197

# ORODHA YA MAJEDWALI

Ukurasa


Jedwali 2.1: Utohozi wa Nomino Zinazohusu Wachezaji na Wasimamizi................29

Jedwali 2.2: Utohozi wa Nomino Zinazohusu Klabu, Usajili wa Wachezaji na Wakufunzi..........................................................................................32

Jedwali 2.3: Utohozi wa Nomino Zinazohusu Hali ya Mchezo................................34

Jedwali 2.4: Uambatishaji wa Kiungo........................................................................41

Jedwali 2.5: Uchopekaji wa Maneno ya Kigeni Kati ya Sentensi.............................42

Jedwali 2.6: Uchopekaji wa Maneno ya Kigeni Mwishoni mwa Sentensi.................45

Jedwali 2.7: Matumizi ya Tashbihi.............................................................................61

Jedwali 2.8: Matumizi ya Tashihisi: Vitenzi...............................................................63

Jedwali 2.9: Matumizi ya Tashihisi: Semi...................................................................65

Jedwali 2.10: Matumizi ya Tashihisi: Nomino............................................................66

Jedwali 2.11: Matumizi ya Misemo kutokana na Kitenzi Piga...................................68

Jedwali 2.12: Matumizi ya Misemo Mingine..............................................................69

Jedwali 2.13: Matumizi ya Misimu Inayohusisha Mchezo wa Kandanda na Makabiliano..............................................................................................72

Jedwali 2.14: Matumizi ya Misimu Inayohusiana na Matukio ya Mchezo................74

Jedwali 2.15: Matumizi ya Misimu Isiyochukua Muundo wa Kitenzi-Nomino.........76

Jedwali 2.16: Matumizi ya Tafsiri Sisisi Zinazohusu Hali ya Mchezo na Usajili wa Wachezaji.......................................................................................89

Jedwali 2.17: Matumizi ya Tafsiri Sisisi inayohusu Lakabu za Klabu za Kandanda..91

Jedwali 3.1 Matumizi ya Vitenzi Vinavyohusisha Mchezo wa Kandanda na Makabiliano....98

Jedwali 3.2 Matumizi ya Vitenzi Kitamathali....101

Jedwali 3.3 Matumizi ya Nomino....105

Jedwali 3.4 Matumizi ya Vivumishi....109

Jedwali 4.1: Vitenzi katika Taaluma ya Ulinzi....144

Jedwali 4.2: Nomino Zinazorejelea Zana za Vita....147

Jedwali 4.3: Nomino Zinazohusisha Mchezo wa Kandanda na Makabiliano au Uhasama....148

Jedwali 4.4: Nomino Zinazohusisha Mchezo wa Kandanda na Nguvu na Mamlaka ya Kiutawala....150

Jedwali 4.5: Vivumishi katika Taaluma ya Ulinzi....152

Jedwali 4.6: Semi katika Taaluma ya Ulinzi....153

Jedwali 4.7: Istilahi za Sajili ya Biashara....155

Jedwali 4.8: Istilahi za Sajili ya Utabibu....158

Jedwali 4.9: Istilahi za Sajili ya Hoteli....160

Jedwali 4.10: Istilahi za Sajili ya Mapenzi....163

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Lugha kama chombo cha kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wanadamu hutumia sauti nasibu na ishara zilizoteuliwa na kukubaliwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za wanajamii wanaohusika. Cook (1969) anasema kuwa binadamu hujamiisha na kumilikisha lugha kama mali yao wanapoitumikisha kwa kufuata kanuni zinazokubalika. Kwa mujibu wa haya, wanajamii hufaulu kuwasilisha mawazo, mahitaji, hisia na tajriba zao kwa kutumia lugha kwa njia ya kipekee.

Halliday na wengine (1964) nao wanaeleza kuwa kama tukio la kijamii, dhima ya lugha ni kufaulisha mawasiliano miongoni mwa wanajamii licha ya kueleza mazingira wanamoishi. Uamilifu wa lugha katika kupambanua binadamu hudhihirika katika uwezo wake wa kusawiri kiwango cha juu cha kupevuka kwa binadamu. Ni muhali kwa tamko lolote la lugha kueleweka ipasavyo linapofasiriwa bila kuhusishwa na ujuzi wa watumizi wake, mahusiano yao, hali zao, mada inayozungumziwa, uwanda, mazingira, umri na taaluma miongoni mwa kaida nyingine zinazoongoza uteuzi wa maneno na kudhibiti mawasiliano.

Katika kufanikisha mawasiliano, lugha huhusisha na kutegemea maneno, semi pamoja na viziada lugha. Bolinger na Sears (1981) wanaeleza kwamba uwezo wa binadaamu wa kujifunza, kuimudu na kuitumia lugha kwa ufaafu hujitokeza katika utumizi wa ishara za kusikika (sauti) na za kuonekana (viziada lugha).



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Uambatishaji wa utumizi wa viziada lugha husahilisha na kurahisisha welewa wa baadhi ya dhana changamano.

Ili kueleweka bayana, lugha huchunguzwa na kupambanuliwa kupitia viwango vyake. Todd (1987) anataja viwango vya lugha kama fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Massamba na wengine (1999) wanarejelea kiwango cha fonolojia kama sarufi sauti au umbo-sauti, mofolojia kama sarufi maumbo au umbo-neno, sintaksia kama sarufi miundo au miundo-maneno na semantiki kama sarufi maana au umbo-maana.

Kulingana na Mgullu (1999), fonolojia ni tawi la isimu linaloshughulikia uchambuzi wa mfumo wa sauti au fonimu zinazotumiwa katika lugha fulani. Anaeleza mofolojia kama tawi la sarufi linaloshughulika na uchambuzi wa mofimu na alomofu zake na jinsi zinavyokaa pamoja kuunda maumbo mbalimbali ya maneno katika lugha. Maelezo ya TUKI (1999) yanaafikiana na maoni ya Massamba na wengine (1999) wanaoeleza sintaksia kama tawi la sarufi linaloshughulikia uchanganuzi wa mpangilio na uhusiano wa vipashio katika sentensi. Ullmann (1972) anasema kuwa semantiki ni nadharia inayoshughulikia sayansi ya maana na namna maana hizo zinavyohusiana. Kwa kuwa maana ya lugha itachunguzwa kulingana na muktadha wa matumizi yake, utafiti huu unaohusu uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda utafuma uchunguzi wa kiwango cha semantiki na jinsi kinavyohusiana na tagaa la pragmatiki.

Utanzu wa pragmatiki huamilisha maana katika lugha. Hivi ni kusema kwamba lugha hutumiwa na watu binafsi kwa namna mbalimbali kuashiria dhana tofauti. Maneno hutumiwa kutaja vitu na kurejelea hali anuwai. Matumizi haya huongozwa, huelekezwa na kudhibitiwa na kaida na maadili ya jamii husika. Dhana zinazoashiriwa na maneno hutarajiwa kutambulika na kubainika na wanajamii. Hudson (1995) anaeleza kuwa kama mfumo nasibu, lugha huhitaji urudifu wa neno linaloashiria dhana fulani ili kulizoesha kwa matumizi hayo. Hali hii huzua miktadha maalum ya matumizi ya lugha.

Miktadha hii mahsusi ndiyo inayozua sajili mbalimbali kutegemea shughuli na mahitaji ya wanajamii. Halliday na Hasan (1989) wanatoa tafsili ya sajili kama maneno anayoyatumia mtu kutegemea shughuli aliyomo. Huu ni upambanuzi wa lugha kwa mujibu wa inakotumiwa na inavyotumiwa.

Ipara na Maina (2008) wanasema kwamba lugha katika upekee wake hukosa kukidhi mahitaji ya watumizi wake katika nyanja zote za mawasiliano. Kutokana na hali hii, watu hujitokeza na namna mbalimbali za kuitumia lugha ile moja. Hii ina maana kuwa mtu mmoja anaweza kutumia lugha kwa namna tofauti kutegemea jambo analotenda na mahali anapolitenda. Namna au mitindo hii mbalimbali ya matumizi ya lugha ile moja ndiyo inayorejelewa kama sajili. Wanaeleza zaidi kuwa sajili hutegemea kaida za matumizi ya lugha kama vile mazingira, kazi, uhusiano, umri, jinsia, hadhi na hali ya wahusika. Kaida hizi hutoa mwongozo

katika uteuzi wa aina fulani ya msamiati, maudhui, miundo ya sentensi na uketo wa sauti.

Kwa mujibu wa Habwe na wengine (2010), sajili ni mtindo wa lugha unaotumiwa katika miktadha maalum. Wanaeleza kuwa mtindo huchukuliwa kuwa sajili inapohusu jinsi mtu au kundi fulani linavyotumia lugha kujieleza. Wanataja sifa arudhi kama vile shadda na kidatu kama vipengele vya kimtindo.

Kulingana na Lehman (1972), sajili ni mtindo wa matumizi ya lugha kwa uzingativu wa taaluma, mahali, jinsia, umri na mahusiano ya wahusika. Aidha, Spolsky (1998) anaeleza kwamba sajili hutambuliwa kwa msamiati na istilahi zinazojenga msingi wa taaluma husika. Crystal na Davy (1969) wanaeleza mitindo ya lugha kama sifa za lugha zilizoamilishwa katika miktadha ya jamii. Baadhi ya mitindo waliyotambua na kupambanua ni ya maabadani, matangazo ya biashara, ripoti ya magazeti na sheria. Wanataja shughuli za wahusika, mahusiano yao na eneo lugha inapotumiwa kama baadhi ya mambo yanayobainisha sajili au mitindo tofauti. Hivyo basi, lugha inayohusishwa na sajili fulani huwa na sifa mahsusi inayotambulishwa nayo.

Hata hivyo, hali hii haijitokezi kila wakati lugha inapotumiwa. Mara nyingine maana ya maneno hubadilika, hutokea ugeuzaji na urefushaji wa maana na upanuzi wa matumizi ya lugha. Mawazo haya yanaoana na ya Halliday na wengine (1964) wanaosema kwamba lugha inakua na kupanuka kimatumizi kupitia tajriba na

mahitaji ya jamii. Waaidha, hudhihirika utegemezi wa istilahi, msamiati na vipashio vya sajili na taaluma mbalimbali kufuma sifa za sajili tofauti. Kwa njia hii pia hubainika uhamishaji wa maana katika sajili tofauti, hasa katika sajili ya mchezo wa kandanda ambayo utafiti huu ulilenga.

## 1.1 Suala la Utafiti

Shughuli zote za kila siku za binadamu humhitaji kutumia lugha kujieleza. Kadiri shughuli hizo zilivyo tofauti ndivyo lugha inavyotumiwa kwa njia tofauti ili kutimiza haja hizo na kubainisha mahusiano miongoni mwa watumizi wa lugha. Mahusiano hayo yanakitwa katika mazingira mahsusi kutegemea sifa bainifu na tambuzi za sajili mbalimbali. Sajili mbalimbali huwepo kwa kudhihirisha upekee wa matumizi ya lugha kimuktadha. Hivi ni kusema kwamba matumizi ya lugha katika shughuli na miktadha mbalimbali hutofautiana. Tofauti hizi ndizo zinazoamilisha lugha kimatumizi.

Hata hivyo, katika hali ya kujitosheleza kimatumizi, sajili ya mchezo wa kandanda huchota maneno kutoka kwingineko na kuyafinyanga kuibua maana. Hivi ni kusema kwamba lugha inatumiwa kwa namna isiyo ya kawaida ili kufanikisha mawasiliano. Kwa hiyo, panatokea upekee wa matumizi ya lugha katika kusuka msimbo teule na kufumba maana katika sajili hii. Hali hii huonyesha mwelekeo wa uhamishaji na upanuzi wa maana na namna ya utegemezi wa sajili ya mchezo wa kandanda katika istilahi za taaluma na sajili nyingine.

Upekee huu wa matumizi ya lugha unaohusisha uibuaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda kwa kutumia vipashio au maneno yasiyotokana na sajili hii ndilo zoezi ambalo utafiti huu ulilenga kuweka wazi. Hii ni kwa sababu wasikilizaji wa matangazo ya mchezo wa kandanda wakati mwingine hutatizika kuelewa jinsi lugha inavyotumiwa na maana inayowasilishwa na vipashio visivyohusiana na sajili hii. Hivi ni kusema kwamba utafiti huu ulinuia kubainisha ni wapi sajili hii huchota vipashio vyake na kwa namna gani inasuka vipashio hivi kuibua maana.

## 1.2 Maswali ya Utafiti

1. Ni mbinu zipi za mawasiliano zinazotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda?
2. Lugha inayotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda huibua maana gani?
3. Sajili ya mchezo wa kandanda hutumia taaluma na sajili zipi ili kujitosheleza?

## 1.3 Malengo ya Utafiti

1. Kutambua mbinu za mawasiliano zinazotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda.
2. Kubainisha msimbo wa maana inayoibuliwa kutokana na matumizi ya lugha katika sajili ya mchezo wa kandanda.

3. Kubainisha taaluma na sajili zinazotumiwa na sajili ya mchezo wa kandanda ili kujitosheleza.

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Mchezo wa kandanda unaendelea kuwa maarufu sana hasa katika miaka ya hivi karibuni. Idadi ya mashabiki wanaokusanyika uwanjani, klabuni na kwingineko kutazama na kusikiliza matangazo ya mchezo wa kandanda wanaendelea kuongezeka kila uchao. Vyombo vya habari navyo vinaendelea kuongeza upeperushaji wa moja kwa moja wa matangazo ya mchezo huu. Nafasi kubwa katika magazeti na majarida pia inaendelea kutumiwa kuandika habari na kuchapisha picha zinazohusu mchezo huu. Hivyo basi ni muhimu kutafiti mada inayohusu mchezo huu unaoendelea kuwatagusanisha watu katika jamii.

Miongoni mwa sababu zinazochangia hali hii ni kuwa mchezo wa kandanda unaendelea kuimarika na kubadilika kuwa taaluma na nyenzo ya ajira kwa wachezaji na wakufunzi mbali na kuwa soko la uwekezaji kwa wamiliki wa timu hizi. Baadhi ya timu hizi huasisiwa na wanajamii huku nyingine zikidhaminiwa na mashirika mashuhuri yanayozitumia kutangaza bidhaa na huduma zao kwa umma mkubwa wa kimataifa. Kwa sababu hii, wakaaji wa miji husika na watumizi wengi wa bidhaa na huduma za kampuni na mashirika haya hupenda kujihushisha, kujitambulisha na kujinasibisha na timu husika na hivyo kuwa mashabiki wake. Hali hii hatimaye huathiri jumla ya ujuzi wao wa lugha na

wanavyoitumia hata katika miktadha tofauti na mahusiano mengine. Uchunguzi wa asili ya vipashio vya lugha vinavyotumiwa na dhana zinazowasilishwa navyo ulikuwa wa umuhimu mkubwa katika utafiti huu.

Aidha, mada hii ilitafitiwa kwa kuwa kwa ufahamu wetu, uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda haujashughulikiwa na tafiti za awali za kitaaluma. Upekuzi wa kina na wa kiusomi wa mada hii kwa lengo la kubainisha uhamishaji huu wa maana ili kuiorodhesha miongoni mwa tafiti zinazohusu semantiki katika isimujamii ni muhimu. Kwa kutimiza haya, mada hii imetoa mchango mkubwa katika ukuzaji wa taaluma ya isimujamii na tagaa la pragmatiki.

**1.5 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulihusu uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda. Kauli au matini zinazotokana na matangazo ya moja kwa moja na ya taarifa za mchezo wa kandanda kutoka studio za redio na runinga ndizo zilizochunguzwa. Hii ni kwa sababu matangazo ya mchezo wa kandanda katika redio hufanywa kwa lugha ya Kiswahili na kufikia mashabiki wengi walio mijini na vijijini. Lugha ya matangazo ilichaguliwa pia kwa sababu ni lugha semwa iliyo na sifa za kipekee kama vile shadda na kiimbo ambazo zina uwezo wa kuibua ruwaza za maana.

## 1.6.0 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Kitengo hiki kinashughulikia maandishi ya kitaalamu na tafiti anuwai zinazohusiana na mada yetu ya utafiti kwa njia moja au nyingine. Yaliyoandikwa kuhusu mada yameangaziwa kwa awamu mbili:

1. Maandishi ya jumla kuhusu mada.
2. Tafiti mahsusi kuhusu sajili.

### 1.6.1 Maandishi ya Jumla kuhusu Mada

Mapitio ya jumla kuhusu uchanganuzi wa matumizi ya lugha yamefanywa kwa kina na wataalamu wengi. Crystal na Davy (1969) wanasema kuwa lugha inaweza kutumiwa kulingana na miktadha mbalimbali. Wanapambanua kuwa matumizi ya lugha katika miktadha na shughuli tofauti hurejelea sajili za lugha. Sajili ya sheria, matangazo ya biashara, matangazo katika redio na televisheni, ripoti katika magazeti na maabadani ni baadhi ya zile ambazo wanaisimu hawa wameangazia sifa zao. Kwa kufanya hivi, wamebainisha aina za lugha mbalimbali ndani ya lugha moja. Maelezo ya wataalamu hawa yalinufaisha utafiti wetu ambao uliangazia sifa za sajili ya mchezo wa kandanda.

Brown na Yule (1983) wanaeleza kuwa usemi unaweza kuchambuliwa kwa kutilia uzito wa maana inayoibuliwa. Hivi ni kusema kwamba watumiaji wa lugha wakati mwingine humaanisha zaidi ya yale wayasemayo hasa wanapozingatia miktadha tofauti. Kwao, usemi huweza kutumiwa kwa maana ya kimsingi au ya kawaida. Matumizi haya hulingana na maana dhanishi ambayo imefumwa katika

utanzu wa semantiki. Kwa upande mwingine, kauli huweza kufasiriwa kiulinganishi pale inapotumiwa kwa njia maalumu. Kwa kuwa mtafiti alichunguza jinsi maana inavyoibuliwa katika sajili ya mchezo wa kandanda, maandishi haya yalikuwa ya umuhimu mkubwa kwetu.

Akizungumzia uchanganuzi wa matini, Wendell (1992) anasisitiza umuhimu wa kuchunguza lugha kulingana na muktadha wa matumizi yake. Anasema kwamba uamilifu wa lugha hukamilika ndani ya matumizi yake katika muktadha maalumu. Maelezo haya yalishabihiana na malengo ya utafiti wetu yaliyonuia kubainisha maana zinazotokana na matumizi ya lugha katika sajili ya mchezo wa kandanda.

Lyons (1968) anasema kuwa maana na uamilifu wa neno hutokana na matumizi yake. Anaeleza kuwa kujua neno ni kujua matumizi yake bali sio kutafuta maana yake. Anasema kwamba maana inayoibuliwa na neno au kauli hutokana na uwezo wake wa kutumika katika mawasiliano. Norwich (1998) anadokeza kwamba neno au kauli hukubaliwa katika lugha kutokana na matumizi yake. Anasema kwamba kila neno au sentensi humaanisha kazi inayotenda katika mazungumzo. Mtazamo huu huangalia lugha sawa na kifaa cha kutekeleza majukumu mbalimbali na kama chombo kinachobadilika kulingana na mahitaji ya watumiaji wake. Kama kifaa kinavyotumiwa wakati mwingine kwa kazi isiyo yake ya kawaida, maana ya maneno au kauli huweza kubadilika kulingana na matumizi tofauti.

Butchavarov (1960) anaendeleza rai hii kwa kusema kwamba maana ya kauli yoyote ile inatokana na matumizi yake bali si kile kinachowakilishwa na kauli hiyo. Anaungwa mkono na Jefwa (2010) anayesema kuwa ili kung'amua matumizi ya maneno na kauli za lugha husika, ni lazima mtu afahamu vizuri mchezo wa lugha hiyo unaovipa vipashio maana. Maandishi haya yalinufaisha utafiti wetu uliotaka kuangazia jinsi maneno yasiyotokana na sajili ya mchezo wa kandanda yanavyotumiwa kuibua maana katika sajili hii.

Maana ya matini yoyote ile huangazia kusudi la mnenaji na msikilizaji. Hivi ni kusema kwamba maana inatokana na matarajio ya washiriki katika mazungumzo (Falk 1973). Maandishi haya yalifaa uchunguzi wetu uliozingatia namna lugha inavyotumiwa kuleta mawasiliano kati ya watangazaji wa mchezo huu na wasikilizaji wao.

Massamba (1987) anaeleza kuwa uibuaji wa maana ya maneno na kauli isiyozoeleka huweza kutokana na mazoea ya matumizi yake kwa njia fulani na pia maendeleo au mabadiliko yanayotokea katika nyanja mbalimbali za maisha. Maelezo haya yalijenga utafiti wetu ulioangalia jinsi maneno yanavyotumiwa kutoa maana tofauti katika sajili ya mchezo wa kandanda.

Njogu na wengine (2006) wanadai kuwa neno linalotumiwa katika muktadha mmoja huweza kupanuliwa ili litumike katika muktadha mwingine. Hivi ni

kusema kwamba neno hilo huweza kutoa maana tofauti na ile inayojulikana au kuzoeleka. Kwa kuwa utafiti wetu uliangalia jinsi maneno ya sajili tofauti na istilahi za taaluma nyingine zinavyotumiwa kuibua maana katika sajili ya mchezo wa kandanda, maelezo haya yalikwa na umuhimu kwetu.

### 1.6.2 Tafiti Mahsusi kuhusu Sajili

Verstergaard na Shroder (1985) wametafiti lugha ya matangazo katika majarida. Walijadili mbinu za lugha zinazotumiwa na namna ya kufasiri maana kwa kutumia nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo. Utafiti huu ulihusiana na wetu kwa kuwa zote zimetumia nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo kufasiri maana katika matini. Hata hivyo, zimetofautiana kwa kuwa huu uliangalia lugha ya matangazo katika majarida huku wetu ukichunguza lugha ya matangazo ya mchezo wa kandanda katika runinga na redio.

Vipashio vya Sarufi Amilifu katika usemi wa Kiswahili vilitafitiwa na Habwe (1989). Alibainisha nyenzo za kupatikana na kupitishwa kwa maana zinazotokana na mazungumzo ya kawaida miongoni mwa wazungumzaji wa Kimvita. Aliangalia maana iliyokusudiwa kutegemea muktadha na mahali. Utafiti huu umehusiana na wetu ulioangalia jinsi maana inavyopatikana na kuhamishwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kupitia lugha ya utangazaji. Aidha, Habwe (1999) ametafiti hotuba za kisiasa nchini Kenya. Aligundua kwamba sitiari na maswali ya balagha hutumiwa mno katika hotuba za wanasiasa. Aligundua pia kuwa maana za hotuba hizi huwa zaidi ya maana ya maneno yanayotumiwa na kwamba wanasiasa

hugeuza maana ili kutosheleza hali tofauti, matarajio na mahitaji ya hadhira yao. Utafiti wake ulimulika mshikamano, muwala na maana kipragmatiki. Kazi hii inalingana na yetu inayozingatia pragmatiki kama nguzo inayowezesha matumizi ya istilahi/msamiati wa taaluma na sajili tofauti kuibua maana katika sajili ya mchezo wa kandanda.

Michira (1993) katika uchambuzi wake wa matini za lugha ya wachuuzi wa soko la *Gikomba* na matangazo ya biashara redioni nchini Kenya, alizingatia mihimili ya nadharia ya elimu-mitindo kutambua sifa bainishi za kiisimu za mitindo hiyo na muundo wa lugha ya mitindo hiyo. Alinuia kuonyesha jinsi aina hizi mbalimbali za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinavyoingiliana na kutofautiana katika kutimiza malengo sawa ya kuwasilisha maana. Aligundua kuwa licha ya uchanganyaji msimbo kusheheni kazi hizo, zilikuwa na makosa mengi ya kissarufi. Utafiti huu unapatana na wetu kwa kiasi kwamba umehusisha uchambuzi wa matangazo ya redio. Tofauti ni kuwa utafiti wetu ulizingatia matangazo ya mchezo wa kandanda huku ikiegemea nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo.

Utafiti wa Tanaka (1994) ulihusu athari za fasiri potofu katika matangazo ya biashara. Alilinganisha matangazo kutoka nchi mbili zenye misingi baidifu kitamaduni na kiuchumi ambazo ni Uingereza na Japani. Aligundua kuwa utangazaji haufanywi kwa nia ya kuwauzia wateja bidhaa tu bali pia kujaribu kuwashawishi kumakinikia matangazo ambayo wangepuuza. Ulingano uliopo kati ya utafiti huu na wetu ni ule wa utangazaji na ufasiri wa maana. Tofauti ni kuwa

alizingatia matangazo ya biashara huku tukijikita katika matangazo ya mchezo wa kandanda.

Uchambuzi wa matini za vipindi vya redio kwa wakulima ulifanywa na Kiai (1996). Alilenga kuonyesha jinsi lugha ilivyotumiwa ili kueleweka na wakulima. Mtafiti huyu aligundua kuwa maneno mengi ambayo hayakueleweka na wakulima katika lugha za Kiswahili na Kikuyu ambazo zilitumiwa katika vipindi vya redio kwa wakulima yalitoholewa au kupewa maana iliyoeleweka katika jamii ya wakulima husika. Kwa sababu tulichunguza jinsi lugha inavyotumiwa katika matangazo ya mchezo wa kandanda ili kueleweka kwa mashabiki, kazi hii imehusiana na utafiti wetu.

Walya (1996) alichambua matini zinazohusu muundo wa mazungumzo katika sekta ya benki. Alinuia kubainisha ruwaza muhimu zinazojitokeza baina ya wahudumu na wateja na namna zinavyoathiri makubaliano kati yao. Aligundua kuwa mbinu au aina ya lugha inayotumiwa na wahudumu hunuia kuwateka na kuwashawishi wateja kuagiza na kulipia huduma za benki. Kwa mujibu wa haya, utafiti huu umelingana na wetu ulionuia kuchunguza aina ya lugha inayotumiwa katika kuibua na kuhamisha maana katika sajili ya mchezo wa kandanda.

Musau (2000) anasema kuwa lugha nyingi za kitaifa ikiwemo Kiswahili zina upungufu wa maneno au istilahi zinazohitajika kufanikisha mawasiliano katika

nyanja na taaluma za kisasa kama vile sayansi, sheria, biashara na spoti miongoni mwa nyingine. Hivyo basi, pana haja ya kukuza na kutia usasa lugha hizi ili ziweze kutimiza mahitaji haya mapya yanayoendelea kuchipuka. Anaeleza kuwa sababu mojawapo ya kufanya hivi ni kupanua matumizi ya maneno nje ya mawanda yake ya kawaida ili kunawirisha sajili zilizopo na hata kujenga nyingine mpya.

Akiangazia jinsi sajili ya mchezo wa kandanda inavyoweza kutumiwa kukuza misamiati katika lugha ya Kiswahili, anatazama lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda kama sitiari. Anasema kwamba kwa mbinu ya sitiari, maneno yanaweza kugeuzwa ili kuibua maana mpya. Anatumia lugha ya utangazaji kama mfano wa kushadidia sitiari kama mbinu muhimu katika welewa wa binadamu unaotumiwa kujenga maana na uhalisia mpya katika mazingira na maisha yake. Maandishi haya yalifaa utafiti wetu ambao nao ulishughulikia sajili ya mchezo wa kandanda. Tofauti iliyopo ni kuwa alijikita katika kuangalia lugha ya mchezo wa kandanda sawa na matumizi ya mbinu ya sitiari.

Ndung'u (2001) ametalii jinsi sifa bainifu za lugha ya mahubiri zinavyojitokeza katika sajili ya maibadani. Uchunguzi huu uliozingatia mtazamo wa kimtindo ulibainisha kuwa kuna ruwaza zilizosheheni sajili hii hasa matumizi ya mianzo ya maamkizi na yale ya maswali. Aidha, alibainisha kuwa sajili hii hushadidiwa na uchanganyaji msimbo. Utafiti wetu umehusiana na huu kwa kuwa tulidhamiria

kubainisha maana katika sajili. Hata hivyo, zimetofautiana kwa sababu utafiti wetu ulijikita katika sajili ya mchezo wa kandanda.

Uchunguzi wa matangazo ya biashara katika televisheni na redio ulifanywa na Aloo (2002). Alilenga kutambua mbinu za ushawishi zinazotumiwa na watangazaji wa bidhaa katika kuendeleza biashara zao na athari ambazo mbinu za lugha zilizotumiwa katika matangazo hayo zilitoa kwa hadhira. Utafiti wake uligundua ya kwamba maneno, picha na muziki ni mbinu changamano za ushawishi zinazotumiwa katika matangazo ya biashara. Alitambua pia kuwa tamathali za semi kama vile tashbihi na mbinu nyingine kama utohozi na kuchanganya msimbo hutumiwa katika matangazo ya biashara. Japo utafiti wetu ulihusisha matangazo ya redio kama huu ulivyofanya, unatofautiana nao kwa kudhamiria kuchunguza maana inavyobainishwa katika sajili ya mchezo wa kandanda.

Adero (2005) amechunguza uwezo wa lugha katika matini za kisiasa nchini Kenya. Ameonyesha jinsi misimamo ya wanasiasa inavyodhihirika wanapotumia lugha katika mazingira hayo. Waaidha, aligundua kuwa wanasiasa hutumia ujuzi na ulumbi uliojaa lugha pinde yenye tamathali kuushawishi umma kukubali sera zao. Utafiti huu unakaribiana na wetu uliohusu jinsi lugha inavyotumiwa kuibua maana katika mazingira maalumu. Tafiti hizi zimetofautiana kwa sababu Adero alilenga wanasiasa ilhali sisi tulilenga matangazo ya mchezo wa kandanda.

Kihara (2006) amechambua matini ili kubaini matumizi ya lugha katika sajili ya matatu. Mbali na kutambua sifa zinazobainisha sajili hii, amechanganua aina za maana zinazowasilishwa na matini zinazotumika na wahudumu pamoja na wateja. Utafiti huu unahusiana na wetu uliodhamiria kubaini jinsi maana inavyopatikana kupitia uhamishaji. Aidha, utafiti wetu umetumikiza nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo ambayo iliongoza utafiti wa Kihara. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kwa kuwa Kihara alilenga sajili ya matatu huku utafiti wetu ulilenga sajili ya mchezo wa kandanda.

Uchanganuzi wa matangazo ya biashara kwenye runinga ulifanywa na Maina (2011). Alinuia kuonyesha mbinu za mawasiliano zitumiwazo katika matangazo hayo. Alibainisha kuwa mbinu za kiisimu kama vile istiara, metonimu, takriri, kuchanganya na kuhamisha msimbo, utohozi, tanakali za sauti, tashbihi, uhuishi, chuku, nyimbo, semi na misimu na zisizo za kiisimu kama vile ishara za uso au macho, mkao wa mwili na mguso huhusishwa ili kuwawezesha watazamaji kufasiri maana zinazotokana na matangazo hayo. Utafiti huu umechangia utafiti wetu katika kuonyesha maana inavyofasiriwa na kwa kubainisha mbinu za mawasiliano zinazofanikisha uibuaji na ufasiri wa maana. Kwa kuwa utafiti wetu ulihusu matangazo ya mchezo wa kandanda, unatofautiana na wa Maina uliozingatia matangazo ya biashara.

Munyasa (2012) alilenga kutambua sifa zinazofanya lugha ya mikahawa ya *Eastlands* kuwa na upekee. Alidhamiria pia kubainisha maana zinazowasilishwa

na lugha inayotumiwa katika mikahawa hiyo. Aligundua kwamba lugha asili za wakazi wa eneo la *Eastlands* hutumiwa kwa uchangamano katika kuathiri mkondo wa maana zinazotokana na matumizi yake. Utafiti huu umechangia wetu ambao ulihusu lugha inavyotumiwa kuibua maana katika sajili mahsusi. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika sajili ya hoteli lakini wetu uliangalia sajili ya mchezo wa kandanda.

**1.7 Misingi ya Kinadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo (SAM). Nadharia hii, iliyoasisiwa na Halliday (1985) inategemea imani kuwa kama tukio la kijamii, lugha iliundwa kwa minajili ya mawasiliano. Inaangalia lugha sawa na mfumo au mtandao wa maana unaowakilishwa kwa maumbo ya kisarufi. Nadharia hii hivyo basi inatukuza maana dhidi ya maumbo. Kwa mtazamo huu, mfumo wa lugha huangaliwa sawa na uamilifu wa maneno. Sarufi Amilifu Mfumo hujivunia uyakinifu wa kiisimu na uhalisia wa kipragmatiki na wa kisaikolojia ambazo kwa pamoja huwiana katika udokezi wa maana.

Sarufi Amilifu Mfumo hutazama kishazi kama kipashio kidogo zaidi au matini ya kimsingi inayotumiwa kuchunguza na kuchanganua lugha. Kipashio hiki kinanasibishwa na sentensi sahili. Katika kuchunguza na kuchanganua lugha, Sarufi Amilifu Mfumo inatambua na kusuka tanzu tatu za kiisimu ambazo ni sintaksia, semantiki na pragmatiki.

Cook na Nelson (1996) wanafafanua sintaksia kama taaluma ya kiisimu inayoshughulikia kanuni za uundaji na uchanganuzi wa maneno, virai na sentensi. TUKI (1999) inaeleza sintaksia kama tawi la sarufi linaloshughulikia uchanganuzi wa mpangilio na uhusiano wa vipashio katika sentensi. Habwe na Karanja (2004) wanatazama sintaksia kama utanzu wa kiisimu unaoshughulika na muundo wa sentensi na elementi nyingine zinazounda sentensi kama vile kategoria za maneno, vikundi na vishazi. Kimsingi, mtazamo huu humithilisha sintaksia na uhusiano wa maumbo mintarafu ya mpangilio wake katika kishazi. Hivi ni kusema kuwa sintaksia inahusika na uamilifu wa maumbo kama yanavyojitokeza katika matini. Kwa mujibu wa uamilifu huu, kipashio kinaweza kujitokeza kama kiima, kiarifu, shamirisho na chagizo.

Kwa mujibu wa Ullmann (1972), semantiki ni nadharia inayoshughulikia sayansi ya maana. Fromkin na Rodman (1978) wanaeleza semantiki kama uchunguzi wa maana ya maneno, vishazi na sentensi. Semantiki hurejelea uhusiano wa maana na maumbo. Kwa jumla, semantiki hujitokeza kama tagaa la isimu linalohakiki maana zilizo katika lugha na namna maana hizo zinavyohusiana. Inashughulikia sifa na dhima mbalimbali za vipashio vinavyounda kishazi.

Levinson (1983) anaeleza pragmatiki kama tapo la kiisimu linaloshughulikia uhusiano kati ya kanuni za vipashio vya lugha na muktadha wa matumizi ya lugha hiyo. Pragmatiki inahusika na muktadha mpana wa lugha na mawasiliano. Inarejelea uhusiano wa maana na msemaji. Kama amali ya urejeshi penyezi,



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

pragmatiki huhakiki ujumbe unaodhamiriwa kuwasilishwa na usemi. Kwa maelezo haya, pragmatiki hujitokeza kama utanzu wa kiisimu unaohusika na jinsi wasemaji wa lugha huitumia katika mazingira halisi. Pragmatiki huangazia thamani ya kiarifu katika muktadha mpana wa uamilifu wa lugha kimawasiliano. Inaangalia lugha kama mfumo wa maana kutegemea muktadha wa mawasiliano; kwamba kauli yoyote inayotolewa hueleweka vyema ikihusishwa na mada inayozungumziwa, taaluma, ujuzi na hali ya wahusika na mahala pa kutokea mazungumzo.

Sarufi Amilifu Mfumo inaangalia kipashio kwa namna ambavyo inakidhi mahitaji ya umilisi mawasiliano na utoshelevu wa kipragmatiki. Hivi ni kusema kwamba utendakazi wa lugha kimuktadha hukamilika tu pale ambapo masuala ya kipragmatiki yanapozingatiwa.

Halliday (2004) anaeleza kuwa tanzu hizi tatu za kiisimu huhusiana, hujengana na kudhitibiana pakubwa. Kwa mtazamo huu, hakuna utanzu unaoweza kujitenga wala kujitosheleza bila mwingine. Hivyo basi, lugha huwa ishara ya kufaulisha mawasiliano pale ambapo pragmatiki hudhibiti semantiki, nayo semantiki ikidhibiti sintaksia. Katika kutimiza mahitaji haya, Sarufi Amilifu Mfumo imetambua aina tatu za maana: maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi.

Maana dhanishi huwakilisha maana kamili au ya kimsingi ya dhana au hali halisi kama zinavyojitokeza katika akili au mawazo ya binadamu. Hii ni safu ya maana inayotokana na uwezo wa msemaji kutambua maudhui katika lugha kimantiki.

Yule (1996) anaeleza maana dhanishi kama jumla ya sifa muhimu au za kimsingi zinazohusiana na matumizi halisi ya neno. Lyons (1981) anasema kuwa maana dhanishi inaweza kuwakilishwa katika kiwango cha leksia na kishazi kwa kupambanua sifa zake bainifu. Maana dhanishi inaangaliwa sawa na uamilifu wa lugha katika kusimba tajriba za kibinafsi za msemaji na zile za kitamaduni katika jamii anamoishi. Kwa kuwa maana dhanishi hujitokeza kama maana asili inayobainisha utendakazi wa lugha, inaendeleza utanzu wa semantiki.

Maana tagusani huangazia jinsi lugha inavyotumiwa kuleta utangamano miongoni mwa watumiaji wa lugha kwa uzingativu wa masharti na vikwazo vya kijamii. Aina hii ya maana inajulikana pia kama maana jamilishi au maana husishi. Maana tagusani huwawezesha watumiaji wa lugha kuasisi, kuimarisha na kudumisha masharti ya mahusiano ya kijamii. Mahusiano haya huchukua mkondo wa ushirikiano na utambulisho wa watumiaji wa lugha na kundi lao. Maana tagusani hubainika kama amali tekelezi ya lugha inayoangalia matumizi ya lugha sawa na tendo la usemi linalotekelezwa na msemaji ili kujieleza na kueleweka na msikilizaji.

Inabainika kuwa maana tagusani ambayo huwa na uamilifu husishi inatumiwa kuyakinisha maana dhanishi. Huku maana dhanishi ikiwakilisha dhati ya ujumbe, maana tagusani huangazia kaida zinazodumishwa na jamii ili kudhibiti mawasiliano. Hivyo basi, inaendelezwa katika utanzu wa pragmatiki. Maana dhanishi na maana tagusani hujitokeza kama amali za kimsingi ambazo utoshelevu wa dhima zake hutegemea amali ya maana matinishi.

Maana matinishi huhusika na kanuni za kisarufi zinazoelekeza matumizi ya lugha kwa lengo la kusarifu ujumbe na kufanikisha mawasiliano. Inazingatia usarifu na ukubalifu wa sentensi pamoja na mshikamano katika kauli ndefu. Maana matinishi hutimiza haya kwa kuoanisha muwala wa matumizi ya lugha na mahitaji pamoja na mshikamano na mazingira, muktadha na kaida za mawasiliano. Ina dhima ya kuwakilisha maana inayodhamiriwa na msemaji bali si yale yanayosemwa waziwazi. Maana matinishi ambayo ina uwiano na utanzu wa sintaksia hutimiza haya kwa mshikamano na maana dhanishi na maana tagusani.

Kwa mujibu wa haya, nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo inatambuliwa kwa mihimili ifuatayo:

Lugha huwa na maana dhanishi/tambuzi.

Lugha huwa na maana tagusani/jamilishi/husishi.

Lugha huwa na maana matinishi.

Mihimili hii ndiyo iliyotumiwa kuchunguza mada yetu ya utafiti na kuchanganua data iliyokusanywa.

### 1.8.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulihusisha mbinu ya usikilizaji. Katika kusikiliza, mtafiti alirekodi matangazo ya moja kwa moja ya mchezo wa kandanda na taarifa zinazohusu mchezo huu kwenye runinga na redio ndipo baadaye akadondoa data na kuzichambua.

### 1.8.1 Uteuzi wa Sampuli

Data inayohusu utafiti huu kutoka nyanjani iliteuliwa sampuli. Uteuzi wa kimakusudi ulitumiwa ili kupata sampuli lengwa. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), usampulishaji kimakusudi hutumiwa pale ambapo mtafiti hulenga kupata kundi fulani analoonelea kuwa lina uwezo wa kuzalisha data zenye sifa na habari anazohitaji. Maelezo haya yanaafikiana na ya Orodho (2005) na Mugenda na Mugenda (1999) wanaosema kuwa usampulishaji kimakusudi ni uamuzi wa mtafiti wa kuteua moja kwa moja idadi ndogo iliyo na uwezo wa kudhihirisha tabia zinazohitajika na utafiti wake. Hivyo basi, mbinu hii ilimwezesha mtafiti kufanya uteuzi wa moja kwa moja ili kupata sampuli iliyowakilisha idadi yote kwa kutoa taarifa muhimu alizohitaji.

Mtafiti alihusisha usikilizaji wa kauli za matangazo ya moja kwa moja ya mchezo wa kandanda yanayopeperushwa kwenye vituo vya redio kwa lugha ya Kiswahili nchini kote. Vituo vya redio vilivyohusishwa ni *Radio Citizen, Radio Jambo,*

*Radio Maisha, KBC Radio Taifa, Q FM* na *Milele FM.* Taarifa zinazohusu mchezo huu kwenye vituo hivi vya redio zilichambuliwa. Aidha, vituo vya runinga vilivyohusishwa katika usikilizaji wa taarifa za mchezo wa kandanda ni *Nation Television (NTV), Q Television (Q TV) Kenya Television Network (KTN), Kenya Broadcasting Corporation (KBC)* na *K 24 Television (K 24).*

Kati ya timu 16 zinazoshiriki katika ligi kuu nchini Kenya, uchunguzi huu ulishirikisha matangazo ya moja kwa moja ya mechi za timu 5 ambazo ni Gor Mahia, AFC Leopards, Tusker, Ulinzi na Sofapaka. Timu hizi ziliteuliwa kimakusudi kwa sababu ni pinzani na maarufu zaidi kwa kushikilia nafasi za mwanzo katika Jedwali la ligi hasa kuanzia mwaka wa 2012 hadi sasa. Hali hii imezifanya timu hizi kuwa na wafuasi wengi zaidi wanaopenda kusikiliza matangazo ya mechi zake. Idadi hii inaoana na kiwango cha sampuli cha 30% cha idadi jumuifu kinachopendekezwa na Kothari (2008) kuwa na uwezo wa kuzalisha data yenye tabia wakilishi.

Mbinu ya uteuzi wa kimaksudi ilitumiwa pia katika usikilizaji wa matangazo ya mechi zinazohusu timu maarufu za Uingereza zilizo na ufuasi mkubwa nchini Kenya. Timu hizo ni Arsenal, Manchester United, Chelsea, Manchester City na Liverpool. Licha ya matangazo ya mechi zinazohusisha timu hizi kupeperushwa moja kwa moja kwenye vituo vya redio vinavyotangaza kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya, ilitarajiwa kuwa data iliyotokana na sampuli hii iliweza kudhihirisha

tabia na kutoa taarifa na data zilizonufaisha utafiti huu. Hali kadhalika, mtafiti alisikiliza taarifa za michezo kutoka vituo mbalimbali vya runinga na redio vilivyotajwa.

### 1.8.2 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mtafiti alihusisha mbinu ya usikilizaji kukusanya data. Mtafiti alisikiliza matangazo ya mchezo wa kandanda yanayopeperushwa moja kwa moja kwenye redio huku akidokoa data muhimu. Usikilizaji wa habari za mchezo wa kandanda kwenye vituo hivi vya redio na runinga ulihusishwa pia. Baadhi ya matangazo haya yalirekodiwa kwa kinasa sauti na kusikilizwa tena baadaye ili kuchambuliwa.

Data iliyokusanywa ilijumuisha misamiati, istilahi, virai, vishazi na sentensi. Jinsi vipashio hivi vinavyounda matini zenye mshikamano na kutoa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda ilishughulikiwa.

### 1.8.3 Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa na kunakiliwa na mtafiti nyanjani iliainishwa kama misamiati, istilahi, virai, kauli na vishazi. Data hii ilipangwa na kuchanganuliwa ili kutambua miundo, mshikamano wa matini na maana zilizowasilishwa. Uchanganuzi huu ulifanywa kwa uzingativu wa mihimili ya nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo ili kutolewa maana. Uchanganuzi wa data hizi uliongozwa pia na maswali ya utafiti na malengo ya utafiti kama yalivyoorodheshwa katika uk 5-6.

### 1.8.4 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya uchanganuzi wa data yamewasilishwa kwa njia ya maelezo yaliyojumuisha matumizi ya majedwali. Maelezo yamehusu maumbo yaliyodhihirika kama msamiati, istilahi, virai, kauli, maswali na vishazi. Uchanganuzi huu umeainisha data katika vikundi tofauti kulingana na maswali ya utafiti na malengo ya utafiti. Utoshelevu wa kimaelezo uliojumuisha utangulizi na mahitimisho ya kila sura umehakikishwa.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imeangazia mambo ya kimsingi yanayojenga usuli wa utafiti huu. Vipengele muhimu vya utangulizi kama vile usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti huu vimeshughulikiwa katika sehemu ya kwanza. Sehemu ya pili ya sura hii imepitia misingi ya kinadharia na mapitio ya maandishi. Mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, mbinu zilizotumiwa kukusanya na kuchanganua data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti zimebainishwa katika sehemu ya tatu. Tumeshughulikia mbinu za mawasiliano zinazotumiwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda katika sura inayofuata.

# SURA YA PILI

# MBINU ZA MAWASILIANO KATIKA UTANGAZAJI WA MCHEZO WA KANDANDA

## 2.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imejenga msingi wa utafiti huu kwa kuangazia usuli na suala la utafiti. Katika sura hii tumechanganua data tuliyokusanya ili kubainisha mbinu za mawasiliano zinazotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda ili kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji wao. Wasikilizaji hawa ambao ndio mashabiki wa timu zinazohusika kwenye mchezo hupata ujumbe kuhusu mwendelezo na matukio ya mchezo huu kupitia utangazaji wa moja kwa moja kwenye redio. Hali kadhalika, ujumbe huu huwafikia kupitia matangazo ya taarifa za mchezo huu kwenye redio na runinga. Hivi ndivyo vyombo vya uwasilishaji na upokezi wa matukio ya mchezo wa kandanda. Kupitia matangazo ya mchezo huu kwenye vyombo hivi, watangazaji wa mchezo huu hunuia kuwasiliana na hufaulu kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji wao.

Kwa mujibu wa Beeman (1977), mawasiliano ni mfanyiko wenye lengo la kuwasilisha ujumbe kwa viumbe ili kubadili tabia na mienendo ya wahusika wote kwenye mfanyiko huo. Lyons (1977) naye anafafanua dhana hii kama uwasilishaji wa ujumbe kwa kutumia mfumo fulani wa uashiriaji. Maoni haya yanaoana na yale ya Berelson na Steiner (1969) wanaofafanua mawasiliano kama uwasilishaji wa maoni, hisia na ufundi wa kutumia ishara. Wanataja maneno, picha na michoro kama baadhi ya ishara zinazotumiwa kufanikisha mawasiliano.

Lyons (1977) anasema kuwa lugha ndiyo mfumo unaotumiwa mno na binadamu kuwasiliana, japo kuna mifumo mingine. Morreale (2004) anaeleza lugha kama mfumo wa ishara za kiusemi unaomwezesha binadamu kuzua taarifa na matamshi zenye maana. Ishara hizi za kiusemi zinaweza kuandikwa au kutamkwa. Tendo la usemi hufaulishwa kwa kuandamanisha ishara za sauti kama vile kupaaza sauti na kasi katika utamkaji na ishara zisizo za kiusemi kama vile ishara za uso, ishara za mikono, miondoko, misogezo ya mwili na hata vifaa halisi ambavyo wanajamii hukubaliana kuwa na maana. Hata hivyo, lugha ya matangazo ya mchezo wa kandanda hutegemea tu ishara za kiusemi.

Sababu kuu ya utangazaji wa mchezo wa kandanda ni hitaji la kuwawezesha wasikilizaji au mashabiki wasioweza kutazama mchezo huu moja kwa moja kuufuatilia unavyoendelea na kupata matokeo yake punde tu unapomalizika. Ili kufikisha ujumbe kwa njia mwafaka zaidi kwa wasikilizaji, watangazaji wa mchezo wa kandanda huteua na kutumia mbinu fulani. Mbinu hizi za mawasiliano hujitokeza kama matumizi ya lugha kwa namna inayoeleweka vyema kwa wasikilizaji. Hivi ni kusema kuwa watangazaji huteua na kutumia lugha kwa njia inayowavutia na kuamsha hamu ya wasikilizaji wao ili wasikilize matangazo hayo kwa muda wote wa mchezo. Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa imeonyesha mbinu zifuatazo.

## 2.1 Utohozi

Appel na Muysken (1987) wanaeleza utohozi kama namna ya ukopaji na uingizaji wa sauti, ishara, maendelezo na maana ya maneno kutoka lugha moja hadi nyingine. Hivi ni kusema kwamba neno hupachikwa umbo la maneno ya lugha pokezi ili kupata maneno mkopo. Wanasema kwamba ni nadra sana kupata lugha isiyoazima kwa sababu hakuna lugha wala utamaduni wowote unaojitosheleza.

Kulingana na Wamitila (2003b), utohozi ni uingizaji wa maendelezo ya lugha moja kama vile Kiswahili katika maneno ya lugha nyingine. Anasema kwamba kama zilivyo lugha nyingine za Kibantu, maneno mengi ya Kiswahili huendelezwa kwa utaratibu wa mfuatano wa konsonanti na irabu ambapo neno huishia irabu, japo linaweza kuanzia konsonanti au irabu. Hata hivyo, ni jambo la kawaida kupata maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyofuatisha irabu mbili au tatu mtawalia hasa yakiwa yenye asili ya Kiarabu.

**Jedwali 2.1: Utohozi wa Nomino Zinazohusu Wachezaji na Wasimamizi**

| **Neno Lililotoholewa** | **Matini** | **Neno asilia** | **Lugha changizi** |
|---|---|---|---|
| Staa | *Staa* wa Arsenal, Ozil, aliyeng'ara katika mchuano dhidi ya Chelsea anatazamiwa kuendelea kuonyesha makali yake katika mchuano wa leo. | Star | Kiingereza |
| Supastaa | *Supastaa* huyu wa Real Madrid, anapigiwa upatu wa kutwaa tuzo ya mchezaji bora duniani baada ya kuikosa kwa miaka mitatu | Super star | Kiingereza |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | iliyotangulia. | | |
| Winga | *Winga* huyu wa AFC Leopards, Were, anakwenda kasi kama swara. | Winger | Kiingereza |
| Beki | Msikilizaji *beki* huyu wa timu ya AFC Leopards, Shikokoti, hapitikiki, ni mgumu kama mwamba. | Back liner | Kiingreza |
| Difenda | *Difenda* huyo anaingia pale na kuondoa mpira katika eneo la hatari, potelea mbali. | Defender | Kiingereza |
| Straika | Jamani *straika* yule Welbeck ametia bao maridadi wavuni, anatisha huyu. | Striker | Kiingereza |
| Refa | *Refa* amemlisha mchezaji Kompany kadi ya njano kwa kuonysha mchezo mbaya. | Referee | Kiingereza |
| Golii; Kipa | Ananyunyiza pale mpira mrefu kwenye lango-oo, *golii* anaruka na kuushika maridadi kabisa. *Kipa* huyu wa Tusker anaunyaka kama nyani na kulala nao. | Goalie; Keeper | Kiingereza |
| Fowadi; Goli | *Fowadi* huyu amefunga *goli* nyingi kuliko wachezaji wote katika kampeni za msimu huu. Hili ni bao lake la kumi na tatu katika mechi ishirini na tano msimu huu. | Forward; Goal | Kiingereza |

Maneno mengi yaliyotoholewa katika lugha ya Kiswahili na kutumika katika utangazaji mchezo wa kandanda ni yale yenye asili ya Kiingereza. Maneno haya yamefuata utaratibu wa lugha ya Kiswahili ambapo konsonanti hufuatwa na irabu

na kisha neno kuishia irabu kama anavyosema Wamitila (2003b). Jedwali lifuatalo linaonyesha data iliyotoholewa na watangazaji wa mchezo wa kandanda katika utangazaji wao.

Kutokana na data iliyochanganuliwa katika jedwali hili, utohozi wa maneno yanayohusu wachezaji ni kama vile *staa, supastaa, winga, beki, difenda, strika, fowadi* na *kipa*. *Staa* limetoholewa kutoka neno la Kiingereza 'star' lenye tafsiri ya nyota. Limetumiwa na watangazaji kumaanisha mchezaji hodari. Neno *supastaa* ni utohozi wa 'super star' linalotumiwa kumaanisha mchezaji hodari sana na maarufu. *Winga* ni utohozi wa 'winger' lenye maana ya mchezaji wa pembeni mwa uwanja katika safu ya mbele, ama upande wa kulia au kushoto.

*Beki* limetoholewa kutoka neno 'back' lenye maana ya nyuma nalo *difenda* ni utohozi wa 'defender' linalomaanisha mlinzi. Maneno haya yanatumiwa kumaanisha mchezaji wa safu ya nyuma anayelinda eneo la lango lake ili kuwazuia wachezaji wa timu pinzani wasifunge. Neno *kipa* limetoholewa kutoka 'keeper' lenye maana ya mtunzaji. Neno hili linatumiwa katika matangazo ya mchezo wa kandanda kumrejelea mchezaji anayesimama kati ya lango ili kuzuia mpira usiingie langoni mwake akitumia mikono au sehemu yoyote ya mwili wake. *Straika* ni utohozi wa 'striker'. Linamaanisha yule anayeshambulia. *Fowadi* limetoholewa kutoka neno 'forward' lenye kumaanisha mbele. Maneno haya yanatumiwa kuwarejelea wachezaji wa safu ya mbele wenye jukumu la kufunga mabao.

**Jedwali 2.2: Utohozi wa Nomino Zinazohusu Klabu, Usajili wa Wachezaji na Wakufunzi**

| **Neno Lililotoholewa** | **Matini** | **Neno asilia** | **Lugha changizi** |
|---|---|---|---|
| Mechi; Klabu | Msikilizaji mpendwa, *mechi* ya leo kati ya *klabu* hizi inatazamiwa kuwa ngumu sana. | Match; Club | Kiingereza |
| Ligi | *Ligi* ya msimu huu umekuwa ngumu kwani timu nne za kwanza katika jedwali la ligi zimetengwa na alama tano peke yake. | League | Kiingereza |
| Timu | *Timu* hii ya Gor Mahia inajivunia washambulizi wakali kama vile Sserenkuma, Kenga na Blackberry Odhiambo. | Team | Kiingereza |
| Meneja; Kocha | *Meneja* huyu wa timu ya Man City alipigwa marufuku ya mechi mbili za Klabu Bingwa Barani Ulaya baada ya matamshi yake dhidi ya refarii. Hii leo *kocha* huyu anarejea kwenye benchi ya timu yake. | Manager; Coach | Kiingereza. |
| Bosi | *Bosi* wa klabu ya Gor Mahia Bob Williams alinukuliwa akisema kuwa amenoa silaha zake kwa makabiliano ya wikendi hii dhidi ya adui zao AFC Leopards. Haya leo ni leo, wakati huu uliosubiriwa kwa hamu na ghamu ndio huu. | Boss | Kiingereza |
| Ofa | Timu hii ya Man United ilitoa *ofa* ya kitita cha pauni milioni 27 kumnunua kiungo huyu matata Mata kutoka | Offer | Kiingereza |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | mahasimu wao Chelsea. | | |
| Dili | Mchezaji huyu mahiri alinunuliwa katika *dili* iliyogharimu timu yake pauni milioni arobaine na mbili. | Deal | Kiingereza |

*Timu* limetoholewa kutoka neno la Kiingereza 'team' huku neno *klabu* likitoholewa kutokana na neno 'club'. Maneno haya yaliyo na maana ya kundi yanatumiwa katika lugha ya utangazaji wa kandanda kumaanisha kundi au idadi fulani ya wachezaji na wakufunzi lililosajiliwa kushiriki katika mchezo wa kandanda. Neno *mechi* ambalo ni utohozi wa neno 'match' linatumiwa kurejelea mchezo uliopangwa kuendelea kati ya timu husika. Ligi ni utohozi wa neno 'league' linalorejelea ratiba iliyotayarishwa ili kushirikisha timu kadha za kandanda katika mchezo.

*Kocha, meneja* na *bosi* yametoholewa kutoka maneno 'coach', 'manager' na 'boss' mtawalia. *Kocha* ni yule anayefunza mwingine jinsi ya kufanya kitu. *Meneja* ni mtu anayesimamia utekelezaji wa shughuli fulani na *bosi* ni mtu mwenye cheo cha juu katika shirika fulani. Maneno haya mawili yanatumiwa na watangazaji kurejelea mkufunzi wa mchezo wa kandanda ambaye pia husimamia shughuli nyingine zinazohusu wachezaji na klabu kwa jumla. *Refa* ni utohozi wa neno 'referee' lenye kumaanisha muamuzi au msimamizi wa mchezo wa kandanda ndani ya uwanja.

*Ofa* na *dili* ni istilahi zinazotumiwa katika shughuli za usajili wa wachezaji. Maneno haya yametoholewa kutoka maneno ya Kiingereza 'offer' na 'deal' mtawalia. Neno *ofa* hutumiwa kurejelea kiasi cha fedha ambazo klabu na wamiliki wa timu mbalimbali wako tayari kulipa ili kusajili au kupata huduma za wachezaji kutoka timu nyingine. *Dili* hutumiwa kumaanisha kiasi cha fedha kilichoafikiwa na timu inayomuuza na ile inayomnunua mchezaji.

**Jedwali 2.3: Utohozi wa Nomino Zinazohusu Hali ya Mchezo**

| Neno Lililotoholewa | Matini | Neno asilia | Lugha changizi |
|---|---|---|---|
| Fauli | Mlinzi wa timu ya Sofapaka amefanya *fauli* katika eneo la hatari. Mpira utapigwa kuelekea lango lao. | Foul | Kiingereza |
| Penalti | Kipa amejipinda kama upinde na kuokoa *penalti* ile. | Penalty | Kiingereza |
| Pasi | Kiungo wa timu ya Sofapaka amemuandalia mshambulizi wao huyu Baraza *pasi* murua iliyozalisha bao la ushindi. | Pass | Kiingereza |
| Presha | Kocha wa klabu ya Manchester United mwenzanu ana *presha* ya kushinda mechi hii ya leo ili kuongeza nafasi ya kuingia nne bora au apigwe kalamu. | Pressure | Kiingereza |
| Krosi | Winga huyo ametoa *krosi* kali iliyowatatiza madifenda na kujifunga. Hilo ni bao la zawadi msikilizaji wangu. | Cross | Kiingereza. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kona | Anachanja pale *kona* nzuri kutoka wingi wa kulia hadi kwenye eneo la penalti- ii, bado! | Corner | Kiingereza |
| Benchi | Wachezaji hawa waliotegemewa sana msimu uliopita kama Kagawa na Nani wanasugua *benchi* baada ya kiwango cha mchezo wao kushuka. | Bench | Kiingereza |
| Fainali | Timu hizi hasimu zinakutana tena katika *fainali* za mwaka za kombe la GoTV. | Finals | Kiingreza |

Maneno *penalti, faulo, pasi presha, kona* na *krosi* yanatoholewa na watangazaji wa mchezo wa kandanda kuelezea mchezo unavyoendelea na matukio yanayoandamana nayo uwanjani. Neno *Penalti* linalomaanisha adhabu inayotolewa kutokana na kosa hutumiwa kurejelea mpira wa adhabu unaopigwa langoni moja kwa moja iwapo mchezaji wa timu pinzani amechezewa visivyo katika eneo la yadi kumi na nane. *Pasi* hutumiwa kumaanisha mpira unaopitishwa au kufikishwa kwa ustadi kutoka mchezaji mmoja hadi mwingine. Neno *presha* lenye maana ya shinikizo hutumiwa kurejelea uzito au joto alilo nalo mchezaji au mkufunzi ili kucheza vizuri na kufunga bao au kupata matokeo bora mtawalia. *Fainali* ambalo ni utohozi wa neno 'finals' linatumiwa kurejelea awamu ya mwisho wa mchezo ambapo ushindi wa taji lazima utwaliwe na timu fulani.

Neno *benchi* lenye maana ya kiti kirefu kinachotengenezwa kwa mbao limetoholewa na kutumiwa kumaanisha ama wachezaji wa ziada au kundi la wakufunzi, wasimamizi na viongozi wa klabu fulani. *Krosi* limetoholewa na kutumiwa katika utangazaji kumaanisha mpira unaopigwa kutoka pembezoni

mwa uwanja kuelekea eneo la lango, nalo *kona* ni mpira wa adhabu unaochezwa kutoka kwenye ukingo wa uwanja iwapo mchezaji wa timu hiyo ametoa mpira nyuma ya lango lake.

Matumizi ya maneno haya katika majedwali 2.1, 2.2 na 2.3 na maelezo yaliyofuatia yanaonyesha ufinyanzi na upanuzi wa maana yake ya kimsingi ili kutosheleza haja za lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda. Matumizi haya yanalingana na mhimili mojawapo ya nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo (SAM) inayosema kwamba lugha huwa na maana dhanishi.

Kulingana na Leech (1966), utohozi huhusishwa katika lugha ya utangazaji kama chambo cha kuvutia au kuteka nadhari ya hadhira ili iweze kujiandaa kusikiliza na kutambua ujumbe uliopo. Appel na Muysken (1987) wanasema kuwa utohozi ni mojawapo ya mbinu za upanuzi wa lugha kupitia uundaji wa msamiati usio na visawe katika lugha pokezi na wakati mwingine kama vipo, matumizi yake hayajazoeleka au hayaeleweki na wengi. Wanaendelea kusema kwamba mbali na kurahisisha matamshi, utohozi huonyesha kuwa matumizi yake yamekubalika na kuzoeleka katika lugha pokezi.

Maoni haya yanaungwa mkono na Njogu na wengine (2006) wanaosema kuwa utohozi ni njia mojawapo ya uundaji au ujengaji wa istilahi na ukuzaji wa lugha. Ujengaji huu huwa na lengo la kutosheleza haja za mawasiliano katika nyanja mpya na ambazo awali zilikuwa hazijashughulikiwa kwa kutumia lugha fulani.

Aloo (2002) anasema kuwa utohozi ni njia mojawapo ya kukuza msamiati wa lugha. Aligundua kuwa maneno yalitoholewa kutoka lugha ya Kiingereza na Kiswahili hadi lugha za kwanza kama vile Kikuyu na Kidholuo. Utafiti wa Kihara (2006) kuhusu matumizi ya lugha katika sajili ya matatu unatazama utohozi kama ukopaji au uswalihishaji wa maneno kutoka lugha na tamaduni nyingine. Anaendelea kusema kuwa utohozi husababishwa na maingiliano marefu ya kitamaduni ya wasemaji wa lugha zinazohusika. Akizungumzia utohozi wa moja kwa moja wa maneno na ule wa dhana na sifa za vitu kama inavyojitokeza katika lugha ya mikahawa ya *Eastlands*, Munyasa (2012) anaeleza kuwa hali hii hutokana na mazoea ya wenyeji wa mitaa hii kuchanganya lugha wanaporejelea vitu vinavyohusishwa na wakazi hawa.

Maina (2011) alitambua utohozi wa maneno ya Kiingereza kwa Kiswahili. Anasema kuwa utohozi hutumiwa kama mbinu mojawapo ya mawasiliano katika matangazo ya runinga nchini Kenya iwapo dhana husika haina kisawe na iwapo kipo, hakitumiwi au hakieleweki na wengi. Anaendelea kusema kuwa japo utohozi hutumiwa kupata msamiati wa kuelezea dhana ngeni na kuifanya hadhira lengwa kujitambulisha na lugha itumiwayo katika tangazo, wakati mwingine hutumiwa kiholela hasa na wale wazungumzaji wenye ujuzi na umilisi wa lugha zaidi ya moja. Hivi ni kusema kuwa kwa wazungumzaji hawa, utohozi ni tukio la kawaida katika mazungumzo. Hata hivyo, matumizi ya utohozi katika matangazo ya mchezo wa kandanda huwa na dhima kimawasiliano.

Mbali na kurahisisha matamshi na mawasiliano kati yao na wasikilizaji, utohozi huwa mbinu maarufu miongoni mwa watangazji wa mchezo wa kandanda kwa sababu asilimia kubwa ya mashabiki na wasikilizaji wa mchezo huu huwa vijana wa kizazi hiki wanaosisimkia mtindo huu wa lugha kama nembo ya usasa. Hivi ni kusema kwamba watangazaji wa mchezo huu hupenda kuhusisha mbinu hii ili kujitambulisha na kujinasibisha na umma mkubwa wa mashabiki wasikilizaji mbali na hitaji la kueleza dhana ngeni zisizo na visawe katika lugha ya Kiswahili. Kwa njia hii, utohozi huipa lugha uamilifu husishi unaotambuliwa na nadharia ya SAM kama maana tagusani. Inajitokeza pia kwamba watangazaji hawana muda wa kutosha wa kutafuta tafsiri mwafaka au visawe vya maneno haya kwa sababu ya kasi ya mchezo wa kandanda ambao lazima wadumishe katika utangazaji wao.

## 2.2 Uchanganyaji Msimbo na Ubadilishaji Msimbo

### 2.2.1 Uchanganyaji Msimbo

Mbinu nyingine inayohusishwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda ni uchanganyaji msimbo. Ipara na Maina (2008) wanafafanua uchanganyaji msimbo kama hali ambapo wazungumzaji hutumia lugha moja kisha kutoka kidogo katika lugha hiyo na kuingilia lugha ya pili au ya tatu kwa muda mfupi kabla ya kurejelea lugha ya awali. Maelezo haya yanaafikiana na ya Buliba na wengine (2006) na Wamitila (2003b) wanaosema kwamba uchanganyaji msimbo ni utumizi wa maneno ya lugha mbili au zaidi katika matini moja au hali moja ya mazungumzo. Richards na wengine (1985) nao wanaeleza dhana hii kama uchopekaji wa maneno ya lugha moja katika usemi ulio katika lugha nyingine. Maoni haya yanalingana na

yale ya Muysken (2000) anayesema kuwa uchanganyaji msimbo hutokea katika mazingira yote ambapo kipengele kimoja cha kileksika na sehemu ya kisarufi kutoka lugha mbili tofauti hutokea kwa pamoja katika sentensi moja.

Deuchar na Quay (2000) wanasema kuwa kuchanganya msimbo aghalabu huanzia miongoni mwa watoto wanaojikuta katika jamii au mazingira yenye lugha zaidi ya moja. Wanasema kuwa katika umri mdogo, ujuzi wa lugha miongoni mwa watoto huongezeka na kubadilika haraka. Wanaeleza kuwa watu wazima nao hawachanganyi msimbo kwa sababu ya ujuzi wao mdogo wa lugha moja tu bali pia kwa sababu ya uwezo mkubwa wa baadhi yao kutumia zaidi ya lugha moja kwa ufasaha.

Utafiti wa Pfaff (1979) kuhusu ulumbi miongoni mwa watu wazima ulionyesha kuwa kuchanganya msimbo hutokea kati ya sentensi kama ishara ya kipimo cha uwezo wa juu wa ulumbi wao. Aloo (2002) anaonelea kuwa uchanganyaji msimbo hutokea pale ambapo badala ya kutafsiri au kuunda istilahi ya kurejelea dhana husika, maneno ya lugha nyingine hutumiwa kwa sababu yamezoeleka na kutambulika kwa urahisi.

Berk-Seligson (1986) anaeleza kuwa kuchanganya msimbo pia kunahusishwa na dhana kuwa lugha moja haijazoeleka au inatawaliwa na nyingine. Nchini Kenya, Kiingereza kinaonekana kutawala Kiswahili hata baada ya lugha ya Kiswahili

kuteuliwa kuwa lugha rasmi ya kwanza katika katiba iliyoidhinishwa mwaka wa 2010. Hivi ni kusema kuwa urasmi wa lugha ya Kiswahili haujaamilishwa katika taasisi na asasi za umma.

Aloo (2002) alitambua kuwa msimbo huchanganywa mno katika matangazo ya biashara kwenye redio na runinga. Alitambua uchanganyaji wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili pamoja na lugha za kiasili kama vile Kikuyu, Kidholuo na Kikisii japo kwa kiwango kidogo. Munyasa (2012) naye alibaini uchanganyaji wa Kiingereza, Kiswahili, Kikuyu, Kikisii, Kikamba na Kidholuo katika lugha inayotumiwa kwenye mikahawa ya *Eastlands*. Kulingana na Kihara (2006), uchanganyaji msimbo unaojitokeza katika sajili ya matatu aghalabu huwa Kiingereza na Kiswahili, japo wakati mwingine unaweza kuhusisha lugha za kiasili na Sheng'. Utafiti wa Maina (2011) nao uligundua uchanganyaji msimbo wa namna hii.

Katika utangazaji wa mchezo wa kandanda, uchanganyaji msimbo hutokea kwa kuchopeka maneno na virai vya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo inayotumiwa na watangazaji kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji. Romaine (1989) ametambua aina tatu zifuatazo za uchanganyaji msimbo.

#### 2.2.1.1 Uambatishaji wa Kiungo

Huu ni uingizaji au uchopekaji wa maneno ya lugha nyingine mwanzoni mwa kauli za lugha ya msingi. Aina hii ya uchanganyaji msimbo hutokea pale msemaji

anapokosa kisawe na hana muda wa kukitafuta. Poplack (1980) anaeleza kuwa aghalabu watu huingiza neno moja kutoka lugha nyingine kwa sababu wanasahau au hawajalijua lile neno katika lugha ya msingi inayotumiwa katika sentensi ile. Katika utangazaji wa mchezo wa kandanda, uchopekaji mwanzoni hutokea kama ilivyoonyeshwa na data ya Jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2.4: Uambatishaji wa Kiungo**

| **Matini** | **Maana** |
|---|---|
| Defender anaondoa mpira katika eneo la hatari. | Mchezaji wa safu ya ulinzi ameondoa mpira kutoka eneo ambalo ungefunga. |
| Goalie amefyatuka kama mshale na kunyaka mpira huo. | Mlinda lango ametoka kwa mbio na kushika mpira. |
| Keeper analala na mpira ule. | Mlinda lango anashika mpira na kulala nao. |
| Referee anapuliza kipenga kumaliza mechi ya leo. | Muamuzi mkuu anapiga filimbi kuashiria kuwa mchezo wa leo umefika mwisho. |
| Game ya leo inaanza hapa kwa kasi msikilizaji wangu. | Msikilizaji wangu mchezo wa leo unaanza kwa kasi. |
| Corner hiyo itachanjwa na kiungo machachari wa timu ya Ulinzi. | Mpira wa adhabu kutoka ukingoni mwa uwanja utapigwa na kiungo machachari wa timu ya Ulinzi. |
| Manager huyu wa Man United alinukuliwa juzi katika vyombo vya habari akisema kuwa hajafurahishwa na kiwango cha wachezaji wake. | Mkufunzi huyu wa klabu ya Man Utd alinukuliwa juzi akisema kuwa hajafurahishwa na kiwanga cha wachezaji wake. |
| Penalty hiyo itachezwa kuelekea lango la Sofapaka. | Adhabu hiyo ya penalti itachezwa kuelekea lango la Sofapaka. |

Jedwali limeonyesha uchopekaji wa maneno ya Kiingereza katika matini za Kiswahili. Maneno *defender, goalie, keeper, referee, game, corner, manager* na *penalty* yametumiwa mwanzoni mwa matini za Kiswahili zinazoeleza mfululizo wa mchezo wa kandanda.

### 2.2.1.2 Uchopekaji wa Maneno ya Kigeni Kati ya Sentensi

Huu ni uingizaji wa vipashio vya lugha nyingine kati ya matini za lugha ya msingi. Aina hii ya uchanganyaji msimbo huwa na maana kwamba maneno ya kigeni huzingatia sheria za kifonolojia za lugha pokezi katika uundaji wa matini. Hivi ni kusema kuwa msemaji anafanya maneno ya Kiingereza kuchukua muundo wa lugha ya Kiswahili katika upatanisho wa kisarufi. Mifano ya data iliyodhihirisha uchopekaji wa maneno ya kigeni kati ya sentensi imechukua muundo wa maneno huru au virai kama ilivyojitokeza katika Jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2.5: Uchopekaji wa Maneno ya Kigeni Kati ya Sentensi**

| Matini | Maana |
|---|---|
| Mshambulizi huyo amechezewa visivyo <u>inside the box, referee</u> anasema ni penalti. | Refa anatoa adhabu ya penalti kwani mshambulizi amechezewa visivyo katika eneo la hatari. |
| Kiungo huyo asiyekubali kupitwa amefanya <u>foul</u> katika duara la katikati. | Kiungo shupavu amecheza visivyo katka eneo la katikati mwa uwanja. |
| Timu ya Ulinzi inaendelea kuiwekea timu ya Sofapaka <u>pressure</u> katika lango lao. | Timu ya Ulinzi inaendelea kuibana timu ya Sofapaka karibu na lango lao. |
| Baada ya kushinda mechi hii, AFC | Baada ya kushinda mechi hii, AFC |



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

| | |
|---|---|
| Leopards yaingia finals za GOtv Cup dhidi ya mahasimu wao wa jadi Gor Mahia. | Leopards yaingia awamu ya mwisho wa mchuano wa kombe la GOtv dhidi ya mahasimu wao wa jadi Gor Mahia. |
| Mchezaji huyu hatari alinunuliwa katika deal iliyowagharimu waajiri wake kitita kikubwa cha pesa. | Mchezaji huyu mahiri alisajiliwa katika kandarasi iliyowagharimu waajiri wake pesa nyingi. |
| Anatoa accurate pass kwenye wing ya kushoto kumtafuta mwenzake. | Anamtolea mwenzake aliye katika safu ya kushoto pasi nzuri. |
| Mkufunzi wa timu ya Tusker analazimika kufanya substitution ya mapema baada ya mlinzi wa safu ya kulia kuumia. | Mkufunzi wa timu ya Tusker analazimika kufanya badiliko la mapema la mchezaji baada ya mlinzi wa safu ya kulia kuumia. |
| Kiungo yule anakwenda na mpira, anakwenda, lakini mlinzi yule anapiga tackle nzuri na kuchukua ule mpira. | Kiungo huyo ananyang'anywa mpira na mlinzi. |
| Anachukua mpira pale, anaguza touch nzuri, anamega kule... | Anachukua mpira na kuucheza vizuri kwa mwenzake. |
| Katika Manchester derby second leg, City inaichapa United magoli matatu bila jibu. | Manchester City imeifunga Manchester United mabao matatu kwa sufuri. |

Matini hizi za uchopekaji wa maneno ya kigeni kati ya sentensi zinahusu matukio yanayotokea uwanjani wakati mchezo unapoendelea. Kwa mfano, matini 'Mshambulizi huyo amechezewa visivyo inside tha box, referee anasema ni penalti' na 'Anatoa accurate pass kwenye wing ya kushoto kumtafuta mwenzake' inaonyesha hali hii. Hali kadhalika, baadhi ya matini hizi kama vile 'Mchezaji huyu hatari alinunuliwa katika deal iliyowagharimu waajiri wake kitita kikubwa cha pesa' na 'Baada ya kushinda mechi hii, AFC Leopards yaingia finals za GOtv cup dhidi ya mahasimu wao wa jadi Gor Mahia' zinahusu maelezo ya mambo yasiyotokea uwanjani.

Uchanganyaji huu wa msimbo unaohusisha uchopekaji wa maneno ya Kiingereza kati ya kauli za lugha ya Kiswahili unaweza pia kuunda vitenzi vya Kiingereza kwa kutumia kanuni za Kiswahili bila kuvunja kanuni za kisintaksia za lugha zote mbili. Haya yanashadidiwa na Poplack (1980: 580) anayesema:

> Kuna uwezekano wa kuchanganya msimbo katika usemi kwa njia ambayo kuingiliana kwa vipengele vya lugha zote mbili hakuvunji kanuni au kaida za kisintaksia za lugha mojawapo. (Ty)

Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda inavyoonyesha aina hii ya uchopekaji.

1. Msikilizaji wangu inasikitisha kuwa mshambulizi huyo mahiri <u>amemiss</u> nafasi ya wazi ya kufunga.
2. Mchezaji huyo chipukizi anayeitwa Wanyonyi, aliingia uwanjani na punde tu <u>akascore</u> bao la ushindi. Gor moja, Ulinzi sufuri.
3. Naona Ulinzi ikiendelea kulemewa hapa baada ya kupachikwa bao la mapema. Kocha analazimika <u>kusubstitute</u> wachezaji kabla ya mambo kuharibika zaidi.
4. Wachezaji wa pande zote walitaka <u>kufight</u> uwanjani baada ya kutoelewana.
5. Anachanja ile penalty go- oo-oool. Msikilizaji Gerrard alimwona keeper <u>akidive</u> kushoto, akaweka shuti kulia.
6. Sofapaka <u>wanawaste</u> time hapa wakijua wako kifua mbele mabao mawili.

7. Wanachukua mpira Chelsea, Hazard anaangalia acheze wapi, anachange wing hadi kuupiga mpira kushoto...
8. Mpenzi msikilizaji timu hii ya Tusker inarindimwa hapa bao la pili. Inaonekana kuwa defense yao inaleak na lazima kocha afanye sub ya mapema.

Uundaji huu wa vitenzi vya Kiingereza kwa kutumia kanuni za Kiswahili kwa njia isiyovunja kanuni za kisintaksia za lugha zote mbili unajitokeza kama mbinu inayomwezesha mtangazaji kusimulia matukio ya mchezo kwa urahisi wa matamshi, mfululizo na kasi inayotokea.

#### 2.2.1.3 Uchopekaji wa Maneno ya Kigeni Mwishoni mwa Sentensi

Katika aina hii ya uchanganyaji msimbo, vipashio vya lugha changizi huingizwa mwishoni mwa sentensi za lugha pokezi. Uchopekaji huu hufuata mikondo miwili. Mkondo wa kwanza unaobainika katika utangazaji wa mchezo wa kandanda ni pale ambapo vipashio vya lugha ya Kiingereza hukamilisha sentensi za lugha ya Kiswahili kama inavyodhihirika katika Jedwali hili.

**Jedwali 2.6: Uchopekaji wa Maneno ya Kigeni Mwishoni mwa Sentensi**

| Matini | Maana |
|---|---|
| Wanakwenda, wanaingia pale lakini wanashindwa kuivunja ile defence. | Wanaingia katika safu ya ulinzi lakini wanashindwa kuipenya. |
| Ajabu hii, penalti hiyo imeokolewa na | Inashangaza kuwa mlinda lango |

| | |
|---|---|
| goal keeper. | ameokoa penalti. |
| Salaale! Difenda huyo amenawa mpira ndani ya box. Penalty! | Inasikitisha kuwa mlinzi huyo anapata adhabu ya penalti kwa kushika mpira ndani ya eneo lisiloruhusiwa. |
| Wachezaji ambao wameshuka leo wamewekwa bench. | Wachezaji walioshuka katika kiwango cha mchezo wamepumzishwa. |
| Anakwenda, ameingia left wing. | Mchezaji anakwenda na mpira katika safu ya kushoto ya uwanja. |
| Anasonga, anacheza mbele faster faster! | Anasonga na kucheza mpira mbele haraka. |
| Refa anamlisha nyekundu kwa kucheza rough. | Mchezaji anatolewa uwanjani kwa kuonyesha mchezo mbaya. |
| Anachenga, anakwenda kule-ee go-ool. Suarez anafunga hat-trick | Suarez amefunga mabao matatu katika mechi moja. |

### 2.2.2 Ubadilishaji Msimbo

Hii ni mbinu nyingine ya mawasiliano inayotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda. Buliba na wengine (2006) wanaeleza kuwa ubadilishaji msimbo hutokea pale ambapo msemaji wa lugha hugeuza mazungumzo yake kutoka lugha moja hadi nyingine kutokana na umilisi wake wa zaidi ya lugha moja. Wanaendelea kueleza kuwa uteuzi wa msimbo badalia hutegemea washiriki, mada, mandhari na mtindo. Wanatoa mfano wa watoto wa Kihispaniola wanaobadilisha usemi kutoka Kihispaniola hadi Kiingereza wanapozungumza na walimu. Hivi ni kusema kuwa kule kubadilisha mazingira kutoka nyumbani hadi shuleni ni msingi wa kubadilisha msimbo. Wanasema kuwa ubadilishaji msimbo pia huweza kutokana na mambo ya taaluma ambapo dhana na istilahi fulani huwa hazimo katika lugha pokezi na hivyo kumlazimisha msemaji kuhamia lugha nyingine ili kuzieleza.

Habwe na wengine (2010) wanaeleza kwamba ubadilishaji msimbo hutokea wakati ambapo mjozi-lugha au mwingi-lugha anatumia lugha mbili kwa kubadilishana. Akimnukuu Weinreich (1957), Naseh (1997:202) anaeleza kuwa ubadilishaji msimbo hutokea katika mazingira ya mazungumzo pale watu wenye zaidi ya lugha moja wanapotoka lugha moja kwenda nyingine kwa mujibu wa taratibu na mabadiliko katika lugha.

Kulingana na Hymes (1974), kubadili msimbo ni matumizi ya mbili au zaidi zinazogusa sentensi zaidi ya moja au hata mitindo tofauti ya lugha. Hivi ni kusema kuwa ubadilishaji msimbo ni uchopekaji wa sentensi ya lugha moja katika sentensi ya lugha nyingine. Mkondo huu huhusisha kubadilisha sentensi kwa namna ambayo kila kishazi huwa katika lugha moja. Hivi ni kusema kwamba sentensi moja hugawanywa mara mbili na lugha inazohusika. Kila sehemu ya sentensi huundwa kwa uzingativu wa sheria za utunzi za lugha husika. Mkondo huu hudhihirisha hali ambapo hakuna matumizi ya maneno ya lugha mbili tofauti ndani ya sentensi ya lugha moja.

Buliba na wengine (2006) na Habwe na wengine (2010) wanaafikiana kuwa japo dhana ya uchanganyaji msimbo na ubadilishaji msimbo hutokana na uwezo wa uwili lugha, wingi lugha na ulumbi, si visawe. Buliba na wengine (2006) na Wamitila (2003b) wanatofautisha dhana hizi kwa kuafikiana kwamba katika ubadilishaji msimbo, msemaji hutumia lugha moja kikamilifu bila kuingiza maneno ya lugha nyingine katikati ya usemi wake kwa muda mrefu kisha ghafla

hubadilisha na kuanza kutumia lugha ya pili wakati katika uchanganyi msimbo, lugha mbili tofauti, au hata zaidi hutumiwa kwa wakati mmoja katika matini. Mawazo haya yanaafikiana na ya Ho (2007) anayesema kuwa ubadilishaji msimbo hutokea baina ya sentensi na nyingine huku uchanganyaji msimbo ukitokea ndani ya sentensi moja.

Inajitokeza kuwa uchanganyaji msimbo aghalabu huhusisha uchopekaji wa vipashio vidogo vya lugha kama vile maneno na virai huku ubadilishaji msimbo ukihusisha uchopekaji wa vipashio vikubwa au kamili hasa vishazi vya lugha tofauti katika kauli moja. Maina (2011) alitambua ubadilishaji msimbo wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kama mbinu mojawapo ya matangazo ya runinga nchini Kenya. Mifano ifuatayo ya ubadilishaji msimbo inadhihirika katika lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda.

1. Wanakimbizana pale wachezaji wale, wanamenyana, anamlaza mwenzake. Inaonekana amemuumiza vibaya na inabidi mchezaji huyo aondolewe uwanjani. That is very dangerous play.
2. Anachukua mpira, anakwenda, anakwenda, anapiga go-goo-oool! He only got one chance and he takes it!
3. Kona hiyo itapigwa kuelekea lango la Tusker. Anaruka pale na kupiga mpira kwa kichwa goo, la, la, la! That was a free header, and he misses a very clear chance!

4. Ndugu msikilizaji, sikiliza penalti hiyo kwa makini. Sasa ni kipa anatazamana na mshambulizi huyu matata. Anachanja pale go-oo anapiga nje! He misses the penalty! You will not believe it. He has not believed it either. And that is the game of football, very strange.
5. Difenda anaondoa mpira maji maji kutoka eneo lake. Wanachukua na kutimua mbio. It's a counter attack, and they score. It's a goal! That was so fast!
6. Naona timu ya Gor inafanya mabadiliko kabla ya kupiga kona hiyo. Anaondoka Rama Salim anaingia Kevin Omondi. Haya. Kona hiyo inapigwa majimaji pale-ee-ee anapiga kichwa Kevin Omondi go-oo-ooo-l. Amini usiamini, mchezaji huyu anafunga bao just on his first touch of the ball! Gor moja, Mathare United bila.
7. Salaale! Ajabu gani hii? He only had the net to beat lakini anajaza mpira nje. La!
8. Anakwenda, anakwenda na mpira, la la la! Msikilizaji it was only him and the goal keeper, lakini anakosa nafasi ya wazi ya kufunga. Kipa anapangua!

Uchanganyaji msimbo na ubadilishaji msimbo huwa mbinu maarufu sana miongoni mwa watangazaji wa mchezo wa kandanda wanapoelezea wasikilizaji jinsi mchezo unavyoendelea. Gumperz (1982) na Appel na Muysken (1987) wanaafikiana kuwa wasemaji hawajikuti wakichanganya tu msimbo kiholela. Wanasema kwamba uchanganyaji msimbo huwa na sababu na dhima katika usemi. Wametambua dhima na uamilifu wa kurejelea, kufafanua, kupendeza na kujitambulisha, kuonyesha hisia na kusisitiza. Buliba na wengine (2006) nao

wanasema kuwa watumizi wa lugha hubadilisha msimbo kwa madhumuni ya mtindo, yaani kusisitiza kile anachosema. Wanaeleza pia kuwa wasemaji hubadilisha msimbo kwa nia ya kupambanua dhana ngeni na katika kudhihirisha hisia fulani. Dhima hizi hudhihirika katika lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda kama ifuatavyo.

**2.2.2.1 Kurejelea**

Watangazaji wa mchezo wa kandanda hutumia maneno ya Kiingereza kurejelea dhana ambazo ama hazina visawe au hawajui visawe vyake katika lugha ya Kiswahili au ambazo matumizi yake katika lugha hiyo ya kigeni (Kiingereza) yamezoeleka na kwa hiyo kueleweka zaidi. Kwa njia hii wasemaji hufidia umilisi wao mfinyu wa lugha moja.

Baadhi ya maneno ya Kiingereza ambayo watangazaji wa mchezo wa kandanda huonekana kutojua visawe vyake ni kama vile *defender, pressure, corner, foul, pass, finals, deal* na *wing*. Hata hivyo, watangazaji hawa wamezoea kutumia maneno kama vile *goalie, keeper, referee, game, manager, inside the box,* na *substitution* bila kuyatafutia visawe. Sababu nyingine ni kuwa mchezo wa kandanda huchezwa kwa kasi isiyowaruhusu watangazaji kupata muda wa kutafuta visawe au tafsiri faafu ya istilahi hizo.

#### 2.2.2.2 Kufafanua

Wasemaji huchanganya msimbo wanapotaka dhana fulani zieleweke waziwazi kwa walengwa. Hii ni kwa sababu wanaamini kuwa dhana hizo hujitokeza dhahiri zikiwasilishwa katika lugha hizo. Hivi ni kusema kwamba wahusika wanachanganya msimbo ili kusahilisha mawasiliano na upashaji wa ujumbe kwa njia angavu miongoni mwao. Uchanganyaji msimbo katika sajili ya mchezo wa kandanda hudhihirisha dhima hii kama inavyojitokeza katika matini zifuatazo.

1. Mshambulizi huyo anachezewa visivyo inside the box, referee anasema ni penalty.
2. Anatoa accurate pass kwenye wing wa kushoto kumtafuta mwenzake.
3. Anakenda, anakwenda na mpira, la, la, la! It was only him and the goal keeper lakini anakosa nafasi ya wazi.
4. Anachukua mpira, anakwenda, anakwenda, anapiga go-goo-ol. He only got one chance and he takes it.
5. Anaruka na kupiga mpira kwa kichwa goo, la, la, la! That was a free header and he misses a very clear chance.
6. Difenda anaondoa mpira huo majimaji kutoka eneo lake. Wanachukua na kutimua mbio. It's a counter attack, and they score. It's a goal! That was so fast.

Uchanganyaji msimbo wenye dhima ya ufafanuzi aghalabu hujitokeza kuwa vishazi ambatano vinavyojumuisha sentensi kadhaa za Kiswahili na Kiingereza

zilizounganishwa pamoja. Hii inamaanisha kuwa ufafanuzi hueleweka bayana na hufikisha ujumbe dhahiri kupitia matumizi ya maneno mengi yanayojenga matini zenye mshikamano. Kwa hiyo, vishazi hivi ambatano vinabainisha nadharia ya SAM ianyosema kuwa lugha huwa na maana matinishi.

#### 2.2.2.3 Kupendeza na Kujitambulisha

Wahusika hutumia maneno kutoka lugha nyingine ili kuwaonyesha wenzao kuwa hata wao wanazijua lugha zile. Hii inamaanisha kuwa watangazaji huchanganya msimbo ili kuonyesha ulumbi wao. Kwa njia hii, maneno haya yanatumiwa sio tu kama ombi la kukubalika kwa mtangazaji miongoni mwa wasikilizaji bali pia kama ombi la kukubaliwa kwa ujumbe wenyewe. Matini zote zinazohusu uambatishaji wa kiungo, uchopekaji wa maneno ya kigeni kati ya sentensi na uchopekaji wa maneno ya kigeni mwishoni mwa sentensi zinaonyesha kwamba mbali na kutaka kufikisha ujumbe kwa njia angavu, mtangazaji hujaribu kuwapendeza, kuwateka, kujitambulisha na kujinasibisha na wasikilizaji ambao baadhi ni wasomi au vijana.

#### 2.2.2.4 Kuonyesha Hisia

Wasemaji wanaweza kuchanganya msimbo ili kudhihirisha hisia mbalimbali zinazoambatana na mada zinazozungumziwa. Mchezo wa kandanda aghalabu huandamana na hisia kama vile hasira, furaha, huzuni maudhi, matumaini na kutamauka miongoni mwa wakufunzi, wachezaji na mashabiki. Hata hivyo,

watangazaji wa mchezo huu pia hujikuta wakidhihirisha hisia zao kupitia lugha yao kama ifuatavyo.

1. Salaale! Ajabu gani hii? He only had the goal keeper to beat, lakini anajaza mpira nje.
2. Anakwenda, anakwenda na mpira, la, la ,la! It was only him and the goal keeper lakini anakosa nafasi ya wazi.!
3. Wanakimbizana pale wachezaji wale, anamlaza mwenzake na inaonekana amemuumiza vibaya. Inabidi aondolewe uwanjani kwa machela. That's very dangerous play indeed.
4. Anaruka na kupiga mpira kwa kichwa, goo, la, la, la! That was a free header and he misses a very clear chance!
5. Ndugu msikilizaji, sikiliza penalti hii kwa makini. Sasa ni kipa anatazamana na mshambulizi huyu matata. Anachanja pale go-oo, anapiga nje! He misses the penalty! You can not believe it. He has not believed it either. And that's the game of football, very strange!
6. Naona timu ya Gor inafanya mabadiliko kabla ya kupiga kona hiyo. Anaondoka Rama Salim anaingia Kevin Omondi. Haya. Kona hiyo inapigwa majimaji pale-ee-ee anapiga kichwa Kevin Omondi go-oo-ooo-l. Amini usiamini, mchezaji huyu anafunga bao just on his first touch of the ball! Gor moja, Mathare United bila.

Matini za 1, 2, 4 na 5 zinaonyesha kauli zinazotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda kudhihirisha hisia zao za kutoridhika na kutamauka wakati matokeo au yanayojiri mchezoni yanapokuwa kinyume cha matarajio ya wengi. Matini ya 3 hutolewa na watangazaji kudhihirisha hisia za huzuni na uchungu wachezaji wanapochezewa visivyo. Hisia hizi zinadhihirika kutokana na kauli kuwa wachezaji wanatarajiwa kucheza vizuri na kufunga mabao wapatapo nafasi.

Ni muhimu ieleweke kuwa kama aina mojawapo ya burudani, upeo wa msisimko wa mchezo wa kandanda ni ufungaji wa mabao na upataji wa ushindi, jambo ambalo lisipotokea, wahusika wote wakiwemo watangazaji huweza kukasirika, kuhuzunika na kutamauka. Matini ya 6 inadhihirisha hisia za mshangao. Anachomaanisha mtangazaji ni kuwa si jambo la kawaida kwa mchezaji kuingizwa uwanjani na kufunga bao anapogusa mpira kwa mara ya kwanza.

#### 2.2.2.5 Kusisitiza

Dhima nyingine ya uchanganyaji msimbo ni msisitizo wa ujumbe. Msisitizo wa ujumbe hutokana na urudifu. Katika sajili ya mchezo wa kandanda, watangazaji wa mchezo huu hutumia kauli ndefu za Kiswahili na Kiingereza zilizounganishwa kusisitiza ujumbe. Matumizi haya ya kauli ndefu za lugha mseto ni njia mojawapo ambayo watangazaji wa mchezo huu huonyesha ulumbi wao katika lugha. Kusisitiza huku kunaonekana katika kauli zifuatazo.

1. Ndugu msikilizaji, sikiliza penalti hiyo kwa makini. Sasa ni kipa anatazamana na mshambulizi huyu matata. Anachanja pale go-go-oo, anapiga nje! He misses the penalty! You will not believe it. He has not believed it either. And that is the game of football, very strange.
2. Difenda anaondoa mpira maji maji. Wanachukua na kutimua mbio. Wanakwenda. It's a counter attack and they score. It's a goal. That was so fast.
3. Ananyunyiza mpira kwake Ramsey, anatuliza maridadi kwenye gamba la kifua, anasonga, anamtilia kisigino Walcott, hiyo pasi ya backheel imetatiza defence hii ya Liverpool.
4. Anachukua mpira haraka pale Kelly, anakwenda Kelly, Kelly, Kelly, anatoa faster faster, ananyunyiza kwa wingi wa kushoto.

Sentensi hizi kimsingi zimejengwa kwa muungano wa sentensi za Kiswahili na za Kiingereza. Kwa mujibu wa maana zinazowasilishwa, sehemu ya pili ya sentensi hizi zilizo katika lugha ya Kiingereza zinaonekana kusisitiza sehemu ya kwanza zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Hivi ni kusema kwamba sehemu ya pili inajitokeza kama tafsiri ya sehemu ya kwanza.

Sehemu ya pili ya sentensi ya 1 iliyo katika lugha ya Kiingereza inajitokeza kama msisitizo. Kipande 'You will not believe it' na 'He has not believed it either' zina maana sawa na zinatilia mkazo suala kuwa 'He misses the penalty' ambayo nayo inakariri kauli kuwa 'anapiga nje!' Katika sentensi ya 2, sehemu 'wanachukua na

kutimua mbio' ina maana sawa na 'It's a counter attack' na 'That was so fast'. Hali kadhalika, kipande '... and they score' katika sentensi ya 2 ni msisitizo wa 'It's a goal' kwa sababu hazitoi ujumbe mpya. Kielezi 'faster faster' katika sentensi ya 4 kinatilia mkazo mwendo wa uchezaji wa mpira. Huo ni msisitizo wa sehemu ya kwanza ya sentensi 'Anachukua mpira haraka'. Hali hii ndiyo inayodhihirika katika sentensi ya 3 ambapo kirai 'hiyo pasi ya backheel' ni msisitizo wa 'anamtilia kisigino'. Hivyo basi ni dhahiri kuwa uchanganyaji msimbo pia ni mbinu inayotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kuonyesha msisitizo wa ujumbe kwa wasikilizaji. Dhima za uchanganyaji na ubadilishaji msimbo za kufafanua, kurejelea, kupendeza, kujitambulisha na kuonyesha hisia hukubaliana na mhimili wa nadharia ya SAM inayosema kuwa lugha huwa na maana tagusani.

## 2.3 Tamathali za Semi

Kwa mujibu wa Wamitila (2003b), tamathali za semi ni maneno au mafungu ya maneno yenye maana fiche. Mojawapo ya dhima muhimu ya tamathali za semi ni kuwa hutia ladha katika lugha na hivyo kuwaburudisha wasikilizaji. Kwa kuwa mchezo wa kandanda hunuiwa kuwaburudisha na kuwachangamsha watazamaji na wasikilizaji, lugha inayotumiwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda hujenga uhusiano na mshikamano miongoni mwa wahusika hawa. Hivyo basi, matumizi ya tamathali za semi hubainisha lugha kama mfumo wenye maana tagusani. Baadhi ya tamathali za semi zilizojitokeza katika uchanganuzi wa data yetu ni takriri, tashbihi, tashihisi, balagha, misemo na misimu.

### 2.3.1 Takriri/ Urudiaji

Takriri ni mbinu ya urudiaji wa silabi/mizani, neno, vifungu, mistari, vishazi au muundo wa kisintaksia (Wamitila 2003b). Hivyo basi, tunaweza kuwa na aina tofauti za takriri kama vile takriri-silabi, takriri-neno, takriri-vifungu na takriri-vishazi. Takriri hujitokeza kama sifa muhimu ya kishairi.

Brierly (1995) anaeleza kuwa takriri hutumiwa kusisitiza na kuthibitisha ujumbe unaopashwa. Kulingana na Leech (1966), takriri ni mbinu inayojenga na huchochea kumbukizi na kuzidisha athari kwa mpokezi wa ujumbe. Akizungumzia msisitizo unaopatikana katika Biblia, Alter (1981) anaeleza kuwa kukaririwa kwa maneno muhimu huwa na nia ya kubainisha waziwazi dhamira kupitia kujitokeza kwake katika sehemu tofauti. Vestergaard na Shroder (1985) nao wanaona takriri kama mbinu ya kuamsha hamu ili msikilizaji au mpokezi wa ujumbe autie maanani. Naye Cook (2000) anaeleza kuwa utangazaji huelekea kutumia lugha kwa namna inayozua uradidi unaoweza kutambuliwa na kubashiriwa. Kwa hiyo, takriri hujitokeza kama mbinu ya kuzua matini zenye kusisitiza na kubainisha wa ujumbe.

Kuna takriri za aina tofauti tofauti ambazo zimebainika katika tafiti mbalimbali. Utafiti wa Kihara (2006) ulitambua urudiaji wa nomino, vibainishi na vitenzi. Aloo (2002) amepata uradidi wa viunganishi vinavyoleta mshikamano kwenye tangazo na uradidi wa jina la bidhaa inayotangazwa. Maina (2011) naye amebaini uradidi

wa kimaandishi na kiusemi wa bidhaa au huduma inayotangazwa na dhana muhimu zinazohusishwa nayo. Kulingana na data yetu, aina za takriri zinazojitokeza katika lugha inayotumiwa kwenye utangazaji wa mchezo wa kandanda ni za vitenzi na nomino.

#### 2.3.1.1 Takriri-Vitenzi

Hii ni aina ya takriri inayohusisha urudiaji wa vitenzi katika usemi. Kwa mfano.

<u>Kitenzi</u> : <u>Usemi</u>

Kwenda : Anakwenda, anakwenda, anakwenda na mpira, anakwenda na mpira...

Chenga : Anachenga, anachenga pale, anachenga moja, anachenga mbili, anachenga tena...

Kimbia : Anakimbia, anakimbia pale, anakimbia na mpira, anakimbia na mpira, anakimbia- aa-aaa...

Panda : Wanapanda, wanapanda na mpira, wanapanda pale, wanapanda kwenye wingi wa kushoto-oo...

Tamba : Wanatamba, wanatamba pale kwenye duara la katikati, wanatamba na mpira...

Kata : Anapokea mpira na kutuliza, anakata moja, anakata mbili, anakata tena..

Vitenzi *kwenda, chenga, kimbia, panda, tamba* na *kata* hukaririwa na watangazaji kueleza jinsi mchezo wa kandanda unavyoendelea. Maelezo haya hufanywa kwa njia inayojenga picha akilini mwa msikilizaji, ni kana kwamba anatazama mchezo ule moja kwa moja. Aidha, urudiaji wa vitenzi hivi huonyesha mfululizo na kasi ya mchezo huu.

**2.3.1.2 Takriri-Nomino**

Aina hii ya takriri huhusisha urudiaji wa nomino katika matini za utangazaji wa mchezo wa kandanda.

| <u>**Nomino**</u> | : | <u>**Usemi**</u> |
|---|---|---|
| Hatari | : | Anakwenda pale. Hatari, hatari katika lango, hatari katika lango, hatari pale, hatari... |
| Wall | : | 'Foul' ile itapigwa kuelekea lango la Gor. Naona 'keeper' wao Onyango anawaambia 'defence' yake "Wekeni wall! Wall! Wall! |
| Goal | : | Anatuma pale zinga zito-o go-go-o-goa-a-al! Goo-aa-ll! |
| Wing | : | Anatuma mpira kwa 'wing' ya kulia, unachukuliwa, anakimbia kwa 'wing', anaendelea kupanda kwa 'wing'... |
| Ramsey | : | Anatuliza pale Ramsey kwenye gamba la kifua, anasonga Ramsey, anaangalia acheze wapi Ramsey, Ramsey, anapokonywa mpira ule. |
| Sserenkuma | : | Anachukua mpira Sserenkuma, anachenga moja Sserenkuma, anakwenda Sserenkuma, Sserenkuma, Sserenkuma na mpira, Sserenkuma katika lango -oo, la! la! la!... |

Urudiaji wa nomino *hatari, lango, wall, wing, goal* na majina ya wachezaji kama vile *Ramsey* na *Sserenkuma* ni maarufu miongoni mwa watangazaji kuelezea mchezo unavyoendelea na kubainisha wachezaji wanaohusika na tukio fulani la mchezo wenyewe. Aidha urudiaji wa majina ya wachezaji huonyesha mfululizo wa mchezaji kuwa na mpira kwa muda fulani kabla ya kuutoa au kuupoteza kwa mchezaji mwingine. Urudiaji wa nomino *hatari* humaanisha kuwa mpira unakaribia kufungwa katika lango huku nomino *wall* ikimaanisha kuwa wachezaji wanapaswa kujipanga katika safu ili kuzuia mpira usipite. Kwa kuwa takriri hujitokeza kama mbinu ya kuzua matini ndefu zenye kusisitiza na kubainisha ujumbe, inatosheleza nadharia ya SAM inayosema kuwa lugha huwa na maana matinishi.

Licha ya msisitizo wa ujumbe au kutilia mkazo maana, mbinu ya uradidi unadhamiriwa kuacha athari na kumbukumbu za kudumu akilini mwa wasikilizaji. Vile vile, urudiaji wa vitenzi na nomino aghalabu huibua hisia za hatari kwa wasikilizaji wa timu inayokaribiwa kufungwa huku ukizua hisia za furaha na uchangamfu kwa wasikilizaji wa timu inayoshinda. Hali hii inaweza kuathiri maingiliano na uhusiano kati ya makundi yanayohusika. Hivyo basi, kauli hii inaafikiana na mhimili wa nadharia ya SAM inayosema kuwa lugha huwa na maana tagusani.

### 2.3.2 Tashbihi

Wamitila (2003a) anaeleza kuwa tashbihi ni misemo ya kilinganishi ambayo hukielezea kitu au sifa zake kwa kukilinganisha na kingine ili kukuza sifa zake. Anaendelea kueleza kuwa tashbihi hutegemea msingi wa picha na stiari kuonyesha ulinganisho wa sifa za vitu. Tashbihi huwa na ulinganisho unaotokana na mlandano fulani unaochukuliwa kuwepo baina ya virejelewa viwili (Chapman, 1989). Hivi ni kusema kuwa tabia ya vitu viwili vinavyorejelewa hufanana. Maoni haya yanaoana na ya Lucas (1955) aliyesema kuwa tashbihi ni mbinu inayotumiwa kuweka dhana mbili sambamba.

**Jedwali 2.7: Matumizi ya Tashbihi**

| **Matini** | **Maana** |
|---|---|
| Kipa ameruka na kuunyaka mpira ule kama nyani. | Mlinda lango ameruka juu na kuushika mpira kwa umaridadi. |
| Mshambulizi huyo amepiga mpira kama risasi. | Mpira umeenda kasi sana kwa kupigwa kwa nguvu nyingi. |
| Kipa amejipinda kama upinde na kukamata mpira. | Mlinda lango ameruka kuelekea upande wa kulia au kushoto na kuushika mpira. |
| Amempiga mwenzake na mpira kama radi. | Amempiga mchezji mwenzake na mpira kwa nguvu inayosikika kama mpasuko |
| Ametuma mpira mkwaju kimo cha paka. | Amepiga mpira mkubwa uliofika mbali. |
| Mshambulizi huyo ni mkali kama wembe. | Mshambulizi huyo ni mchezaji mzuri anayefunga kila apatapo nafasi. |
| Mshambulizi huyo alifyatuka mbio kama mshale. | Mshambulizi huyo alikimbia kwa kasi sana. |
| Refa analamba kipenga kana kwamba kimepakwa asali. | Refa hupenda kuweka kipenga mdomoni kwa muda mwingi. |



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

| | |
|---|---|
| Kiungo huyo ametuma mawe kimo cha kanga | Mchezaji huyo wa kati amepiga mpira kwa nguvu kuelekea langoni. |
| Kizito ni beki asiyepitika hapa, ni mzito kama nanga | Kizito ni mlinzi mnene asiyepitika kwa urahisi. |
| Anakwenda pale nyota huyo-oo anavurumisha kombora kimo cha nyoka. | Mchezaji mahiri amepiga mpira kwa nguvu nyingi kulenga lango. |
| Anakwenda, anakwenda Were, anapita pale, winga huyu wa Leopards ni mwepesi kama swara | Mchezaji Were anakimbia kwa kasi sana anapocheza. |

Kulingana na data tuliyochanganua, mbinu hii imetumiwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kuonyesha usambamba, mfanano au ulingano wa mchezo huu na vitu vingine. Kwa mfano, jinsi mlinda lango anavyoruka ili kushika mpira kunalinganishwa na anavyoruka nyani mitini huku mpasuko unaotokea mchezaji anapopigwa na mpira unafananishwa na radi. Aidha, ubora wa mchezaji wa safu ya mbele katika ufungaji wa mabao unalinganishwa na ukali wa wenbe huku uzito au uzani wa mchezaji wa safu ya ulinzi ukimithilishwa na ule wa nanga.

Ufananisho huu unaotumiwa sana katika lugha ya matangazo una dhima ya kuwasaidia wasikilizaji kuelewa mchezo huu unavyochezwa na kuendelea kwa kuwajengea picha anuai. Ujenzi huu wa picha unaotokana na yaliyomo kwenye mazingira ya watangazaji na wasikilizaji unathibitisha ukweli wa mhimili wa nadharia ya SAM inayozingatia kuwa lugha ina uamilifu wa kupambanua hali halisi kwa kuzingatia tajriba za kijamii.

### 2.3.3 Tashihisi

Njogu na Chimerah (1999) wanafafanua tashihisi kuwa ni mbinu ambayo kwayo kitu kisicho na uhai, yaani uwezo wa kuona, kushika, kunusa, kuhisi na kuwa na urazini wa kibinadamu hupewa uwezo huo. Wamitila (2003b) naye anaeleza kuwa tashihisi ni hali ya kukipa kitu kisicho na uhai uwezo wa kutenda kana kwamba kina uhai.

Kihara (2006) ametambua uhuishaji wa magari ya matatu kwa kupewa uwezo wa kula abiria. Utafiti wa Maina (2011) umebainisha kuwa baadhi ya ishara zinazotumiwa kurejelea bidhaa huwa zinaashiria uwepo wa sifa za kibinadamu. Anasema kuwa watangazaji hufanya hivi ili kusifu na kuonyesha ubora wa bidhaa au huduma husika ili kuvutia wateja.

Uchanganuzi wetu wa data umeonyesha matumizi ya tashihisi kama mbinu mojawapo inayopendelewa na watangazaji wa mchezo wa kandanda kutilia uzito ujumbe kwa wasikilizaji wao na kuutia uhai au uchangamfu mchezo huu.

**Jedwali 2.8: Matumizi ya Tashihisi: Vitenzi**

| Data | Matini | Maana |
|---|---|---|
| Toka | Mpira umekuwa mwingi na <u>kutoka nje.</u> | Hali ya mpira kuwa nje ya uwanja unaochezewa. |
| Pambana | Timu hizi zinaendelea <u>kupambana</u> hapa vikali. | Timu hizo zinaendelea kuwa na mchezo mgumu kati yao. |
| Kwaruza | Mchezo unaendelea kuwa mgumu huku timu hizi | Timu hizi zinaendelea kushindana vikali. |

| | | |
|---|---|---|
| | zikiendelea kukwaruzana | |
| Nyanyasa | Msikilizaji mchezo unamalizika hapa, timu ya AFC Loepards imenyanyasa Gor Mahia mabao 2-0. | Timu ya AFC Loapards imeshinda Gor Mahia mabao 2-0 baada ya mchezo kumalizika. |
| Adhibu | Sofapaka yaendelea kuiadhibu Tusker hapa. Inaendelea kuongoza mabao 3-1. | Sofapaka inafunga Tusker mabao 3-1 kabla ya mchezo kumalizika. |
| Shambulia | Timu zote mbili zinashambuliana vikali bila mafanikio. | Timu zote mbili zinapiga mipira kadhaa katika lango la nyingine bila kupata bao. |
| Osha | Mchezo unafika mwisho hapa, Ulinzi imeosha Sofapaka. | Ulinzi imeishinda Sofapaka kwa mabao mengi. |
| Tawala | Timu ya Liverpool inaonyesha mchezo mzuri sana. Inaendelea kutawala mchezo huu na wanaongoza Man United mabao 3 kwa nunge. | Timu ya Liverpool imeshafunga timu ya Man United mabao 3 kwa sufuri kwa sababu inamiliki sehemu kubwa ya mchezo. |
| Ingia; kataa | Mchezo unashika kasi hapa, Chelsea inaingia kupenya ngome hii lakini Man City inakataa katakata. | Timu ya Chelsea inajaribu kufunga katika lango la Manchester City lakini juhudi hizo hazifanikiwa. |

Jedwali hili linaonyesha kwamba klabu mbalimbali za kandanda zimepewa sifa na uwezo wa kuwa na uhai na kutenda kama binadamu. Vitenzi *toka, pambana, kwaruza, nyanyasa, adhibu, shambulia, osha, tawala, ingia* na *kataa* vinaweza tu kutumiwa na viumbe vyenye uhai, hasa binadamu. Vitenzi hivi vimetumiwa katika matini hizi kwa njia inayosawiri klabu za kandanda kama binadamu maadui wanaotumia kila nafasi wanayopata kuwaangamiza wenzao. Maana

inayowasilishwa hapo ni kwamba wachezaji wa timu zote zinazoshiriki katika mchezo wa kandanda hujitahidi kwa namna zote kuibuka na ushindi kila wanapocheza.

**Jedwali 2.9: Matumizi ya Tashihisi: Semi**

| **Data** | **Matini** | **Maana** |
|---|---|---|
| Lala njaa | Malango haya yanaendelea kulala njaa. | Timu zinazocheza kuwa katika hali ya kutofungana bao lolote. |
| Tuma mpira | Mshambulizi huyu ametuma mpira mrefu kimo cha kanga. | Amepiga mpira kwa nguvu uliouwezesha kufika mbali. |
| Rusha mawe | Tusker anazidi kurushia Sony Sugar mawe. | Tusker inaendelea kupiga mipira mingi katika lango la Sony Sugar. |
| Ona lango | Inasikitisha kuwa baada ya makabiliano haya, hakuna timu iliyoona lango la nyingine. | Timu hizo hazijafungana mabao yoyote licha ya mechi kuwa ngumu. |
| Kodoa macho | Jamani klabu hizi zinaendelea kukodoleana macho kwenye mchezo huu mgumu. | Klabu hizi zinaendelea kushindana vikali kwenye mchezo. |
| Tia mkononi | Amini usiamini, Arsenal inatiwa mkononi na miamba hawa Chelsea. Wanalazwa mabao 6-0. | Inashangaza kuwa Arsenal imeshindwa mabao 6-0 na Chelsea. |
| Kula na kutapika | Msikilizaji popote pale ulipo, tunakufahamisha kuwa mechi hii imehudhuriwa na mashabiki wengi ajabu. Uwanja umekula na kutapika. | Uwanja umejaa sana kutokana na mashabiki wengi wanaotaka kutazama mechi. |

Tashihisi inayojitokeza katika jedwali hili imehusisha matumizi ya lugha kitamathali. Timu mbalimbali za mchezo wa kandanda zimepewa uwezo wa kulala, kutuma, kurusha, kuona, kula, kutapika na kukodoa macho. Misimu *tuma mpira, rusha mawe, ona lango,* na *kula na kutapika* na misemo *lala njaa, tia mkononi* na *kodoa macho* imetumiwa kwa njia inayohuisha timu za kandanda. Misimu *tuma mpira* na *rusha mawe* hurejelea hali ya kupiga mpira kwa nguvu ili kufunga huku *Ona lango* ukitumiwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kumaanisha timu kufunga bao. Uga wa kuchezewa mpira unahusishwa na uwezo wa *kula na kutapika*. Msimu huu unatumiwa kuonyesha hali ya uwanja kujawa sisisi na mashabiki.

Msemo *lala njaa,* wenye maana ya kupitisha usiku wote bila kula, umetumiwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kumaanisha kuwa hakuna bao ambalo limefungwa katika lango lolote. Msemo *tia mkononi* wenye maana ya kutwaa au kupata kitu hutumiwa kurejelea hali ya timu fulani kupata ushindi mkubwa dhidi ya nyingine huku msemo *kodoa macho* wenye maana ya kufungua macho sana kwa mshangao ukipewa matumizi ya timu husika kucheza kwa ukakamavu ili kuikera nyingine.

**Jedwali 2.10: Matumizi ya Tashihisi: Nomino**

| Data | Matini | Maana |
|---|---|---|
| Hasimu | Hii ni mechi kali inayotazamiwa kuwa ngumu sana kwa sababu inahusu timu | Hii ni mechi ngumu inayohusu timu pinzani tangu zamani. |

| | | |
|---|---|---|
| | hizi mbili mahasimu tangu jadi. | |
| Kiwete | Wenzangu mambo yanawaendea viwete hawa vibaya, washazamishwa mabao matatu bila jibu. | Timu hii hafifu imeshafungwa mabao matatu kwa sufuri. |

Timu hafifu hunasibishwa na *kiwete* ambaye ni binadamu aliyelemaa miguuni na asiyeweza kutembea. Hivi ni kusema kwamba hii ni timu legevu inayopoteza mechi zake nyingi. Timu zozote mbili zinazohusika katika mchezo huonekana kama *mahasimu* wanaopanga njama ya kuangamiza nyingine.

Vitenzi, nomino na semi hizi zimetumiwa kwa namna inayopanua maana yake ya kimsingi au halisi kulingana na tajriba za jamii inayozunguka watumiaji wake. Matumizi haya ya lugha hivyo basi, huonyesha kuwa lugha huwa na maana dhanishi kama inavyoelezwa na nadharia ya SAM.

### 2.3.4 Misemo/Nahau

Kwa mujibu wa Ngure (2003), misemo ni mafungu yenye maneno ya kawaida lakini ambayo huwa yamesitiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno hayo katika matumizi yake ya kawaida. King'ei na Kisovi (2005) wanaeleza misemo na nahau kuwa ni fungu la maneno lenye maana iliyofichika. Matei (2011) naye anasema kwamba misemo ni semi ambazo zinabeba ukweli wa kijumla na nahau ni fungu la maneno lenye maana ambayo haitokani moja kwa moja na maana za maneno yaliyoziunda. Wamitila (2004) anaeleza kwamba misemo na nahau ni

vifungu ambavyo hutumiwa kwa maana fulani ambayo huenda isiafikiane na maana halisi ya maneno yaliyohusishwa kwenye vifungu vyenyewe. Tofauti baina ya misemo na nahau ni kuwa nahau aghalabu huwa na muundo wa kirai kitenzi.

Misemo imetumika kama njia mojawapo ya kunogesha na kutia urembo lugha ya mchezo wa kandanda ili kuwavutia na kuwasisimua wasikilizaji wa matangazo ya mchezo huu. Utafiti wetu umedhihirisha matumizi ya misemo kama ifuatavyo:

**Jedwali 2.11: Matumizi ya Misemo Kutokana na Kitenzi Piga**

| Msemo | Matini | Maana |
|---|---|---|
| Piga bao | Kocha wa Arsenal apiga bao kushinda mechi ya leo. | Kocha wa Arsenal apanga mikakati ya kushinda mechi hii. |
| Piga deki | Anachengwa pale vibaya, defender huyo amepigishwa deki. | Mlinzi huyo amechengwa hadi akaanguka chini huku akijaribu kuinuka kwa mikono. |
| Piga pembe | Mchezo unamalizika kutoka uwanja huu wa Nyayo, leo hii Ulinzi yaipiga pembe Sofapaka. | Leo hii Ulinzi yaishinda timu ya Sofapaka kwa mabao mengi. |
| Piga randa | Bandari wanatoka hapa City Stadium vichwa vikiinamishwa, wamepigwa randa na Tusker wakalainika. | Bandari wameaibishwa kwa kushindwa na Tusker. |
| Piga risasi | Msikilizaji, Ulinzi inapigwa risasi nyingine hapa, inaonekana wanaendelea kulemewa. | Timu ya Ulinzi inafungwa bao jingine na wanaendelea kuzidiwa. |

Jedwali hili linaonyesha misemo iliyoundwa kutokana na kitenzi *piga*. Kinge'i na Ndalu (1988) wanaeleza kuwa msemo *piga bao* humaanisha kutabiriwa au kubashiriwa na kujulishwa yaliyopita na yajayo na mganga. Msemo huu unatumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kurejelea mipango na mbinu zinazotumiwa na timu au mkufunzi kujaribu kushinda mechi zao. *Piga deki* ni msemo unaolezwa na Kinge'i na Ndalu (1988) kuwa na maana ya kusafisha sakafu kwa maji huku msafishaji akiinama. Inatumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kurejelea mchezaji anayechengwa hadi akaanguka huku akijaribu kuamka ili kukimbilia mpira.

Msemo *piga pembe* wenye maana ya kusukuma kwa nguvu kwa pembe ili kujeruhi na *piga randa* wenye maana ya kulainisha mbao kwa randa hutumiwa katika lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda kwa maana ya kupata ushindi dhidi ya timu fulani. *Piga risasi* ni msemo unaomaanisha kupiga kwa bunduki au bastola kwa lengo la kuua. Msemo huu hutumiwa kurejelea hali ya kucheza mpira kwa nguvu kuelekea lango ili kufunga bao.

**Jedwali 2.12: Matumizi ya Misemo Mingine**

| **Msemo** | **Matini** | **Maana** |
|---|---|---|
| Kaba koo | Timu hizi mahasimu zimejitayarisha na naona ziko tayari kukabana koo. | Timu hizi pinzani ziko tayari kuonyeshana ushindani mkali kati yao. |
| Mezea mate | Mchezaji huyu matata ni mtamu kweli, si ajabu | Klabu nyingi za ngazi ya juu zinatamani/ zina nia ya |

| | | |
|---|---|---|
| | anamezewa mate na klabu nyingi za ligi kuu. | kumsajili/ kutafuta huduma za mchezaji huyu hodari. |
| Tia mkononi | AFC imetiwa mkononi na Sofapaka, imeshatandikwa hapa mbili nunge. | Timu ya AFC Leopards imezidiwa na timu ya Sofapaka katika mchezo na imeshafungwa mabao mawili kwa sufuri. |
| Achwa kwenye mataa | Anapenya pale, anachega, kiungo huyo ameachwa kwenye mataa. | Kiungo huyo amechengwa na kuachwa kama amezubaa. |
| Kufa na kupona | Msikilizaji wangu mechi hii ya fainali itakuwa ya kufa na kupona, hakuna timu itakayokubali kushindwa. | Mechi hii itakayoamua mshindi wa taji itakuwa ya ngumu sana kwani kila timu itajizatiti kuishinda. |
| Lala njaa | Mechi hii ngumu inaingia dakika ya themanini na tano lakini milango bado imelala njaa. | Mchezo unaelekea kumalizika lakini hakuna bao ambalo limefungwa katika lango lolote. |
| Kodoa macho | Jamani klabu hizi zinaendela kukodoleana macho kwenye mchezo huu mgumu. | Klabu hizi zinaendelea kushindana vikali kwenye mchezo. |
| Panga njama | Anaregesha mpira ule Wanyonyi hadi safu ya ulinzi ili kupanga njama ya kupangua ngome ya mahasimu wao... | Mchezaji Wanyonyi anacheza mpira walipo walinzi wa timu yake ili watafuta jinsi ya kufikia lango la timu pinzani. |

Jedwali hili linaonyesha misemo mingine inayotumiwa katika lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda. Kulingana na Kinge'i na Ndalu (1988), msemo *kaba koo* humaanisha kusongoa au hali ya kushika shingo kwa nguvu na kuiminya kwa lengo la kuua. Msemo huu hutoa dhana ya makabiliano au vita baina ya watu au makundi tofauti. Mchezo wa kandanda baina ya timu mbili huonekana kama vita

kwa sababu kila timu hujitahidi kupata ushindi. Msemo *mezea mate* humaanisha kuwa na hamu au tamaa ya kitu hasa chakula kitamu. Kila timu hutamani kuwa na wachezaji hodari wanaoweza kuzisaidia timu zao kupata ushindi. *Tia mkononi* ni msemo unaotumiwa kwa maana ya kupata au kushika. Msemo huu hutumiwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kumaanisha kuadhibu vikali. Kushindwa kwa timu katika mechi hasa kwa kufungwa mabao mengi kunanasibishwa na adhabu kali.

Msemo *lala njaa* wenye maana ya kupitisha usiku wote bila kula umetumiwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kumaanisha kuwa hakuna bao ambalo limefungwakatika lango lolote huku msemo *kodoa macho* wenye maana ya kufungua macho sana kwa mshangao ukipewa matumizi ya timu husika kucheza kwa ukakamavu ili kuikera nyingine. *Achwa kwenye mataa* ni msemo wenye maana ya kudanganywa au kuhadaiwa kwa hila. Msemo huu hurejelea hali ya kuchengwa kwa mchezaji hadi huzubaishwa na kuchanganyikiwa.

*Kufa na kupona* hutumiwa kurejelea kila namna, mbinu na nguvu zinazotumiwa na timu mbalimbali kushinda mechi ngumu huku msemo *panga njama* ukitumiwa kwa maana ya jinsi na mikakati inayotumiwa na timu fulani kufikia lango la timu pinzani. Maelezo haya yanaonyesha matumizi ya misemo hii katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kwa njia ya kipekee inayopanua na kugeuza maana yake tambuzi au halisi. Kwa hiyo, matumizi haya ya misemo hubainisha mhimili wa nadharia ya SAM inayosema kuwa lugha huwa na maana dhanishi.

### 2.3.5 Misimu/Simo

Wamitila (2004) anarejelea misimu kama maneno ya kimafumbo ambayo huficha maana yake na hivyo huhitaji uchanganuzi kuyatambua. Anaeleza kuwa kimsingi, misimu ni semi zinazohusishwa na kikundi kidogo cha wanajamii katika matumizi yao yasiyo rasmi. Matei (2011) anaeleza misimu kama semi za muda zinazobuniwa na kutumiwa katika mazingira maalum na kipindi mahsusi. Misimu hutofautiana kutegemea wahusika. Kwa mfano, vijana mtaani, wanafunzi shuleni au utingo barabarani huwa na misimu inayowatambulisha.

Ngure (2003) anafafanua misimu kuwa maneno au misemo ambayo huzuka ghafla wakati fulani hasa kufuatana na matukio maalum ya wakati au msimu huo. Katika sajili ya mchezo wa kandanda, baadhi ya misimu inayotumiwa huihusisha na vita, uhasama au makabiliano kama ilivyobainishwa katika Jedwali 2.1.3.

**Jedwali 2.13: Matumizi ya Misimu Inayohusisha Mchezo wa Kandanda na Makabiliano**

| Msimu | Matini |
|---|---|
| Vunja ngome | Mshambulizi amepenya/ amevunja ngome ya adui wao na kufunga bao. |
| Angusha bomu | Mshambulizi huyo ameangusha bomu zito lililomlipua kipa. |
| Pokonya silaha | Timu hii ya Tusker inapokonywa silaha timu ya AFC Leopards. |
| Haribu sura | Klabu ya Ulinzi yaharibu sura Bandari kwa kuinyuka hapa goli tatu bila. |
| Ingia jehanamu | Klabu hii ya Man United imeingia jehanamu katika mechi tatu zilizopita. |

| | |
|---|---|
| Laliwa manowari | Anakwenda, anakwenda lakini analaliwa manwari. |
| Vunja benki | Msikilizaji, timu hii ya Arsenal ilivunja benki ili kumnunua staa Ozil. |
| Achilia kombora | Anajivuta na kuachilia kombora nzito kutoka katikati ya uwanja kuelekea langoni-ii, inatoka nje! La! |

Jedwali hili linaonyesha misimu inayohusiana na istilahi za zana za vita au madhara yanayotokana na vita. *Angusha bomu* na *achilia kombora* ni misimu yenye maana ya kupiga mpira kwa nguvu kiasi cha kutoweza kuzuiliwa na mlinda lango. Kwa mfano, matini "Mshambulizi huyo ameangusha bomu zito lililomlipua kipa" inamaanisha kuwa mshambulizi huyo amepiga mpira kwa nguvu na kumfunga mlinda lango. Aidha, *laliwa manowari* ni msimu unaomaanisha hali ya mchezaji fulani kuchezewa visivyo kwa kuangushwa. Misimu *pokonya silaha* na *haribu sura* inarejelea hali ya kushindwa kwa timu kwa kufungwa mabao mengi huku *ingia jehanamu* ikionyesha hali ya timu fulani kuandikisha msururu wa matokeo mabaya. Kwa mfano, matini "Klabu ya Ulinzi yaharibu sura Bandari kwa kuinyuka hapa goli tatu bila" inamaanisha kuwa Klabu ya Ulinzi imeishinda ile ya Bandari vibaya kwa kuifunga mabao matatu kwa nunge.

*Vunja ngome* ni msimu wenye maana ya wachezaji wa timu fulani kupita safu ya nyuma ya timu pinzani ili kufunga ilhali *vunja benki* ukiwa na matumizi ya timu fulani kujitolea au kuamua kutumia kiasi kikubwa cha fedha ili kupata huduma za mchezaji maarufu. Matini "Msikilizaji, timu hii ya Arsenal ilivunja benki ili kumnunua staa Ozil" inarejelea hali ya klabu ya Arsenal kutumia pesa nyingi ili kumsajili mchezaji mahiri Ozil.

Hali kadhalika, baadhi ya misimu inayozuliwa na kutumika katika sajili ya mchezo wa kandanda huhusu hali na matukio ya mchezo huu unapofanyika kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2.14: Matumizi ya Misimu Inayohusiana na Matukio ya Mchezo**

| Msimu | Matini |
|---|---|
| Umiza nyasi | Timu hizi ziliumiza nyasi bure msimu uliopita, lakini mechi ya leo tumeshaona mabao matatu. |
| Lamba mchanga | Klabu ya Ulinzi imelambishwa mchanga na City Stars. |
| Pika bao | Mchezaji huyu machachari ambaye amepika mabao mengi msimu huu anaendelea kuonyesha umahiri wake. Leo amepika mawili. |
| Pora mpira | Wanang'ang'ana pale kwenye katikati ya uwanja, Arteta anampora mwenzake mpira na kuucheza mbele. |
| Rudisha mkono | Ulinzi wanafunga na kurudisha mkono hapa. Mabao ni moja kwa moja. |
| Nawa mpira | Hatari hii, difenda amenawa mpira ndani ya box, ni penalty. |
| Sugua benchi | Namwona Kagawa pale kwa bench. Mchezaji huyu siku hizi anasugua benchi kutokana na mchezo wake hafifu. |
| Mega/gawa mpira | Anatuliza mpira maridadi kifuani, anammegea mwenzake mpira pale mbele |
| Visha kanzu | Anachukua mpira ule, anakwenda nao, anamvisha kanzu pale, anamvisha ya pili... |
| Jenga kibanda | Wanakwenda pale lakini wanajenga kibanda katika eneo la wenzao bila idhini. |
| Badilisha mita bendi | Kiungo huyu anakwenda, anabadilisha mita bendi hadi wingi wa kulia. |
| Pasha misuli moto | Chelsea inataka kuongeza makali hapa. Naona wachezaji wa akiba wanapasha pale misuli moto. |

Lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda huibua na kutumia misimu kuelezea hali na matukio ya mchezo wenyewe. Misimu iliyochanganuliwa katika Jedwali hili imeundwa kwa kitenzi na nomino. Misimu *umiza nyasi* hutumiwa kurejelea hali ya timu mbili kucheza bila kufungana bao lolote, *lamba mchanga* kumaanisha timu kushindwa vibaya, *pika bao* kumaanisha kuandaa nafasi nyingi na nzuri za kufunga bao, *pora mpira* kurejelea hali ya mchezaji kumpokonya mwenzake mpira na *nawa mpira* kwa maana ya mchezaji kushika au kugusa mpira kwa mkono. Kwa mfano, matini "Mchezaji huyu machachari ambaye amepika mabao mengi msimu huu anaendelea kuonyesha umahiri wake. Leo amepika mawili" inamaanisha kuwa mchezaji huyu hodari ambaye ametoa pasi nzuri au kuandaa nafasi nyingi za kufunga msimu huu anaendelea kuonyesha ubora wake kwa kuandaa nafasi zilizozalisha mabao mawili.

Hali kadhalika, misimu *rudisha mkono* hutumiwa kumaanisha kusawazisha bao, *sugua benchi* kurejelea hali ya mchezaji kutopata nafasi nyingi za kucheza kutokana na kushindwa kuonyesha mchezo mzuri, *mega/gawa mpira* kwa maana ya kutoa pasi nzuri, *visha kanzu* kuonyesha uwezo wa mchezaji kumchenga mwenzake kwa kupitisha mpira juu yake huku msimu *jenga kibanda* ikirejelea mchezaji wa timu moja kupatikana katika eneo la timu nyingine wakati usiofaa. "Namwona Kagawa pale kwa 'bench'. Mchezaji huyu siku hizi anasugua benchi kutokana na mchezo wake hafifu" ni matini inayomaanisha kuwa mchezaji Kagawa siku hizi hapati nafasi ya kucheza kutokana na kiwango cha mchezo wake kushuka.

Msimu *badilisha mita bendi* hurejelea tendo la kucheza mpira kutoka safu moja ya uwanja hadi nyingine Aidha, *pasha misuli moto* ni msimu inayotumiwa kurejelea hali ya wachezaji wa ziada kujiandaa ili kuchezeshwa kwa kunyosha viungo. Matini "Chelsea inataka kuongeza makali hapa. Naona wachezaji wa akiba wanapasha pale misuli moto tayari kuingia" inamaanisha kuwa wachezaji wa ziada wa timu ya Chelsea wanajitayarisha kuingia uwanjani ili kuimarisha mchezo wa timu yao kwa kunyosha miguu.

Misimu inayohusisha mchezo wa kandanda na makabiliano katika Jedwali 2.13 na ile inayohusiana na matukio ya mchezo katika Jedwali 2.14 ni ile inayochukua muundo wa Kitenzi-Nomino. Jedwali lifuatalo linaonyesha misimu isiyochukua muundo wa Kitenzi-Nomino katika utoshelevu wake wa kimatumizi kwenye sajili ya mchezo wa kandanda.

**Jedwali 2.15: Matumizi ya Misimu Isiyochukua Muundo wa Kitenzi-Nomino**

| Msimu | Matini | Maana |
|---|---|---|
| Cheka na wavu | Anakwenda na mpira, anakwenda van Persie-eee anacheka na wavu msikilizaji. | Mshambulizi van Persie anakwenda na mpira na kufunga bao. |
| Toa ndani weka katikati | Timu ya City Stars inatoa ndani na kuweka katikati tena. Ulinzi mbili, City Stars bila. | Timu ya City Stars inaanzisha tena mchezo baada ya kufungwa bao la pili na Ulinzi. |
| Mpira wa madhambi | Anajaribu kupenya ngome ile... anaangushwa. Mpira wa | Mpira utachezwa kuelekea lango la Sofapaka kwa |

| | | |
|---|---|---|
| | madhambi utachezwa kuelekea lango la Sofapaka. | sababu wachezaji wake walicheza visivyo. |
| Mpira kuwa mwingi | Anafuata mpira ule , anajaribu kuuzuia lakini unakuwa mwingi na kutoka nje. | Mchezaji anafuata mpira ili kuudhibiti lakini unamzidi kasi na kuelekea nje ya uwanja wa mchezo. |
| Kipindi cha lala salama/lala kwa mkono wa buriani | Msikilizaji wangu ukiwa kando ya redio yako, tunaingia kipindi cha lala salama. Timu hizi zinaanza kuingiwa pressure hapa ya kupata bao. | Timu zinaanza kuingiwa wasiwasi kwa sababu mchezo umeingia kipindi cha pili lakini hazijafunga bao lolote. |
| Kucheza na shilingi karibu na shimo | Wanacheza kule nyuma pole pole hawa Mashetani Wekundu. Hawana haraka kwa sababu wako mbele...Anafunga bao la kushawazisha katika dakika za majeruhi...Manchester United wamecheza na shilingi karibu na shimo na ikaingia ndani. | Timu ya Manchester United imecheza bila uangalifu kwa kuwa walishafunga na muda wa mchezo ulikaribia kumalizika lakini wenzao wameshawazisha bao katika dakika ya ziada kwa sababu ya mzaha wao. |

Misimu iliyochanganuliwa katika jedwali hili ni ile isiyo na muundo wa Kitenzi-Nomino. Hivi ni kusema kuwa misimu hii inachukua sura ya maelezo. Msimu *badilisha mita bendi* hurejelea tendo la kucheza mpira kutoka safu moja ya uwanja hadi nyingine huku *mpira kuwa mwingi* ukimaanisha mpira kuchezwa na kudingiria hadi nje ya uwanja. Msimu *cheka na wavu* humaanisha kufunga bao ilhali *toa ndani weka katikati* ikirejelea kufungwa bao. *Mpira wa madhambi* ni mpira unaochezwa kuelekea lango fulani kutokana na au kama adhabu ya mchezo mbaya.

Aidha, *pasha misuli moto* ni msimu inayotumiwa kurejelea hali ya wachezaji wa ziada kujiandaa ili kuchezeshwa kwa kunyosha viungo huku *kipindi cha lala salama* au *lala kwa mkono wa buriani* ikitumiwa kwa maana ya kipindi cha pili cha mchezo ambapo wachezaji hujizatiti kupata ushindi. *Kucheza na shilingi karibu na shimo* ni misimu inayoangaliwa sawa na kutomakinika katika mchezo kwenye eneo la lango ambapo bao linaweza kufungwa. Tazama Kiambatisho 1 kwa mifano zaidi.

Kwa jumla, misimu hii yote imetumiwa kwa njia ya kipekee na ya kitamathali katika sajili ya mchezo wa kandanda kuibua maana hamishwa au geuzwa inayoeleweka tu na wanaohusika na mchezo huu, yaani watangazaji na wasikilizaji. Hivi ni kusema kuwa maana halisi ya lugha inayotambuliwa na nadharia ya SAM inapanuliwa kulingana na muktadha wa matumizi. Hali kadhalika, matumizi ya misimu katika utangazaji wa mchezo wa kandanda ni njia mojawapo inayowawezesha watangazaji kujinasibisha na kujitambulisha na wasikilizaji wao na hivyo kudhihirisha maana tagusani inayotambuliwa na nadharia ya SAM.

Misimu hii hivyo basi hujitokeza kama misemo miteule ambayo huweza kushika kani na kukita mzizi kama sehemu ya misemo ya lugha sanifu ya Kiswahili. Kwa njia hii, uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda huweza kuchangia ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwa jumla.

### 2.3.6 Methali

Matei (2011) anaeleza kuwa methali ni semi fupi fupi za kimapokeo zenye kueleza fikra, maarifa, hekima na mafunzo yanayotokana na uzoefu wa jamii mahsusi. Ngure (2003) anaeleza methali kama semi fupi zenye maana fiche zinazokubalika na kutumiwa kufafanua ukweli na hekima ya jamii. Gichohi na Kagwa (2007) wanafafanua methali kuwa semi fupi inayotumiwa kwa busara na iliyo na maana ya fumbo na ambayo inapofasiriwa hupata mizizi katika jamii inayotumika. Wamitila (2004) naye anasema kuwa methali ni msemo wa kimapokeo ambao una muundo mahsusi, unaokumbukika na unaokusudia kuelekeza, kuadibu, kusuta, kulaumu na kushauri.

Kwa jumla, methali hujitokeza kama semi za kimapokeo zenye muundo maalum, zinazodhihirisha hekima ya jamii na zinazotumiwa kupigia mfano maisha ya jamii. Methali huhusishwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda katika kuonyesha hali ya mchezo, jinsi mchezo unavyoendelea, unavyobadilika na kukamilika. Data tuliyochanganua inaonyesha matumizi ya methali kama ifuatavyo:

1. Anasonga pale na mpira, anachenga, anapiga goo-oool! Ndugu msikilizaji, *hayawi hayawi huwa.* Timu hii imetafuta bao kwa nguvu, wakapoteza nafasi kadha za kufunga, kipa akiokoa mikwaju kama mitano hivi, lakini sasa hawa wanapenya ngome yake, wanafunga goli maridadi hapa.

Methali hii inayoelezwa na Ndalu na King'ei (1989) kuwa na maana ya 'jambo lisiloonekana kama halitatokea mwisho huja kutokea' imetumiwa kumaanisha



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kuwa timu inayorejelewa hatimaye imefaulu kufunga bao baada ya kujaribu mara kadha.

2. Mpenzi msikilizaji, amini usiamini timu hii ya Nakuru Top Fry iliyopandishwa daraja majuzi kuingia ligi kuu inapata bao la pili. Mabingwa watetezi Gor wanakaangwa hapa. Hakika *usione wembamba wa reli gari moshi hupita.*

Ndalu na Kinge'i (1989) wanaeleza maana ya methali hii kuwa 'usimdharau mtu kwa kumwona duni kwani anaweza kuwa na nguvu au uwezo mkubwa.' Methali hii imetumiwa kumaanisha kuwa timu ya Nakuru Top Fry inayoonekana changa na hafifu kwa sababu ya kupandishwa daraja kutoka ligi ya chini imeishinda timu kubwa ya Gor Mahia ambao ndio mabingwa watetezi.

3. Mchezo unamalizika hapa, na mabingwa watetezi Gor wanasalimu amri. Nakuru Top Fry mbili, Gor moja. Naona wachezaji wa Gor wakisalimiana na wenzao, ishara kuwa *asiyekubali kushindwa si msindani.*

Methali hii imetumiwa kuonyesha kuwa timu ya Gor Mahia inayotetea ubingwa wa ligi ilikubali kuzidiwa na wenzao wa Nakuru Top Fry katika mchezo.

4. Anaipokea pasi ile vizuri na kutuliza mpira. Anapenya pale, anachenga moja, mbili, anapigwa kiatu anakubali kwenda chini. Anagaragara pale chini kwa maumivu. Naona daktari wa timu yake anaingia uwanjani upesi

kumpa *gangaganga ya mganga ambayo humwacha mgonjwa na matumaini.* Haya!

Kwa mujibu wa Ndalu na King'ei (1989), methali hii inamaanisha kuwa msaada wa mara kwa mara humpa mtu matarajio ambayo aghalabu yanadumu. Methali hii imetumiwa kuonyesha kuwa mchezaji anayetibiwa baada ya kuumizwa na mwenzake uwanjani huamini kuwa amepona na huwa na moyo wa kuinuka na kuendelea kucheza.

5. Wanachukua mpira katikati ya uwanja, wanatambariza, wanakwenda, wanacheza hapa pasi za kuonana hawa, wanaingia ndani ya box, anatuma mkwaju mkali la! la! la! Goo-ooool! Salaale! Msikilizaji mpendwa timu hii ya Tusker ilianza kumiliki mchezo tangu mwanzo, na kwenye dakika ya ishirini na moja, wanapata bao la kwanza. Kweli *siku njema huonekana asubuhi.*

Kulingana na Wamitila (2001), methali hii huwa na maana kuwa 'mtu hujua kuwa siku fulani itakuwa njema kwake kutokana na dalili za asubuhi.' Methali hii imetumiwa kwa maana kwamba timu ya Tusker ilianza kuonyesha dalili nzuri ya kufunga bao kwa kucheza vizuri kuanzia mwanzo wa mchezo na hatimaye kufanikiwa.

6. Msikilizaji *dalili ya mvua ni mawingu,* timu hii ya Arsenal ilianza vibaya mchezo wa leo kwa kupoteza mipira mingi kwa hawa wapinzani wao wa

Chelsea. Beki wao wa kushoto pia akalishwa nyekundu kwa kushika mpira ndani ya box. Si ajabu ndani ya dakika kumi na tano wako nyuma magoli matatu bila jibu.

Methali hii inayoelezwa na Ndalu na King'ei (1989) kuwa na maana ya 'mawingu yatandapo huwa dalili kwamba kutanyesha.' Methali hii imetumiwa kumaanisha kuwa timu ya Arsenal ilianza kuonyesha ishara za kupoteza mechi kuanzia mwanzo kwa kuwa walipoteza mpira mara kadha kabla ya mlinzi wao kuondolewa uwanjani kutokana na mchezo mbaya.

7. Anachukua mpira pale na kummegea mwenzake, wanacheza haraka haraka wakitafuta bao la ushindi, wanakwenda, wanapenya, hatari, hatari kwenye lango-ooo goo-oool! Huu ni miujiza msikilizaji, walikuwa wamefungwa hapa mabao mawili timu ya AFC Leopards, wanatoka nyuma na kuizaba Bandari mabao matatu kwa mawili. Waswahili husema *usione simba kanyeshewa ukadhani paka,* Leopards wanarudi hapa kwa vishindo. Kweli *kutangulia si kufika.*

Ndalu na King'ei (1989) wanaeleza maana ya methali ya kwanza kwamba 'haifai kumdharau mtu shujaa au mwenye nguvu kwa kuwona hali yake imekuwa mbaya kwani bado anazo sifa zake hizo'. Wanaeleza methali ya pili kuwa 'mtu anapotangulia katika jambo fulani haimaanishi kuwa ndiye atakayemaliza wa kwanza.' Methali hizi zimetumiwa kuonyesha kuwa klabu yenye umaarufu huwa

na ujasiri wa kujikakamua kupata ushindi hata inapoanza mchezo vibaya na kufungwa kwanza.

8. Mpendwa msikilizaji kweli *mcheza kwao hutuzwa*. Mchezo unamalizika hapa, Gor inapata ushindi mwingine hapa, inaichapa Sony Sugar katika uwanja wao wa nyumbani wa City kwa mabao mawili kwa sufuri. Kwa mara nyingine Sony inakuwa *jogoo wa shamba asiyeweza kuwika mjini.*

Kwa mujibu wa Wamitila (2001), methali ya kwanza inamaanisha kuwa 'mtu anayecheza kwao hupewa zawadi au hutunzwa vizuri.' Kuhusu methali ya pili, anaeleza kuwa 'jogoo la shamba linapopelekwa mjini hushindwa kuwika kwa kuwa katika mazingira mapya.' Methali hizi zimetumiwa kumaanisha kuwa timu inayocheza katika uwanja wake wa nyumbani huwa na uwezekano mkubwa wa kushinda mechi kuliko timu iliyotoka kwingineko. Hii ni kwa sababu uzoefu wa mazingira yao na uungaji mkono na mashabiki wao wengi.

9. Wanacheza nyuma kule pole pole hawa Mashetani Wekundu. Hawana haraka kwa sababu wako mbele. Wanapiga katika duara la katikati kwake Carrick. Anapokonywa ule mpira na nani yule Lalana, anatoka mbio, anampatia Kim, anakwenda, anaachilia bado-oo goo-ool! Amini usiamini, Mkorea huyu Kim anaweka gozi lile ndani ya wavu! Anafunga bao la kusawazisha katika dakika za majeruhi. Jamani Waswahili walishauri dhidi ya *kukata ubeleko kabla ya mtoto kuzaliwa.* Manchester United

wamecheza na shilingi karibu na shimo na ikaingia ndani. Cardif City mbili, Manchester United mbili.

Methali hii ambayo Wamitila (2001) anasema kuwa inaonya dhidi ya kujivunia vitu ambavyo hatujapata imetumiwa kumaanisha kuwa timu ya Manchester United ilicheza kwa uzembe na bila uangalifu katika dakika za mwisho wa mchezo kwa kufikiri kuwa wangeshinda mechi lakini wakaishia kwenda sare.

### 2.4 Maswali ya Balagha

Japo istilahi hii imefasiriwa kwa namna anuai na wataalamu tofauti, Leech (1969) na Richards na wengine (1985) wanaafikiana kuwa maswali ya balagha ni kauli zilizo na nguvu zikiwa katika muundo usiohitaji majibu. Leech (1983) anasema kuwa maswali ya balagha ni maneno yanayotumiwa kuchochea fikra fulani na kuibua majibu na kutoa athari ya ndani kwa ndani kwa mpokeaji wa ujumbe.

Habwe (1999) anasema kwamba maswali ya balagha huonekana kuwa na mvuto wa juu kama lina pengo la ujumbe na hivyo basi huweza kuhitaji jibu. Anaendelea kusema kwamba maswali ya balagha hutumiwa na mzungumzaji anapohitaji kutawala au kuchochea hisia za watu wafikirie zaidi. Anaafikiana na Goody (1978) anayeangazia uamilifu wa maswali kama mbinu inayoathiri uwezo wa kupanga na kuwasilisha ujumbe kwa njia toshelevu.

Maswali ya balagha huamilishwa kama kifaa cha kiisimu cha kufikirisha, kupasha ujumbe na kutoa maana. Tannen (1984:20) anasema:

> Iwapo mzungumzaji katika mahusiano anatumia kifaa ambacho anayekisikiliza huelewa kama ilivyodhamiriwa, basi hali ya kujitambulisha kipragmatiki hujitokeza.(Ty).

Data ifuatayo inaonyesha baadhi ya maswali ya balagha yanayohusishwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda.

1. ... anaingia katika kisanduku kile lakini anacheza nje. Ilikuwa nafasi ya wazi na unajiuliza *ni kwa nini hakufunga bao hilo?*
2. Salaale! *Ajabu gani hii?* He only had the net to beat lakini anajaza nje! La!
3. ... wanamenyana pale, anamshika mwenzake jezi na kumwangusha chini. *Jamani ni mchezo gani huu?*
4. ... anapata pasi na kusonga nao, anapiga mbele vibaya. Aaah! *Hii ni pasi ya aina gani wasikilizaji?*
5. ...anapata mpira peke yake-eee lakini anakosa bao la wazi. Inashangaza wapenzi wasikilizaji. *Kwani lango lile kubwa mchezaji huyu hana macho?*
6. ...ananyunyiza palee-ee... *Sasa anacheza wapi ule mpira?*
7. ...*anamtilia nani yule-ee* anachukua Carrick, Carrick anakwenda...
8. *Anachanja pale goal kick kwake nani,* anachukua Rama Salim katikati ya uwanja...

9. *...anapiga wapi palee-ee* wanakwenda kwenye wingi wa kulia Ulinzi Stars...

Maswali "Ni kwa nini hakufunga bao hilo?", "Ajabu gani hii?" na "Kwani lango lile kubwa mchezaji huyu hana macho?" yanaonyesha kutamauka kwa mtangazaji anayeona nafasi za wazi ya kufunga bao zinapopotezwa. Maswali "Jamani ni mchezo gani huu?" na "Hii ni pasi ya aina gani wasikilizaji?" nayo yanatumiwa na watangazaji kuonyesha kutoridhishwa kwao kutokana na uchezaji mbaya wa mpira. Aidha, balagha hizi zina uamilifu wa kukejeli wachezaji wanaohusika na hivyo kuathiri jinsi mashabiki wanavyowachukulia na kuhusiana na wachezaji hawa. Hali hii inaakisi nadharia ya SAM inayosema kuwa lugha huwa na maana tagusani.

Maswali "anamtilia nani yule-ee?", "anachanja pale goal kick kwake nani?" na "anapiga wapi palee-ee?" hujitokeza kama sehemu ya mfululizo wa matangazo ya mchezo wa kandanda. Maswali yanaonyesha hali ya watangazaji kutokuwa na hakika kuhusu majina ya wachezaji au kutoweza kuwaona vizuri wachezaji waliohusika katika tukio fulani la mchezo.

Maswali mengine ya balagha ni yale yanayokisiwa na watangazaji kuwa yanatokea kati ya wachezaji na waamuzi uwanjani. Maswali haya huulizwa na wachezaji kwa waamuzi wanaotoa adhabu dhidi ya mchezo mbaya au usiozingatia sheria au kwa wachezaji wenzao wanoonyesha mchezo mbaya. Data ifuatayo inadhihirisha hali hii.

1. Anakwenda pale kwenye lango-oo, analazwa chini. Refarii anasema ni penalty! Naona mchezaji aliyeadhibiwa akimwendea refarii kwa hamaki na kumuuliza, "*Unasema ni nani amemwangusha? Kwa nini unasema ni penalty na mimi sijamgusa? Huoni kuwa amejiangusha? Nani anastahili nyekundu?* Mimi sikubaliani na uamuzi wako."

2. Anamegewa pasi nzuri mbele, anaingia pale-ee na kibendera kile kiko juu, ameotea. Mchezaji yule anamchemkia mbeba kibendera. Ni kana kwamba anamfokea. Anamuuliza, "*ni kwa nini unabeba kibendera na mimi sikuotea? Mbona unanionea?*"

3. Anachukua mpira katikati ya uwanja, anachenga moja, anakwenda, anachezewa visivyo na kuangushwa lakini refa anaashiria mchezo uendelee. Mchezaji yule anamfuata refarii, ni kama anamuuliza, "*ni kwa nini nachezewa vibaya na huoni? Ama unawapendelea?*"

4. Kipa anaanzisha mpira mrefu katikati ya uwanja-aa wanaruka pale kupiga kichwa na anaangushwa chini. Mchezaji anagaagaa chini kwa maumivu, anashika kichwa....Rooney anamwendea Kompany na kumkemea, "*mbona unanipiga mkumbo? Unataka kuniumiza?*"

5. ...anatiliwa pasi murua na kuingia maridadi. Anacheza kule-eee anaangushwa ndani ya box. Amini usiamini, refa anaashiria mchezo

uendelee. Difenda yule anamwendea Wallcort na kumfokea, ni kama anamwambia, *"ni kwa nini unajiangusha? Unataka penalty au kilishwe nyekundu?"*

Maswali haya ya balagha hujtokeza kama mwendelezo wa kauli mfululizo za utangazaji wa mchezo wa kandanda kwa sababu ya kasi ya mchezo huu. Maswali haya yanaonyesha hamaki na kutoridhika kwa wachezaji kutokana na maamuzi ya refarii kama inavyodhihirika katika maswali 1, 2 na 3 au kuudhika na wachezaji wenzao wanaowachezea visivyo kama inavyodhihirika katika maswali 4 na 5. Maelezo yanaafiki uamilifu husishi wa lugha kama mfumo unaoweza kuibua hisia za kuudhika.

Japo maswali ya balagha hayahitaji kujibiwa, anayeulizwa aghalabu hujijibu nafsini mwake. Goody (1978) anasema kuwa mbinu ya maswali huathiri uwezo wa kupanga na kuwasilisha ujumbe. Hii ina maana kuwa anayeulizwa swali huyapanga na kutoa mawazo yake kwa njia toshelevu na hivyo kustawisha mahusiano miongoni mwa wahusika ambao ni wachezaji, waamuzi, watangazaji na wasikilizaji. Dhima hizi zinayakinisha mhimili wa nadharia ya SAM inayosema kuwa lugha huibua maana tagusani. Kimtindo, maswali ya balagha hutumiwa huamsha mshawasha na hamu ya wasikilizaji ili kuendelea kusikiliza matangazo ya mchezo. Aidha, maswali haya huvuta nadhari ya msikilizaji ili kumakinikia matangazo.

### 2.5 Tafsiri Sisisi

Hii ni mbinu nyingine ya mawasiliano katika sajili ya mchezo wa kandanda. Tafsiri inaelezwa na Catford (1965) kama uwekaji wa vipashio au maneno ya lugha pokezi ili kuchukua nafasi ya yale ya lugha changizi. Tafsiri sisisi nayo inaelezwa na Njogu na wengine (2006) kama ile ya neno kwa neno ya istilahi ya lugha changizi. Wanaendelea kusema kuwa tafsiri sisisi inayotokea sana katika dhana zisizo na visawe au zenye muundo wa kimaelezo wakati mwingine huwa na uwezekano wa kupotosha ujumbe. Tafsiri sisisi inayojitokeza katika lugha ya sajili ya mchezo wa kandanda hutokana na upungufu wa misamiati mwafaka katika lugha ya Kiswahili inayoweza kutumiwa katika utangazaji.

**Jedwali 2.16: Matumizi ya Tafsiri Sisisi Zinazohusu Hali ya Mchezo na Usajili wa Wachezaji**

| Neno | Tafsiri sisisi | Matini |
|---|---|---|
| Golden boot | Kiatu cha dhahabu | Anapokea mpira, anakwenda pale Suare-ee-z, anafunga bao maridadi. Mchezaji huyu hatari yuko mbioni kijinyakulia tuzo ya *kiatu cha dhahabu*. Sasa amefunga mabao ishrini na sita. |
| Transfer window | Dirisha la uhamisho | Anatuliza mpira ule kwenye gamba la kifua, anachenga moja, anachenga mbili, tatu, la! Jamani mchezaji huyu anaonyesha ni kwa nini timu zilimng'ang'ania sana katika *dirisha la uhamisho* wa msimu huu. |
| Inside the box | Ndani ya kisanduku | Mshambulizi huyo anasonga, anaingia *ndani ya kisanduku* kile-ee anaangushwa. Penalty! |
| Player on | Mchezaji wa | Anakwenda, anaingia pale Lukaku-uu anapiga |

| | | |
|---|---|---|
| loan | mkopo | go-oool. Msikilizaji, *mchezaji huyu wa mkopo* anarudi Stamford Bridge kuiroga Chelsea. Ajabu! |
| Buying a player | Kununua mchezaji | Anachukua mpira ule Ozil, anatuliza, anaangalia ancheze wapi, anababaisha pale, anatoa pasi murua kwake Podolski. Msikilizaji Arsenal haikupoteza kwa *kumnunua kiungo huyu* kutoka Real Madrid. |
| Selling a player | Kuuza mchezaji | Anamegewa mpira mzuri katika eneo la hatari-ii Giroud anakosa nafasi ile ya wazi. Arsenal inaonekana kukosa makali tangu *iuze mshambulizi* wake van Persie. |
| Injury time | Muda wa majeruhi | Msikilizaji dakika zangu tisini nazimaliza, zilizobaki ni *muda wa majeruhi* za refarii. Anaongeza hapa dakika nne. |

Maneno au virai *Golden boot, Transfer window* na *Inside the box* yametafsiriwa moja kwa moja lakini yametumiwa kutoa maana tofauti na tafsiri hizo. *Golden boots* iliyotafsiriwa kama 'kiatu cha dhahabu' ni kirai kinachotumiwa kumaanisha tuzo anayopewa mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi katika msimu. *Transfer window* iliyotafsiriwa kama 'dirisha la uhamisho' limetumiwa kwa maana ya muda maalumu wa miezi mitatu wa usajili wa wachezaji wapya. *Inside the box* iliyotafsiriwa kama 'ndani ya kisanduku' humaanisha eneo lililo karibu na lango lenye yadi kumi na nane na ambapo adhabu ya penalti hutolewa iwapo mchezaji wa timu pinzani amechezewa visivyo au wachezaji wengine ambao sio mlinda lango wanaposhika mpira.

Matumizi ya virai *Player on loan, Buying a player* na *Selling a player* vimetafsiriwa na kutumiwa kwa njia inayosawiri wachezaji kama bidhaa au mali zinazoweza kufanyiwa biashara sokoni ili kupata huduma zake au faida. Hali kadhalika, kirai *Injury time* kinachotafsiriwa kama 'muda wa majeruhi' ni dakika chache za ziada zinaoongezwa na mwamuzi ili kufidia muda wowote ambao huenda haukutumiwa katika mchezo kwa sababu ya mpira kupigwa nje ya uwanja, wachezaji kutibiwa kutokana na kuchezewa visivyo au mwamuzi kusemezana na wachezaji.

Lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda pia husheheni tafsiri sisisi inayohusu lakabu zinazotumiwa kurejelea na kusifia klabu mbalimbali za kandanda.

**Jedwali 2.17: Matumizi ya Tafsiri Sisisi Inayohusu Lakabu za Klabu za Kandanda**

| Neno | Tafsiri sisisi | Matini |
|---|---|---|
| The Red Devils | Mashetani Wekundu | Mchezo unaelekea kuanza hapa msikilizaji. Leo hii *mashetani wekundu* wanawaalika majirani zao na watani wa jadi Manchester City. |
| The Gunners | Wanabunduki | Wanaanza mchezo hapa kwa kasi Arsenal. Wanaingia pale na kuvurumisha kombora kali. La! *Wanabunduki* hawa wanaonyesha nia ya mapema ya kushinda mechi hii. |
| The Reds | Wekundu | Mchezo unatokota hapa msikilizaji, *Wekundu* hawa leo wanona nyekundu katika uwanja wao wa nyumbani. Kufikia sasa wako nyuma mabao |

| | | |
|---|---|---|
| | | mawili<br><br>kwa mtungi. |
| The Blues | Wanasamawi | Wapenzi wasikilizaji mchuano huu kati ya *Wanasamawi* na majirani zao wanabunduki unatazamiwa kuwa mkali sana ikizingatiwa kuwa timu nne za mwanzo zimetengwa na pointi tatu pekee. |
| The Black Cats | Paka Weusi | Amini usiamini, hawa *paka weusi* wanaona weusi katika uga huu wa Wembley. Wanabunduki wanatoka nyuma na kufunga bao la ushindi katika muda wa ziada wa fainali hii ya Kombe la FA. Arsenal tatu, Hull City mbili. |
| The Hammers | Wananyundo | Msikilizaji mpira unamalizika hapa Etihad Stadium, Man City wanaibuka washindi na kutawazwa mabingwa wapya wa Ligi Kuu ya Uigereza. Wanawachapa *wananyunda* magoli mawili kwa moja. |

Maneno *The Red Devils, The Gunners, The Reds, The Blues, Paka Weusi* na *Wananyundo* ni lakabu za timu za Uingereza ambazo ni Manchester United, Arsenal, Liverpool, Chelsea, Hull City na West Ham mtawalia. Lakabu hizi nazo zimetafsiriwa moja kwa moja na watangazaji wa mchezo huu kama 'Mashetani Wekundu', 'Wanabunduki', 'Wekundu', 'Wanasamawi', 'Paka Weusi' na 'Wananyundo' mtawalia ili kuonyesha umahiri, nguvu na uwezo wa kipekee wa klabu hizo. Kwa mfano, uwezo wa timu ya Arsenal wa kufunga mabao unamithilishwa na kuzipiga timu pinzani risasi kwa kutumia bunduki huku ule wa timu ya West Ham wa kushinda mechi ukilinganishwa kuzipiga timu nyingine kwa nyundo. Hali kadhalika, lakabu za 'Mashetani Wekundu' na 'Paka Weusi'

zinadhamiriwa kutisha timu zinazocheza na timu ya Manchester United na Hull City kwa kuzihusisha na viumbe wanaoogofya.

Lakabu hizi pia zinaoana na rangi ya sare za timu husika, nembo au kauli mbiu zao. Inajitokeza kuwa rangi ya sare za timu ya Chelsea ni samawati huku ya timu ya Liverpool ikiwa nyekundu. Ulinganisho wa tafsiri za istilahi hizi na matumizi yake unaonyesha kuwa tafsiri sisisi huweza kupotosha ujumbe uliodhamiriwa hasa kwa wale wasio mashabiki wa mchezo huu. Hii ina maana kuwa tafsiri sisisi hukubalika na kukamilisha ujumbe miongoni mwa wahusika.

Habwe na wengine (2010) wanaeleza kuwa lugha ya matangazo huwa sahili na isiyo na utata wa ufasiri na kwamba lugha ya matangazo ya kandanda huchukua sura ya mazungumzo ya moja kwa moja kati ya msikilizaji na mtangazaji, kama kwamba anakabiliana ana kwa ana na hadhira yake. Wanaeleza kuwa lugha hii huibua taswira, chuku na taharuki. Aidha, wanaangalia baadhi ya mbinu za mawasiliano zilizochambuliwa kutumika katika sajili ya mchezo wa kandanda sawa na sifa bainifu za sajili hii. Wanataja uchanganyaji msimbo, misimu, kauli ndefu za kimaelezo, kukatizwa kwa usemi, kurejelea wachezaji kwa majina na matumizi ya vihisishi kama sifa bainifu za sajili hii.

### 2.6 Hitimisho

Sura hii imechanganua matini ili kubainisha mbinu zinazotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda kuwasiliana na kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji wao.

Kwa sababu watangazaji wa mchezo wa kandanda hutumia lugha ya uneni, wanahusisha mbinu za kiisimu. Miongoni mwa mbinu zilizobainika kutumiwa ni utohozi, uchanganyaji msimbo, ubadilishaji msimbo, maswali ya balagha, tafsiri sisisi na tamathali za usemi kama vile urudiaji, tashbihi, tashihisi, misemo, misimu na methali.

Uambatishaji kiungo, uchopekaji wa maneno ya kigeni kati ya sentensi na uchopekaji wa maneno ya kigeni mwishoni mwa sentensi ni aina za uchanganyaji msimbo zilizobainika. Katika utangazaji wa mchezo wa kandanda, uchanganyaji msimbo na ubadilishaji msimbo umeonyesha dhima ya kurejelea, kufafanua, kusisitiza, kupendeza na kujitambulisha na kuonyesha hisia.

Imebainika kuwa lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda hutumia misemo na misimu kama mbinu ya kuwachangamsha wasikilizaji na kujitambulisha na mashabiki. Misimu inayotumiwa na watangazaji hutambuliwa na kueleweka kwa wasikilizaji bila utata wowote. Hali kadhalika, tafsiri sisisi inayohusishwa na watangazaji haitatizi mawasiliano kati yao na wasikilizaji kwa sababu wanaelewa muktadha wa matumizi yake. Aina za takriri zilizobainika ni takriri-vitenzi na takriri-nomino. Mbali na msisitizo, takriri kutumiwa kuonyesha mfululizo wa mchezo wa kandanda. Matumizi ya mbinu hizi kwa uchangamano hufaulisha mawasiliano kati ya watangazaji wa mchezo wa kandanda na wasikilizaji wao.

Katika sura inayofuata tumechanganua aina za maana zinazojitokeza katika matini za utangazaji wa mchezo wa kandanda. Kulingana na nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo, lugha huwa na maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi. Tumeonyesha jinsi mihimili hii ya nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo inavyohusiana kudhihirisha upataji wa ujumbe na uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda.

# SURA YA TATU

# MAANA KATIKA MATINI

## 3.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeangazia mbinu za mawasiliano zinazotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji wao. Katika sura hii tumechanganua na kubainisha aina tofauti za maana zinazotokana na matumizi ya lugha katika sajili ya mchezo wa kandanda. Halliday (1985) ametambua aina tatu za maana: Maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi. Aina hizi tatu za maana hujitokeza kama mihimili ya nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo (SAM) inayoongoza utafiti huu. Nadharia hii inashikilia kuwa kama tukio la kijamii, lugha iliundwa kwa minajili ya mawasiliano. Nadharia hii inaangalia lugha sawa na mtandao wa maana unaowakilishwa kwa maumbo ya kisarufi.

Kwa kuwa maana tagusani huamilisha na kuyakinisha maana dhanishi, aina hizi za maana hujitokeza kama amali za kimsingi ambazo utoshelevu wa dhima zake hutegemea amali ya maana matinishi. Hivi ni kusema kuwa aina hizi za maana huingiliana na kukamilishana katika kufanikisha mawasiliano.

## 3.1 Maana Dhanishi

Kama tulivyoonyesha katika uk.18, Yule (1996) anaeleza maana dhanishi kama jumla ya sifa muhimu za kimsingi zinazohusiana na matumizi halisi ya neno. Maana hii inaangaliwa sawa na uamilifu wa lugha kutokana na kusimba tajriba za kibinafsi za msemaji na zile za kitamaduni katika jamii anamoishi. Kwa hivyo,

maana dhanishi humwezesha mtumiaji wa lugha kuujua ulimwengu wake na kuutumia ujuzi huo kueleza tajriba zake. Kwa kuwa maana dhanishi hujitokeza kama maana tambuzi au asili inayobainisha utendakazi wa lugha, inaaendeleza utanzu wa semantiki.

Lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda huelekea kufananisha mambo na vitendo vinavyotokea katika mazingira ya watangazaji na wasikilizaji na namna mchezo huu unavyochezwa na kusimamiwa. Lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda hutumia vipashio vya lugha kwa namna inayohamisha na kugeuza maana yake. Hivi ni kusema kuwa vipashio vya lugha hupewa maana na matumizi mapya yaliyo nje ya muktadha wake wa kawaida. Hii ina maana kwamba muktadha wa matumizi ya vipashio hivi hupanuliwa.

Inajitokeza kuwa huenda matumizi haya yatatize na yasieleweke kwa wale wasiohusika na mchezo huu. Kwa hiyo, lugha inatumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kwa njia inayosuka maana dhanishi kuwa msingi wa kuibua vivuli vingine vya maana kulingana na matumizi yake. Kulingana na data yetu, baadhi ya vipashio vya lugha vinavyohusishwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda katika uwasilishaji wa maana dhanishi ni vitenzi, nomino na vivumishi.

### 3.1.1 Matumizi ya Vitenzi

Vitenzi ni mojawapo ya vipashio vya lugha vinavyotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kuibua maana dhanishi katika mazingira ya kipekee. Jedwali lifuatalo

linaonyesha matumizi ya vitenzi kwa namna inayohusisha mchezo wa kandanda na hali ya vita au makabiliano.

**Jedwali 3.1 Matumizi ya Vitenzi Vinavyohusisha Mchezo wa Kandanda na Makabiliano**

| Kitenzi | Matini |
|---|---|
| Pepeta; Menya | Popote ulipo msikilizaji karibu kwenye mechi hii ya kukata na shoka. Mara ya mwisho timu hizi mahasimu *zilipomenyana* AFC *ilipepeta* Gor mabao matatu kwa moja. |
| Tamba; Adhidu | Katika dakika ya themanini na mbili msikilizaji, mafuriko yanaendelea kuonekana, Salah anafunga bao la sita, timu ya nyumbani Chelsea inaendelea *kutamba* leo, *inaiadhibu* hapa Arsenal mabao sita mtungi. |
| Tandika | Naona dakika zinaendelea kuyoyoma hapa, na wakati wowote refarii ataweza kumaliza mchezo. Sofapaka wanawaste time pale kwa sababu wako kifua mbele, na wakati huo huo mpira umekwisha. Sofapaka *imeitandika* Tusker mabao manne kwa mawili. |
| Kaanga | Mchezo unamalizika msikilizaji, mabingwa watetezi Gor Mahia *wanakaangwa* hapa na limbukeni hawa. Nakuru Top Fry moja, Gor bila. |
| Chapa; Lipua; Zika | Katika Manchester derby second leg, Ciy *inaichapa* United mabao matatu bila jibu baada ya *kuilipua* mabao manne kwa moja katika mkondo wa kwanza. Tangu Moyes kuchukua ukufunzi wa Manchester United, imekuwa maiti wa *kuzikwa* na timu yoyote. |
| Charaza; Rarua | Mechi inaanza hapa Anfield. Kumbuka kwamba timu hizi mbili zimetengwa na alama tano tu, Liverpool *ikicharaza* Chelsea watabeba, vijana hawa wa Mourihno *wakirarua* Liverpool watakuwa na nafasi. |

Kwa mujibu wa TUKI (2013), kitenzi *adhibu* kina maana ya tesa au sumbua huku *tandika* kikiwa na maana ya piga au chapa. *Pepeta* ni kitenzi chenye maana ya rusharusha nafaka katika ungo ili kuondoa makapi na takataka. *Charaza* ni kitenzi chenye maana ya piga ngoma au kinanda kwa mfululizo. Kitenzi *rarua* kinamaanisha pasua kitu kama vile karatasi au nguo vipande vipande kwa kuvuta bila utaratibu maalum na kitenzi *lipua* kina maana ya kufanya kitu kifumke au kipasuke kwa nguvu kwa sababu ya moto. Hali kadhalika, kitenzi *zika* kina maana ya fukia kitu, mzoga au maiti ndani ya shimo au kaburi, kitenzi *chapa* kinamaanisha kupiga kwa kutia adabu au kuumiza, kitenzi *zaba* nacho kikimaanisha kupiga kwa kofi huku *kaanga* kikiwa na maana ya choma au pika chakula kwa mafuta. Vitenzi hivi vinatumika katika lugha ya utangazaji wa kandanda kumaanisha kuwa timu fulani imecheza vizuri na kupata ushindi mkubwa dhidi ya timu nyingine.

Katika jedwali la 3.1 matini 'Chelsea imeweza *kuiadhibu* Arsenal mabao sita mtungi' inamaanisha kuwa timu ya Chelsea imepata ushindi wa mabao sita kwa nunge dhidi ya Arsenal. Aidha, katika matini 'Sofapaka *imeitandika* Tusker mabao manne kwa mawili' inamaanisha kuwa timu ya Sofapaka imeifunga ile ya Tusker mabao manne kwa mawili. Katika matini 'Mara ya mwisho timu hizi mahasimu zilipokutana AFC Leopards *iliipepeta* Gor Mahia magoli mawili kwa moja' imetumiwa kwa maana kuwa timu ya AFC Leopards iliishinda Gor Mahia katika mchezo huo.

Matini 'Mabingwa watetezi Gor *wanakaangwa* hapa na limbukeni hawa. Nakuru Top Fry moja, Gor bila' nayo imetumiwa kwa maana kwamba timu ya Nakuru Top

Fry imeishinda ile ya Gor Mahia kwa kuifunga bao moja kwa bila. Hali kadhalika, matini 'Katika Manchester derby second leg, City *inaichapa* United mabao matatu bila jibu baada ya *kuilipua* mabao manne kwa moja katika mkondo wa kwanza' inamaanisha kuwa klabu ya Manchester City iliishinda ile ya Manchester United mabao manne kwa moja katika mkondo wa kwanza kabla ya kuishinda mabao matatu kwa nunge katika mkondo wa pili.

Kulingana na data yetu, watangazaji wa mchezo wa kandanda pia hutumia vitenzi kama *uma, bwaga, nyakua, laza, zima, nyamazisha, nyanyasa, kung'uta, chinja, ua, kwaruza, garagaza, menya, ng'ang'ania, pokonya, lima, twanga, bwaga, bambanya, fyeka, komoa, ramba, tesa, kandamiza, nyoa, umiza, tahiri, najisi, tesa, nyuka, pora, vamia, vizia, kamua, tamba, vaa, pagawa, roga, tawala, twaa, sakama, dhulumu, angusha, nyonga, banja, chambua, zamisha* na *adilisha* kwa njia hii kumaanisha kuwa wachezaji wa timu fulani walijizatiti kumiliki na kudhibiti mchezo na hatimaye kufaulu kupata ushindi dhidi ya timu nyingine kama ilivyoonyeshwa katika Kiambatisho 2.

Mbali na kuhamisha matumizi ya vitenzi moja kwa moja kwa namna inayohusisha mchezo wa kandanda na vita au makabiliano, kuna vitenzi vingine vinavyopewa matumizi ya kitamathali kama inavyobainika katika Jedwali hili.

**Jedwali 3.2 Matumizi ya Vitenzi Kitamathali**

| Kitenzi | Matini |
|---|---|
| Iva;<br>Chanua | Anachenga moja Suarez, anachenga mbili, tatu, anapiga pale go-ooo-ol! Hakika mshambulizi huyu ambaye amekuwa *akichanua* hivi karibuni sasa *ameiva* kweli kweli. Si ajabu amevunja rekodi ya ufungaji mabao Liverpool. |
| Noa;<br>Nasa;<br>Nyemelea | Naona anatoka Ramsey anaigia Ozil. Kiungo huyu amesaidia sana *kunoa* timu hii ya Arsenal. Msikilizaji kabla ya *kunaswa* na The Gunners, nyota huyu Mjerumani ambaye amekuwa nguzo ya safu ya katikati *alinyemelewa* na timu maarufu kama vile Chelsea na Manchester United. |
| Fua | Wachezaji wa timu zote mbili wanarudi uwanjani baada ya *kijifua* kutokana na mawaidha ya makocha wao. |
| Tua;<br>Winda; | Mpenzi msikilizaji tangu mshambulizi huyu van Persie *kutua* Man United baada ya *kuwindwa* na timu hii kwa misimu miwili iliyopita, kweli amekuwa akiwapagawa waajiri wake hawa wa zamani. Leo amerudi hapa kuwaroga tena Arsenal, anafunga bao maridadi la kusawazisha. Huyu ni mchawi kweli. |
| Nunua;<br>Uza;<br>Rutubisha | Msikilizaji huyu Mata, kiungo matata kutoka Hispania *aliyenunuliwa* na Man United kutoka Chelsea kwa dili ya kitita cha pauni milioni ishirini na saba, aliingia *kurutubisha* midfield na baada ya dakika tano tu uwanjani, alipachika bao la tatu kimyani na sasa anaongeza la nne dhidi ya Norwich City. Si ajabu Chelsea *ilimuuza* shingo upande. |
| Mega;<br>Vurumisha;<br>Jibu | Wanakwenda Man United, Kagawa *anammegea* Evra, *anavurumisha* pale kombora go- goo-oo-l! United moja, wenyeji Bayern sufuri. Wanaanza pale katikati Bayern, wanakwenda mbele, hatari pale, anatoa cross rojorojo anatia kichwa goo-go-ooo-l! Amini usiamini msikilizaji, Bayern *wanajibu* hapa dakika moja tu baada ya Man United kufunga. |
| Wika; | Anatuliza mpira Suarez kwenye gamba la kifua, anachenga moja, |

| | |
|---|---|
| Chumbia | anachenga tena, anatoa pasi ya back heel kwake nani yule-ee Sturridge. Anachukua tena, anapenya pale go-go-goo-oool! Anafunga hapa bao lake la thelathini msimu huu na kuvunja rekodi ya ufungaji mabao Liverpool. Mchezaji huyu *anawika* kweli, amekuwa moto wa kuotea mbali, huyu ni mtambo wa kufunga mabao na si ajabu *alichumbiwa* sana na timu kadha kama Arsenal na Real Madrid katika dirisha la uhamisho wa msimu uliopita. |

Kulingana na TUKI (2013), *iva* ni kitenzi kilicho na maana ya kuwa mbivu au pevuka kama vile tunda. Pia kinamaanisha pikika kwa chakula na kuwa tayari kwa ajili ya kuliwa. Kitenzi *chanua* kina maana ya kufumuka kwa maua kwa namna inayovutia macho huku *wika* kikimaanisha kutoa sauti inayoweza kufika mbali kama jimbi. Vitenzi hivi vinatumika katika sajili ya mchezo wa kandanda kwa maana ya wachezaji fulani kusifika kwa kuwa katika hali ya kuonyesha mchezo mzuri na kuwafurahisha mashabiki kuliko wengine. Kulingana na matini, mchezaji 'aliyeiva', 'kuchanua' na 'kuwika' ni Suarez. Mchezaji mzuri anafananishwa hapa na tunda bivu, chakula kilichopikwa au maua yanayovutia macho.

Kitenzi *nyemelea* kinafafanuliwa na TUKI (2013) kama kuendea kitu kimyakimya na polepole kama wafanyavyo wawindaji. *Kuwinda* ni kwenda msituni kwa mwindaji ili kutafuta wanyama kwa kitoweo. *Kuchumbia* ni kupeleka maombi kwa wazazi wa binti kutaka kumwoa. Katika sajili ya mchezo wa kandanda, vitenzi hivi vinarejelea jitihada na mipango ya wakufunzi au usimamizi wa klabu fulani kupata huduma za mchezaji fulani kwa kumsajili na kuwa miongoni mwa wachezaji wake. Matini "...tangu mshambulizi huyu van Persie kutua Man United baada ya *kuwindwa* na timu hii kwa misimu miwili iliyopita...", "...huyu ni mtambo wa

kufunga mabao na si ajabu *alichumbiwa* sana na timu kadha kama Arsenal na Real Madrid..." na "...nyota huyu Mjerumani ambaye amekuwa nguzo ya safu ya katikati *alinyemelewa* na timu maarufu kama vile Chelsea na Manchester United." zinamaanisha kuwa wasimamizi wa timu zilizohusika walifanya juhudi za kupata huduma za wachezaji waliotajwa.

*Nasa* ni kitenzi chenye maana ya kushika kama mtego au kufaulu kushika kitu kilichotegwa kama vile wanyama msituni. Kitenzi hiki kinatumiwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kurejelea kufaulu kwa mkufunzi au usimamizi wa klabu fulani kumsajili mchezaji katika klabu hiyo. Matini "Msikilizaji kabla ya *kunaswa* na The Gunners..." inarejelea wakati ambapo mchezaji Ozil alikuwa hajasajiliwa na The Gunners.

Mchezaji anapojiunga na klabu husika ili kuchangia kuimarika kwake, inasemekana kuwa *ametua* katika klabu hiyo ili *kuirutubisha,* kama walivyofanya van Persie na Mata mtawalia katika klabu ya Manchester United kulingana na matini. Hali kadhalika, kitenzi *noa* kilicho na maana ya kutia silaha makali na *fua* chenye maana ya kutengeneza kitu kutokana na madini vinatumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kurejelea juhudi za wachezaji wa timu fulani kuboresha kiwango au hali ya mchezo wao kupitia mazoezi. Matini "Kiungo huyu amesaidia sana kunoa timu hii ya Arsenal" inamaanisha kuwa mchezaji Ozil amechangia kuboresha kiwango cha timu ya Arsenal. Maelezo haya yanaonyesha kwamba mchezo wa kandanda unalinganishwa pia na shughuli za uwindaji, unyumba au posa.

*Nunua* ni kitenzi kinachomaanisha kutoa fedha ili kupata kitu kinachouzwa. Kitenzi hiki hutumiwa kurejelea idhini ya kupata huduma za mchezaji mpya baada ya kulipa kiasi fulani cha fedha kwa usimamizi wa klabu aliyokuwa. *Uza* ni kitenzi kinachomaanisha kubadilisha kitu kwa fedha au kitu kingine. Kinatumika katika sajili ya mchezo wa kandanda kumaanisha kuruhusu mchezaji kujiunga na klabu nyingine baada ya ada fulani kulipwa. Matumizi ya vitenzi hivi husawiri wachezaji wa kandanda kama bidhaa au huduma zinazoweza kufanyiwa biashara sokoni.

*Mega* humaanisha vunja au kata kipande cha kitu katika sehemu ndogo ndogo. Kitenzi hiki kinapata matumizi ya mchezaji mmoja kumchezea mwenzake pasi nzuri au kupigia mwenzake mpira unaomfikia kama ambavyo mchezaji Kagawa alivyomfanyia mwenzake Evra katika matini. Kitenzi *vurumisha* kinachomaanisha tupa kitu kama vile jiwe au gongo kwa nguvu kinatumiwa na watangazaji wa sajili ya mchezo wa kandanda kurejelea kupiga mpira kwa nguvu nyingi ili ufike mbali na lango la yule aliyeupiga au kuelekea lango la timu pinzani ili ufunge kama alivyofanya mchezaji Evra dhidi ya timu ya Bayern Munich katika matini.

Kitenzi *jibu* chenye maana ya itikia kwa maneno, maandishi au ishara kinatumika katika sajili ya mchezo wa kandanda kurejelea hali ya timu fulani kufunga bao la kusawazisha. Matumizi ya kitenzi hiki yanaonyesha kuwa hali ya timu kufungwa bao kwanza ni sawa na 'kuulizwa swali' ambalo 'linajibiwa' na timu husika inapofunga bao la kusawazisha kama ilivyofanya timu ya Bayern katika matini.

Uchanganuzi huu unabainisha kwamba vitenzi hivi havitumiwi kwa maana ya moja kwa moja iliyozoeleka. Hivi ni kusema kwamba vitenzi hivi vimepewa matumizi ya kitamathali au kimafumbo ili kueleweka na wasikilizaji wa matangazo ya mchezo wa kandanda. Imebainika kuwa maana dhanishi imesukwa hapa kama msingi wa kuibua maana kama matumizi katika mazingira haya mahsusi. Ni kwa jinsi hii ambavyo uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda hubainika.

Aidha, vitenzi kama vile *tema, tuma, alika, achilia, nyata, poteza, mega, fua, ng'aa, tongoza, tisha, otea, uza, komboa,* na *lisha* navyo vinatumiwa kwa namna ya kipekee na kupewa maana maaalum katika sajili ya mchezo wa kandanda (Tazama Kiambatisho 2).

### 3.1.2 Matumizi ya Nomino

Mbali na vitenzi, nomino ni kipashio kingine cha lugha kinachotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kwa njia inayopanua maana yake tambuzi au ya kimsingi. Hali hii imebainishwa katika Jedwali lifuatalo.

**Jedwali 3.3 Matumizi ya Nomino**

| **Nomino** | **Matini** |
|---|---|
| Bomu; Mshambulizi | Anapiga pale kimo cha nyoka goo-oo bado goo-oool! *Mshambulizi* huyu Rooney ameangusha *bomu* zito lililomlipua kipa. |
| Silaha; Mapambano; Adui | Bosi wa klabu ya Gor, Boby Williamson alinukuliwa akisema amenoa *silaha* zake kwa *mapambano* dhidi ya *adui* zao AFC Leopards. Leo ni leo, wakati huu ulisubiriwa kwa hamu na ghamu. |

| | |
|---|---|
| Adhabu; Mahasimu | Naona mkufunzi wa timu ya Chelsea analalamika dhidi ya *adhabu* hiyo ya penalti ambayo *mahasimu* wao Sunderland wamefunga. |
| Vigogo; Makali; Mashambulizi | *Vigogo* hawa Liverpool wanapigiwa upatu wa kutwaa taji la ligi ya Uingereza mwaka huu baada ya kuonyesha *makali* katika safu ya *mashambulizi.* |
| Kombora; Mkwaju; | Anakwenda, Hazard, anachenga moja, anachenga mbili, tatu anatuma *kombora* zito pale-ee *mkwaju* ule unajaajaa kimyani! Naona mashabiki wa Chelsea wanashangilia bao hilo. |
| Patashika; Kizaazaa | Wanang'ang'ania mpira pale, mshambulizi anakataa katakata kupokonywa mpira, *kizaazaa* kwenye lango, kivumbi kinatifuka, *patashika* nguo kuchanika. |
| Miamba; Ubabe; Mapinduzi | Karibu tena katika kipindi cha pili msikilizaji, mambo hapa ni mawil kwa mawili. Kumbuka kwamba *miamba* hawa wa soka AFC na Gor wanapokutana huwa ni derby hapa Nairobi, kila timu ikijaribu kufanya *mapinduzi* na kuonyesha *ubabe* wake. |

TUKI (2013) inatoa ufafanuzi wa *bomu* kama silaha inayotengenezwa kwa vitu vinavyolipuka na ambavyo husababisha madhara makubwa. *Mkwaju* ni fimbo ya kuchapia. *Kombora* ni bomu linalofyatuliwa na mzinga huku *mashambulizi* yakiwa ni matendo ya kuvamia au kuhujumu. Nomino hizi hutumiwa katika lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda kwa maana ya mpira uliopigwa kwa nguvu nyingi na unaokwenda kwa kasi ya kutoweza kuuzuia. Matini "Mshambulizi huyu Rooney ameangusha *bomu* zito lililomlipua kipa" na "... Hazard anachenga moja, ...anatuma *kombora* zito pale-ee, mkwaju ule inajaajaa kimyani!" zinamaanisha kuwa wachezaji Rooney na Hazard walipiga mpira kwa nguvu nyingi na kufunga. Nomino nyingine kama *risasi, jiwe, mzinga,* na *chuma* hutumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kwa maana hii (Tazama Kiambatisho 3).

*Silaha* inaelezwa kama kitu kinachotumika kupigania na ambacho kinaweza kujeruhi au kuua. Wachezji wazuri huangaliwa sawa na silaha. Katika matini, wachezaji wa klabu ya Gor Mahia ndio wanaorejelewa kama silaha. Nomino *bunduki* pia hutumiwa badala ya silaha kumaanisha wachezaji wazuri sana wasioweza kudhibitiwa hasa wa safu ya mbele na walio na uwezo wa kufunga mabao mengi. Hali kadhalika, nomino *kifaa, mshambulizi, moto, dawa, kipenzi, nyuki, nyota* na *mchawi* aghalabu hutumiwa kurejelea wachezaji wazuri sana na walio na uzoefu katika safu ya ufungaji. Nomino kama vile *injini, mtambo, nguzo, ukuta* na *ngome* ni baadhi ya zile zinazotumiwa pia kurejelea wachezaji wazuri na wa kutegemewa katika safu ya nyuma au katikati.

*Mapinduzi* ni nomino yenye maana ya uondoaji madarakani viongozi wa serikali hususan kwa kutumia nguvu. Nomino hii inapewa matumizi ya hali ya timu fulani ambayo ilishafungwa kusawazisha bao hilo na kufunga tena mabao mengine ya kuipa ushindi mkubwa. Nomino *kikosi* yenye maana ya kundi la majeshi inatumiwa kurejelea jumla ya wachezaji wa klabu yoyote ile. Hii ni kwa sababu kama kikosi hufanya kwa jeshi, wachezaji hawa huwa tayari kuingia uwanjani na kuichezea timu zao ili kuzipa ushindi (Tazama Kiambatisho 3). Uchanganuzi huu umebainisha kuwa mbali na ugomvi, maangamizi na vita vya silaha kali na hatari, sajili ya mchezo wa kandanda pia inapewa picha ya mfumo wa kuzalisha na ushirikina.

Nomino *mwamba* humaanisha jiwe au jabali kubwa. Katika sajili ya mchezo wa kandanda, nomino hii imepewa maana ya klabu nzuri au wachezaji mahiri wenye ujasiri na waliosifika kwa kutwaa mataji mengi ya mchezo. Nomino zaidi zinazotumiwa kwa maana hii ni kama vile *vigogo, wafalme, majogoo* na *mibabe.* Katika matumizi haya, klabu zenye uthabiti na wachezaji wakakamavu wanaangaliwa sawa na watu wenye mamlaka makubwa.

*Adui* au *hasimu* ni mtu anayemtendea mwenzake vibaya. Wachezaji wa timu moja huwaona wenzao wa timu nyingine kama maadui zao wanaopangiwa njama za kuwaangamiza kwa kushindwa katika mchezo. Kulingana na matini, wachezaji wa timu ya Gor Mahia wameelezwa kama maadui wa wachezaji wa AFC Leopards huku wachezaji wa Chelsea wakionekana kama mahasimu wa wachezaji wa Sunderland.

*Patashika* ni nomino yenye maana ya hali ya kugombea kitu kwa nguvu na vishindo (TUKI 2003). Aidha, *kizaazaa* inamaanisha hali ya fujo ambapo watu hawasikilizani. Nomino hizi zinarejelea hali ya wachezaji walio uwanjani kufanya kila jitihada ili kupata mpira au kumiliki mchezo. *Pambano* ni shindano la maneno au vitendo. Nomino hii inatumiwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kurejelea mchezo uliopangwa kuendelea. Kulingana na matini, mchezo uliopangwa kuendelea kati ya klabu ya Gor Mahia na AFC Leopards unaangaliwa sawa na mapambano. Nomino nyingine zilizopewa matumizi haya ni kama vile *mchuano, kindumbwendumbwe, kipute, kivumbi, kinyang'anyiro* na *dimba.* Hali kadhalika,

nomino kama vile *ngozi, kinda, mafuriko, mtungi, manowari, hatari, mlinzi, mauzo, ukame, zawadi, maembe, mteja, maiti* na *tasa* zinatumiwa kwa maana maalum na teule katika lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda (Tazama Kiambatisho 3).

Matumizi ya vitenzi na nomino katika matini za utangazaji wa mchezo wa kandanda yamesawiri mchezo huu kwa kiasi kikubwa kama uhasama, ugomvi na vita ambavyo kilele chake ni ushindi wa sehemu au timu mojawapo. Japo mchezo wa kandanda unadhamiriwa kuchangamsha na kuburudisha watazamaji na wasikilizaji, unaonekana kuzua hisia kali kutoka timu pinzani katika hali halisi. Si ajabu wakati mwingine panashuhudiwa hasira, vita, majeruhi, na hata vifo vya wachezaji na mashabiki wa timu zinazoshindana. Uchangamfu na burudani inayotazamiwa hupatikana tu iwapo timu inayoshabikiwa na mrengo fulani inapata ushindi, hali ambayo bado huzua hasira na huzuni kwa mrengo unaoshindwa.

### 3.1.3 Matumizi ya Vivumishi

Kipashio kingine cha lugha kinachotumiwa kuibua maana katika sajili ya mchezo wa kandanda ni kivumishi. Matumizi yake yamebainishwa katika Jedwali hili.

**Jedwali 3.4 Matumizi ya Vivumishi**

| Kivumishi | Matini |
|---|---|
| Butu | Wanaingia pale Arsenal, Carzola kwake Wilshire, Wilshire anamtilia Giroud, anakwenda –aa nje! Anakosa nafasi ya tatu ya wazi huyu |

| | |
|---|---|
| | Giroud, amekuwa *butu* hapa. |
| Mkali | Msikilizaji, Odhiambo anaingia uwanjani and just in his second touch on the ball, anafunga! Kweli mshambulizi huyu ni *mkali* sana. |
| Mbivu; Mbichi | Msikilizaji wangu, wadadisi wengi wa kabumbu wanatabiri kuwa leo hii Jumapili ndio siku ambayo wafalme wapya wa EPL watajulikana hapa ugani Anfield. *Mbivu* na *mbichi* itajulikana kati ya wenyeji Liverpool na Chelsea. |
| Matata; Mtamu | Anacheza pale nani yule Silva wa Man City, anamegea Aguero-ooo Piga go-ooo! Mazingaombwe haya nini. Aguero, mshambulizi *matata* kutoka Argentina ni *mtamu* kweli, bila kupoteza muda anatuma kitu hadi kimyani. |
| Mbaya; Hatari | Anaingia pale Rama Salim, anachega, anachenga ya pili mchezaji huyu *hatari*, anamvisha kanzu yule hapa Opiyo, anakwenda la! Huyu hapa ni *mbaya,* anacheza kweli kweli. |
| Mrefu | Kipa anaweka ngoma ile chini, anarudi nyuma na kupiga mpira *mrefu* hadi duara la katikati. |
| Mwingi | Anafuata mpira ule, anajaribu kuuzuia lakini unakuwa *mwingi* na kutoka nje. |
| Mkubwa | Anapata pale pasi katikati ya uwanja, anakwenda nao Lampard wa Chelsea, anapiga mpira *mku-uu-bwa* unatoka nje. |
| Nzuri; Hafifu | Wanachukua ngoma ile Man City, wanasonga nao, wanaingia pale, Dzeko anamegewa pasi *nzuri* pale-eee lakini anapiga mpira *hafifu* sana. Kipa anayaka bila wasiwasi. |

TUKI (2013) inasema kuwa *butu* ni kivumishi kilicho na maana ya kitu kuwa katika hali isiyo kali. Kivumishi hiki kinatumiwa kurejelea timu au mchezaji anayepoteza nafasi nyingi za kufunga zilizo wazi. Katika matini "...Anakosa nafasi ya tatu ya wazi ya kufunga huyu Giroud, amekuwa *butu* hapa", maana inayojitokeza ni kuwa mchezaji Giroud si mchezaji makini katika ufungaji wa mabao. *–kali* ni kivumishi chenye maana ya kitu chenye ncha iliyochongeka inayoweza kuchoma au kinachoweza kukata kwa urahisi. Aidha, kina maana ya kitu chenye ladha

isiyopendeza kinywani. *–tamu* kinamaanisha ladha ya kuridhisha kinywani huku *–baya* kikitoa maana ya kitu cha kuchukiza, kudhuru au kuleta hasara. Vivumishi hivi vinapewa matumizi ya mchezaji bora ambaye mchezo wake unapendeza na anayetumia takriban nafasi zote anazopata kufunga bao.

Kivumishi *-refu* ina maana ya kitu chenye kimo au kipimo kikubwa kwa kusimama wima au kwa mlalo. *–kubwa* humaanisha kitu chenye kuzidi kwa umbo au kimo huku *-zuri* kikimaanisha -enye kupendeza au -isiyokuwa na hitilafu. *–ingi* nacho ni kivumishi chenye maana ya idadi kubwa au tele. Vivumishi hivi hutumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kurejelea hali ya kupiga mpira kwa nguvu na kufika mbali ambapo wachezaji hawawezi kufikia. *Hafifu* ni kivumishi chenye maana ya kitu chenye thamani ndogo au kitu kisichofaa. Kivumishi hiki hutumiwa kurejelea hali ya mchezaji kupiga mpira bila makini wala nguvu zinazohitajika kuuwezesha mpira huo kufunga.

Neno *hatari* ni nomino yenye maana ya hali ya kutokuwa na usalama, yaani hali ya kuleta maafa. *Matata* nayo ni nomino inayomaanisha hali ya ghasia, sokomoko na mvurugiko wa mambo. Maneno haya yametumiwa kama vivumishi vya nomino kumaanisha mchezaji hodari na aliye na uwezo wa kufunga mabao. Katika matini, mchezaji Odhiambo anarejelewa kuwa 'mkali', Aguero kuwa 'matata' na 'mtamu' na Rama Salim kuwa 'mbaya' na 'hatari' kwa sababu wao ni makini katika kucheza vizuri na kufunga mabao.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

*–bivu* ni kivumishi chenye maana ya pevu au lililioiva. Kinatumiwa katika lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda kurejelea timu iliyo na uwezo wa kupata matokeo ya ushindi kwa kuwa na wachezaji wazuri. Kivumishi *-bichi* kinachomaanisha isiyopikwa au kuiva vizuri kinatumiwa kurejelea timu dhaifu ambayo aghalabu hushindwa katika mechi zake.

Uchanganuzi wa matini hizi unaonyesha kuwa vivumishi *butu, -tamu, -bivu, -bichi, -refu, -kubwa, -zuri, -ingi* na *hafifu* vimepewa matumizi mateule huku *-kali, -baya, matata* na *hatari* vikitumiwa kwa maana ya kinyume. Hivi ni kusema kuwa maana ya vivumishi hivi hueleweka tu kwa wasikilizaji wa matangazo ya mchezo wa kandanda vinapotumiwa kwa njia hii kukamilisha maana.

Maelezo ya maana ya matini katika majedwali 3.1, 3.2, 3.3 na 3.4 yanaonesha kwamba wakati mwingine vipashio vya lugha vinaweza kutumiwa kwa njia au maana isiyo ya moja kwa moja. Vitenzi, nomino na vivumishi vilivyojitokeza katika matini vimepewa matumizi maalum, teule na ya kipekee. Hivi ni kusema kwamba vipashio hivi vimetumiwa kwa namna inayogeuza, kupanua na kuhamisha maana yake halisi ili kuafiki na kutosheleza mahitaji ya mawasiliano katika sajili ya mchezo wa kandanda. Hivyo basi, matumizi ya lugha kwa namna hii hufuma na kuyakinisha utanzu wa semantiki na wa pragmatiki. Hivi ni kusema kuwa matumizi haya ya lugha husuka maana dhanishi na maana tagusani.

Mawazo haya yanaoana na ya Halliday na wengine (1964) wanaosema kwamba lugha inakua na kupanuka kimatumizi kupitia tajriba na mahitaji ya jamii. Maoni haya pia yanaendeleza yale ya Brown na Yule (1983) wanaosema kuwa usemi unaweza kuchambuliwa kwa kutilia uzito maana inayoibuliwa. Hivi ni kusema kwamba watumizi wa lugha wakati mwingine humaanisha zaidi ya yale wayasemayo hasa wanapozingatia miktadha tofauti na kaida zinazodhibiti mahusiano na mawasiliano katika jamii. Kwa hiyo matumizi haya yanaendeleza maana tagusani. Wendell (1992) anasisitiza umuhimu wa kuchunguza lugha kulingana na muktadha wa matumizi yake. Anasema kwamba uamilifu wa lugha hukamilika ndani ya matumizi yake katika muktadha maalumu. Lyons (1968) anasema kuwa maana na uamilifu wa neno hutokana na matumizi yake. Anaeleza kuwa kujua neno ni kujua matumizi yake bali sio kutafuta maana yake. Anasema kwamba maana inayoibuliwa na neno au kauli hutokana na uwezo wake wa kutumika katika mawasiliano.

Norwich (1998) naye anadokeza kwamba neno au kauli hukubaliwa katika lugha kutokana na matumizi yake; kwamba kila neno, matini au sentensi humaanisha kazi inayotenda katika mazungumzo. Mtazamo huu huangalia lugha sawa na kifaa cha kutekeleza majukumu mbalimbali na kama chombo kinachobadilika kulingana na mahitaji ya watumizi wake. Kama kifaa kinavyotumiwa wakati mwingine kwa kazi isiyo yake ya kawaida, maana ya maneno au kauli huweza kubadilika kulingana na matumizi tofauti.

Butchavarov (1960) anaendeleza rai hii kwa kusema kwamba maana ya kauli yoyote ile inatokana na matumizi yake bali si kile kinachowakilishwa na kauli hiyo. Anaungwa mkono na Jefwa (2010) anayesema kuwa ili kung'amua matumizi ya maneno na kauli za lugha husika, ni lazima mtu afahamu vizuri mchezo wa lugha hiyo unaovipa vipashio maana. Massamba (1987) anaeleza kuwa uibuaji wa maana ya maneno na kauli isiyozoeleka huweza kutokana na mazoea ya matumizi yake kwa njia fulani na pia maendeleo au mabadiliko yanayotokea katika nyanja mbalimbali za maisha ambayo yanaweza kuleta mabadiliko ya kisemantiki ya vipashio vya lugha kama ilivyobainika katika matini zilizochambuliwa.

Hivi ni kusema kuwa maana dhanishi imejitokeza katika uchanganuzi huu wa matini za sajili ya mchezo wa kandanda kama msingi wa kuyakinisha ujumbe na kutosheleza mawasiliano na hivyo kuwa kivuli kinachofuma maana kama matumizi. Kwa jumla, maelezo haya yanalingana na nadharia ya SAM inayoshikilia kuwa lugha huwa na maana dhanishi pale watumiaji wake wanaposimba tajriba za ulimwengu wao katika kuzipambanua hali zinazowazunguka.

### 3.2 Maana Tagusani

Maana tagusani huangazia jinsi lugha inavyotumiwa kuleta utangamano miongoni mwa watumiaji wa lugha kwa uzingativu wa masharti na vikwazo vya kijamii. Hii ina maana kwamba mhimili huu wa nadharia ya SAM unaangalia lugha kuwa na uamilifu wa kuleta ushirikiano, mshikamano na utambulisho kupitia mazungumzo. Maana tagusani huwawezesha watumizi wa lugha kuakisi, kuimarisha na

kudumisha masharti ya mahusiano ya kijamii. Maana tagusani hubainika kama amali tekelezi ya lugha inayoangalia matumizi ya lugha sawa na tendo la usemi linalotekelezwa na msemaji ili kujieleza na kueleweka.

Yule (1996) anaeleza kuwa tendo la usemi hutokea pale ambapo utoaji wa usemi huzua kitendo, yaani, kusema ni sawa na kutenda. Austin (1962) anaeleza matendo ya usemi kama matamshi yenye uamilifu fulani katika mawasiliano. Anachomaanisha ni kuwa lugha hupata matumizi yake inapotumiwa kutimiza malengo fulani. Sifa mojawapo ya tendo la usemi anayoangazia Austin (1962) ni kuwa usemi hulenga mguso bayana katika kuarifu, kuonya, kuagiza, kushawishi, kurai, kuliwaza, kutumbuiza, kuahidi, kuudhi na hata kuuliza na kujibu maswali. Hivi ni kusema kuwa matendo yanatokana na ujumbe halisi unaodhamiriwa na msemaji.

Njogu na wengine (2006) wanaeleza kuwa maana ya usemi inapatikana pia katika jukumu lake la kujamiisha na kutagusanisha watu. Wanaeleza kuwa licha ya uwezo wa kuwasiliana kuhitaji sarufi na matamshi, unahusisha pia kaida za kijamii. Wanasisitiza umuhimu wa msemaji wa lugha kujua kuamkua, kutoa kauli, kusihi na kushukuru. Hali kadhalika, wasikilizaji wanapaswa kujua kama wanaulizwa swali, wanaruhusiwa kufanya jambo au kushutumiwa. Kwa njia hii, matendo ya usemi hudhihirisha sifa ya utegemezi wa muktadha katika matumizi ya lugha.

Ili kuamilisha maana tagusani, anayeshiriki katika usemi huongozwa na imani, mawazo na mielekeo ya wenzake. Kulingana na Halliday na Hasan (1976), kila mshiriki katika maongezi hunuia kuchangia kikamilifu na kuonyesha hisia zake huku akimsikiliza na kumhusisha mwenzake. Katika utangazaji wa mchezo wa kandanda, maana tagusani hubainika kupitia maagizo, maswali, rai na maelezo.

### 3.2.1 Maagizo/Amri

Lugha ya maagizo hutumiwa na watangazaji ili kujaribu kuwazia na kuelezea mazungumzo yanayoweza kutokea kati ya waamuzi na wachezaji uwanjani. Haya ni mazungumzo ambayo ni vigumu kwa mtangazaji kusikia kwa sababu ya kelele za mashabiki na umbali wa uwanja kutoka pale wanapotangazia. Kwa sababu watangazaji hunuia kuwaeleza wasikilizaji matukio yote yanayohusu mchezo, wanajikuta wakibuni maneno na kauli ambazo huenda zinatumiwa na waamuzi kwa wachezaji. Hii ni kwa sababu mashabiki wanaosikiliza matangazo redioni hutazama mchezo wa kandanda kupitia maneno ya mtangazaji. Mifano ya kauli za maagizo ni kama ifuatavyo.

1. ...anamchezea mwenzake pale visivyo na kumuumiza. Naona refarii akimwita: *"Njoo haraka!"* Mchezaji anasema "Ndio mkubwa". Anamuamuru: *"Geuka!"* Mchezaji anatii. Anaamuuliza: *"Nipe jina!"* Anamwambia jina. Naona refarii anamlisha nyekundu na kumwagiza: *"Toka nje!"* Mchezaji anasalimu amri.

2. ...anakwenda pale na mpira, anaingia katika eneo la hatari, anaangushwa na hiyo ni penalty. Naona pale refarii akitoa maagizo kwa wachezaji. Anawaambia: "*Tokeni ndani ya box!*" Sasa anamwambia mchezaji atakayepiga penalti. "*Subiri kipenga!*" Halafu anaongea na mlinda lango, ni kama anamwambia kuwa "*Usitoke kwenye lango kabla ya mpira kupigwa!*"

3. Wanafanya hapa mabadiliko timu ya Man City. Anatoka Navas na kuingia Milner. Anatembea taratibu, hana haraka, anajua wako mbele. Naona refarii anamwendea na kumwagiza: "*Toka nje upesi. Kimbia! Don't waste our time!*"

Kauli za amri katika matini hizi hudhihirisha hisia za hasira za mwamuzi na maelekezo yake kwa wachezaji uwanjani. Kupitia amri hizi washiriki katika tendo la usemi hugawana na kutimiza majukumu yao. Huku waamuzi wakitoa maagizo, wachezaji huwaridhisha kwa kutii na kutekeleza wanayoagizwa. Hali hii husaidia kujenga na kudumisha uhusiano kati yao.

### 3.2.2 Kurai

Lugha ya kurai hutumiwa na watangazaji kukisia mazungumzo yanayoweza kutokea kati ya mchezaji na mwamuzi, hasa mchezaji anapomwomba msamaha kwa kutofuata sheria za mchezo au kwa kumchezea mwenzake visivyo. Data ifuatayo inaonyesha hali hii.

1. Anamfuata pale mwenzake, anamfukuza katika duara la katikati, anamlaza. Refa anapuliza kipenga kuashiria foul. Anamwita mchezaji yule Shikokoti anayemwendea kwa unyenyekevu. Anambembeleza refa pale, anamwambia, "*tafadhali nisamehe mkubwa, sikumwangusha kimaksudi.*" Referii anamwambia kuwa asirudie tena. Haya, *foul* ile inapigwa...

2. Anakwenda, anakabiliana na mlinzi yule, anamchenga moja, mbili lakini anakataa, anamwangusha pale. Refarii anakimbia pale huku akiweka mkono mfukoni kutoa kadi. Naona mchezaji yule anamwinamia, ni kama anamwambia, "*tafadhali usinilishe kadi, sikudhamiria kumuumiza mkubwa.*"

3. Anaingia kwenye eneo la hatari, anasonga-aa, anaanguka chini. Ajabu hii, refarii anaandika kwenye kijitabu chake, ni kama anataka kumuonyesha kadi ya njano, ishara kuwa mchezaji huyu amejiangusha mwenyewe. Mchezaji anainuka kwa unyonge, anamwambia refa, "*mimi sijajiangusha, naomba usiniadhibu, mimi si mkosaji, nimeangushwa.*"

4. Anamegewa pasi safi Toure. Anafyatuka pale Aguero, anaingia kule-ee anachapwa kiatu anakubali kwenda chini. Anagaagaa kwa maumivu. Nahodha wa Chelsea John Terry anamshika mkono na kumnyanyua.

Msikilizaji, Aguero ananyanyuka kwa kuchechemea, Terry anamwambia, *"pole ndugu yangu, hii ni hali ya game."*

Kauli hizi za kurai zinadhihirisha hisia za huzuni na kujihukumu miongoni mwa wachezaji wanapoonekana kukiuka sheria za mchezo wa kandanda. Kwa kuomba msamaha, rai hizi huwawezesha wachezaji kujenga uhusiano kati yao na wasimamizi wa mchezo na wachezaji wenzao. Aidha, kurai huku kunadhihirisha hadhi na mamlaka ya refarii kama msimamizi anayeelekeza na kudhibiti mchezo huu.

### 3.2.3 Maswali

Lengo la kuuliza maswali ni kutafuta habari au kutaka ufafanuzi kuhusu jambo fulani. Maswali mengi yanayotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda aghalabu huchukua umbo la balagha. Maswali haya hutumiwa na watangazaji ili kudhihirisha hisia zao kuhusu matukio uwanjani. Yafuatayo ni baadhi ya maswali yanayotumiwa na watangazaji katika sajili ya mchezo wa kandanda.

1. ... anaingia katika kisanduku kile-ee lakini anacheza nje. Ilikuwa nafasi ya wazi na unajiuliza *ni kwa nini hakufunga bao hilo?*
2. ... wanamenyana pale, anamshika mwenzake shati na kumwangusha chini. *Jamani ni mchezo gani huu?*
3. ... anapata mpira na kusonga nao, anapiga mbele vibaya. Aaah! *Hii ni pasi ya aina gani wasikilizaji?*

4. ...anapata mpira peke yake lakini anakosa. Inashangaza wapenzi wasikilizaji. *Kwani lango lile kubwa mchezaji huyu hana macho?*
5. Ananyunyiza juu juu pale, *anamtilia nani yule-ee? Sasa anacheza wapi ule mpira?*
6. Salaale! *Ajabu gani hii?* He only had the net to beat lakini anajaza nje! La!

Maswali "Ni kwa nini hakufunga bao hilo?", "Kwani lango lile kubwa mchezaji huyu hana macho?" na "Ajabu gani hii?" yanaonyesha kutamauka kwa mtangazaji anayeona nafasi ya wazi ya kufunga bao zinapotezwa. Maswali "Jamani ni mchezo gani huu" na "Hii ni pasi ya aina gani?" nayo yanatumiwa na watangazaji kuonyesha kutoridhishwa kwao kutokana na mchezo mbaya.

Maswali mengine ni yale yanayokisiwa na watangazaji kuwa yanatokea kati ya wachezaji na waamuzi uwanjani au kati ya wachezaji wenyewe. Maswali haya huulizwa na wachezaji kwa waamuzi wanaotoa adhabu dhidi ya mchezo mbaya au usiozingatia sheria au kwa wachezaji wenzao wanaowachezea visivyo. Data ifuatayo inadhihirisha hali hii.

1. Anakwenda pale kwenye lango-oo, analazwa chini. Refarii anasema ni penalty! Naona mchezaji aliyeadhibiwa akimwendea refarii kwa hamaki na kumuuliza, *"Unasema ni nani amemwangusha? Kwa nini*

*unasema ni penalty na mimi sijamgusa? Huoni kuwa amejiangusha? Nani anastahili nyekundu?* I don't deserve that red card."

2. Anamegewa pasi nzuri mbele, anaingia pale-ee na kibendera kile kiko juu, ameotea. Mchezaji yule anamchemkia mbeba kibendera. Ni kana kwamba anamfokea. Anamuuliza, *"ni kwa nini unabeba kibendera na mimi sikuotea? Mbona unanionea?"*

3. Anachukua mpira katikati ya uwanja, anachenga moja, anakwenda, anachezewa visivyo na kuangushwa lakini refa anaashiria mchezo uendelee. Mchezaji yule anamfuata refarii, ni kama anamuuliza, *"ni kwa nini nachezewa vibaya na huoni?"*

4. Kipa anaanzisha mpira mrefu katikati ya uwanja-aa wanaruka pale kupiga kichwa na anaangushwa chini. Mchezaji anagaagaa chini kwa maumivu, anashika kichwa....Rooney anamwendea Kompany na kumkemea, *"mbona unanipiga mkumbo? Unataka kuniumiza?"*

5. ...anatiliwa pasi murua na kuingia maridadi. Anacheza kule-eee anaangushwa ndani ya box. Amini usiamini, refa anaashiria mchezo uendelee. Difenda yule anamwendea Wallcort na kumfokea, ni kama anamwambia, *"ni kwa nini unajiangusha? Unataka penalty au kilishwe nyekundu?"*

Maswali haya hujtokeza kama mwendelezo wa kauli mfululizo za utangazaji wa mchezo wa kandanda kwa sababu ya kasi ya mchezo huu. Maswali haya yanaonyesha hamaki na kutoridhika kwa wachezaji kutokana na maamuzi ya refarii yasiyowaridhisha. Maswali haya aghalabu huzua majibizano na mazungumzo baina ya wachezaji na wasimamizi na baina ya wachezaji wenyewe. Kwa kuulizana na kujibizana ifaavyo, lugha hutekeleza jukumu lake la kuleta makubaliano na maridhiano kwa kuwaunganisha wachezaji na waamuzi. Jambo hili linadhihirisha ukweli wa nadharia ya SAM kuwa lugha huwa na maana tagusani inapowawezesha washiriki katika mazungumzo kujieleza na kueleweka na wanaozungumza nao.

### 3.2.4 Maelezo

Lugha ya maelezo huwa na uamilifu husishi inapotumiwa na washiriki katika mazungumzo kujieleza ili kueleweka na kuwaridhisha wanaozungumza nao. Kwa njia hii basi, ujumbe husemekana kuwa umewafikia walengwa. Matukio ya mchezo wa kandanda kama yanavyofanyika uwanjani huwafikia wasikilizaji kupitia maelezo marefu na ya mfululizo yanayotolewa na watangazaji wa mchezo huo. Hii ni kwa sababu mchezo wa kandanda huendelea mfululizo kwa muda wote uliowekwa. Hivyo basi, inambidi mtangazaji kueleza au kusimulia yote yanayotendeka bila mpumuo.

Katika lugha ya matangazo, masikio ya msikilizaji ndiyo huwa kama macho anayotumia kuonea kila sehemu na matukio ya mchezo, huku maelezo ya

mtangazaji yakiwa kama picha za mchezo wenyewe. Mifano ya mfululizo wa maelezo iliyojitokeza katika data yetu ni kama ifuatavyo.

1. *Mpendwa msikilizaji popote ulipo tunakukaribisha katika dimba hili la leo. Hii ni mechi kali inayotazamiwa kuwa ngumu sana kwa sababu inahusu timu mbili hasimu tangu jadi na zinazotazamia kunyakua taji la ligi msimu huu. Mara ya mwisho timu hizi maadui zilipokutana ziliweza kufanya ukatili wa kuumiza nyasi bure kwa kutoka sare tasa, sijui leo mambo yatakuwa vile vile au vipi. Malango yote mawili ya timu hizi maarufu yalilalamika kwa sababu ya kulazwa njaa, haya tusubiri tuone kama leo yatapikiwa mabao na kulishwa.*

2. *Timu zote mbili, AFC na Gor zinajivunia ubingwa wa miaka ya nyuma na wachezaji wakali waliosifika sana katika ligi hii na kanda yote ya Afrika Mashariki na Kati. Naona zimejinoa hapa katika harakati zao za kuendeleza ubabe wao, na refarii mzuri atakayeamua dimba hili ni dakika tisini.*

3. *Mpendwa msikilizaji mechi inaanza pale katikati ya uwanja baada ya refa kupuliza kipenga chake ambacho daima huwa mdomoni mwake utadhani kimepakwa asali ya nyuki Anaregesha mpira ule Wanyonyi hadi kwenye safu ya ulinzi ili kupanga njama mpya ya kupenya ngome ya mahasimu wao ambao daima huwa thabiti kama chuma. Ulinzi wa*

*ngome hii unaongozwa na mchezaji huyu mzito kama nanga mwenye miraba minne na aliye na tajriba kubwa ya miaka na mikaka. Ni kama itawagharimu maadui zao majasho ya damu kupangua ngome hii thabiti.*

4. *Anachukua mpira ule vizuri kwenye duara lile la katikati na kufyatuka nao kama mshale kuelekea eneo la hatari. Anachenga moja, anachenga mbili, tatu, anavurumisha kombora nzito- oo go go-ooo-l! Mazito haya jamani. Mchezaji anaonyesha kuwa yeye si mchache, anamdhihirishia kocha wake kwamba alifanya busara kumpatia namba.*

5. *Wanang'angania mpira pale, wanamenyana, mshambulizi yule anakataa kupokonywa, kizaazaa kwenye lango lile, kivumbi kinatifuka, patashika nguo kuchanika, wachezaji kuanguka na goli kukosekana. La!*

6. *Ndugu msikilizaji, sikiliza penalti hii kwa makini, lisikupite hata neno. Naona sasa goal keeper na mshambulizi yule machachari wanakabiliana ana kwa ana. Anachanja pale-ee goo- oool. Anafunga hapa hat-trick mchezaji huyu na kusherehekea kwa kujipiga kifua. Anajigamba pale. Anajiambia kuwa mimi ndiye dume wa kufanya mambo.*

Mfululizo huu wa matumizi ya lugha huwawezesha watangazaji kujieleza na kueleweka na wasikilizaji wao. Mfululizo huu wa maelezo wakati mwingine huonekana kukariri ujumbe unaohusu matukio ya mchezo wenyewe kwa namna

inayojenga taswira na kutiwa chuku ili kuwafurahisha na kuwachangamsha wasikilizaji huku mtangazaji akijitambulisha nao. Kwa jinsi hii lugha huwa na uamilifu husishi wa kuwaunganisha na kuwatagusanisha wasikilizaji. Hivi ni kusema kuwa licha ya kuwafahamisha wasikilizaji kuhusu mchezo unavyoendelea, lugha ya maelezo hunuiwa kuwafurahisha na kuwachangamsha wasikilizaji ambao hujikuta wakijinasibisha na kujitambulisha na timu husika. Hapa, lugha huwa pia na uamilifu husishi wa kutumbuiza (Tazama Kiambatisho 4 kwa mifano zaidi).

### 3.3 Maana Matinishi

Kama mhimili mojawapo wa nadharia ya SAM, maana matinishi huhusika na kanuni za kisarufi zinazoelekeza matumizi ya lugha kwa lengo la kusarifu ujumbe na kufanikisha mawasiliano. Inazingatia usarifu na ukubalifu wa sentensi pamoja na mshikamano katika kauli ndefu. Aidha, inahusika na jinsi vipengele vya usemi vinavyounganishwa na vingine ili kuleta mshikamano katika matini. Hivi ni kusema kwamba maana matinishi hutekeleza jukumu la kuunda matini inayoeleweka kama ujumbe uliokamilika na wala si vipande vya maneno au vishazi vilivyotengwa.

Halliday na Hasan (1989) wanaeleza kuwa kuunganishwa huku kwa vipashio mbalimbali ili kujitokeza na matini kamilifu na amilifu ndiko kunakorejelewa kama mshikamano wa matini. Wanasema zaidi kuwa mbali na sintaksia, mshikamano wa matini ni dhana ya kisemantiki inayoelezea ufungamano na

uhusiano wa kimaana unaopatikana katika vipashio vya lugha vinavyojenga matini. Wanasema kwamba mshikamano hutokea ikiwa kufasiriwa kwa kipashio fulani katika usemi au matini kunategemea kipashio kingine kinachofuata au kutangulia.

Ufasiri huu huzingatia matumizi ya lugha kimuktadha pamoja na mshikamano na mazingira na kaida za mawasiliano. Hivi ni kusema kwamba maana matinishi humwezesha msemaji kupanga usemi wake kwa namna inayowasilisha ujumbe kulingana na muktadha. Lugha ya matangazo inayotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda inadhihirisha mshikamano wa matini kupitia ugeuzaji, uwakilishaji, udondoshaji na uunganishi.

### 3.3.1 Ugeuzi

Wakimnukuu Omondi (1994:104), Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa ugeuzi ni utaratibu wa sarufi ambao unapotekelezwa kwenye mfululizo wa ishara za kileksika katika mfumo fulani, unatoa athari fulani. Wanasema kuwa ugeuzi hutokana na Nadharia Geuzi iliyoasisiwa na Noam Chomsky katika kitabu chake *Syntactic Structures* (1957). Wanaendelea kusema kuwa ugeuzi unaweza kufanywa kwa kudondoshwa, kuchopekwa au kupanguliwa. Kupitia njia hizi, sifa kuu ya nadharia geuzi ambayo ni uwezo wa sheria chache kuzalisha sentensi nyingi zisizoweza kuhesabika katika lugha kutokana na umilisi wa mzawa wa lugha hubainika.

Lugha ya Kiswahili, kama zilivyo lugha nyingine za ulimwengu, ina namna ya kupanga vipashio vyake ili kuunda sentensi au matini zenye maana. Sintaksia inajitokeza kama mojawapo ya tanzu za kiisimu inayotambuliwa na nadharia ya SAM ili kuweka kanuni za upangaji wa vipashio vya lugha katika sentensi. Upangaji huu hufanywa kwa njia inayozingatia usarifu na ukubalifu wa sentensi pamoja na mshikamano katika kauli ndefu.

Sentensi za Kiswahili kwa kawaida huwa na mfuatano wa vipashio ambapo Kundi Nomino (KN) hutangulia Kundi Tenzi (KT). Katika utaratibu huu, Kundi Nomino huchukua uamilifu wa kiima huku Kundi Tenzi likichukua uamilifu wa kiarifu. Hata hivyo kutokana na sheria geuzi, mpangilio wa vipashio katika sentensi huweza kugeuzwa ili kuzalisha sentensi nyingine.

#### 3.3.1.1 Upanguaji

Hii ni aina ya ugeuzi ambapo panatokea ubadilishaji wa nafasi za elementi katika tungo. Hii inamaanisha kuwa elementi za tungo hukaa mahali ambapo si pake katika sentensi. Mifano ya upanguaji uliojitokeza katika data yetu ni ifuatayo.

1. *Jamani ni mchezo gani huu?* badala ya 'Huu ni mchezo gani jamani?'
2. *Sasa anacheza wapi ule mpira?* badala ya 'Anacheza mpira ule wapi sasa?'
3. *Upesi upesi anarudi nyuma difenda kuokoa ule mpira* badala ya 'Difenda anarudi nyuma upesi upesi kuokoa mpira ule.'

4. *Anatoa ile pasi Rooney kwake Valencia* badala ya 'Rooney anatoa pasi ile kwake Valencia.'
5. *Ile kona itachezwa kuelekea lango la Ulinzi* badala ya 'Kona ile itachezwa kuelekea lango la Ulinzi.'
6. *Anaingia pale kwenye eneo la hatari mchezaji Wanga* badala ya 'Mchezaji Wanga anaingia pale katika eneo la hatari.'
7. *...anakwenda na mpira mshambulizi huyu van Persie, anacheka na wavu msikilizaji* badala ya 'Msikilizaji mshambulizi huyu van Persie anakwenda na mpira, anacheka na wavu.'
8. *Anatuliza mpira Suarez kwenye gamba la kifua* badala ya 'Suarez anatuliza mpira kwenye gamba la kifua.'

Kutokana na upanguaji huu chagizo 'sasa' na 'upesi upesi' katika matini ya 2 na 3 zimetangulia kiarifa 'cheza' na 'rudi' mtawalia. Katika matini ya 3, chagizo 'upesi upesi' na kiarifa 'rudi' vimetangulia kiima 'difenda.' Hali hii inajitokeza pia katika matini ya 4 na 5 ambapo kivumishi 'ile' kinatangulia nomino 'pasi' na 'Rooney' huku kivumishi 'ile' kikitangulia nomino 'kona' mtawalia. Katika matini ya 6, kiima 'mchezaji Wanga' inatanguliwa na kiarifa 'anaingia pale'. Hali hii inajitokeza pia katika matini ya 7 ambapo kiima 'mshambulizi huyu van Persie' inatanguliwa na kiarifa 'anakwenda na mpira' na katika matini ya 8 ambapo kiarifa 'anatuliza mpira' kinatangulia kiima 'Suarez'. Licha ya kuonyesha uhalisia wa lugha ya maongezi ya kawaida ambapo wakati mwingine wazungumzaji hawawi makini kuzingatia kanuni za kisintaksia, upanguaji hubainisha uwezo wa

mtumizi wa lugha kuzua matini nyingi zenye kuwasilisha dhana sawia na hivyo kurahisisha mawasiliano.

#### 3.3.1.2 Uchopekaji

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza uchopekaji kuwa ni uingizaji wa elementi katika tungo hasa pale sentensi ya kauli ya kutenda inapogeuzwa katika kauli ya kutendwa. Uchanganuzi wa matini zifuatazo unaonyesha ugeuzi huu.

1. *Yule difenda anachengwa na mshambuliaji matata* badala ya 'Mshambuliaji matata anamchenga difenda yule.'
2. *Timu ya Thika United imefungwa mabao matatu kwa moja na timu ya Tusker* badala ya 'Timu ya Tusker imeifunga timu ya Thika United mabao matatu kwa moja.'
3. *Anatiliwa pasi nzuri pale Sserenkuma, anakwenda, anakwenda, anaingia ndani ya box, analazwa chini na Situma* badala ya 'Anatiliwa pasi nzuri pale Sserenkuma, anakwenda, anakwenda, anaingia ndani ya box na Situma anamlaza chini.'
4. *Mchezo unamalizika msikilizaji, mabingwa watetezi Gor wamekaangwa na limbukeni hawa Nakuru Top Fry* badala ya 'Mchezo unamalizika msikilizaji, limbukeni hawa Nakuru Top Fry wanawakaanga mabingwa watetezi Gor Mahia.'
5. *Mlinzi huyu aliyetemwa na Tusker amekuwa nguzo muhimu katika timu yake mpya ya AF Leopards* badala ya 'Mlinzi huyu amekuwa nguzo

muhimu katika timu yake mpya ya AFC Leopards baada ya Tusker kumtema.'

Katika mpangilio wa kawaida wa vipashio vya lugha katika sentensi ya Kiswahili, kitenda au kiwakilishi chake (KN1) hutangulia kitendwa (KN2). Matini hizi zinaonyesha kuwa nafasi ya KN1 na KN2 zinabadilika. KN2 linalobeba vitendwa 'Yule difenda', 'Timu ya Thika United' na 'Sserenkuma' vinatangulia KN1 linalosheheni vitenda 'Mshambulizi matata', 'Timu ya Tusker' na 'Situma' katika matini ya 1, 2 na 3 mtawalia. Ugeuzaji wa namna hii umedhihirisha mnyambuliko wa vitenzi 'chenga', 'funga' na 'lala 'kutoka kauli ya kutenda hadi kauli ya kutendwa. Hali hii ndiyo inayodhihirika pia katika matini ya 4 na 5 ambapo vitenzi 'kaanga' na 'tema' vinanyambuliwa katika kauli ya kutendwa mtawalia.

Hii ni kwa sababu ya uchopekaji wa mofimu {*w*} kama kiambishi kifuatilizi na kihusishi *na* kinachopekwa ili kutangulia KN2 na kuonyesha kuwa ndicho mtenda katika sentensi. Ugeuzaji huu wa vipashio katika sentensi unadhihirika kama njia mojawapo inayotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda kuunda matini zinazowasilisha ujumbe kwa njia rahisi na bora zaidi.

#### 3.3.1.3 Udondoshaji

Kwa mujibu wa Njogu na wengine (2006), udondoshaji ni uondoaji wa baadhi ya vipashio vya sentensi kwenye matini. Kwa sababu hii, kauli hazikamiliki. Hata hivyo, licha ya baadhi ya maneno au vipashio fulani kuachwa, ujumbe bado

humfikia mlengwa kwa sababu msemaji anachukulia kuwa licha ya kujieleza kwa maneno machache, msikilizaji wake anamwelewa kikamilifu.

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza udondoshaji kuwa ni ugeuzi unaohusisha kuondolewa kwa baadhi ya viambajengo vya sentensi. Hali hii hufanya sentensi kuwa fupi kuliko inavyopaswa kuwa. Wanaendelea kusema kuwa msemaji hudokeza maneno machache tu huku wakimaanisha zaidi ya kile wanachosema. Matini zifuatazo za udondoshaji zilijitokeza katika data yetu.

1. Anamegewa pasi ya mwaka pale na kutuliza. Anakwenda na mpira, anakwenda nao, (mpira), anakwenda (na mpira) anapiga (mpira unatoka) nje.
2. Wanaanza mpira Sofapaka, wanakwenda mbele, wanakwenda (mbele), hatari katika lango, hatari pale (katika lango), hatari... (katika lango).
3. Mechi inakaribia kuanza hapa Anfield. Kumbuka kwamba timu hizi mbili zinatengwa na alama tano tu. Liverpool wakiwacharaza Chelsea watabeba (kombe/taji), lakini vijana hawa wa Mourinho wakirarua Liverpool wana nafasi (ya kushindania taji).
4. Anachenga pale moja Suarez, (anachenga ya) pili, (anachenga ya) tatu, anaachilia (kombora) goo-oool!
5. Anatoa krosi nzuri kwenye lango (kuwatafuta wenzake) lakini wanachelewa (kufikia mpira huo).

6. Anakwenda na mpira, anapanda (kwenye wingi wa kushoto), anapiga mkwaju, la la la! (Anshindwa kufunga).
7. Anacheza pale-ee, kipa anaondoa (mpira ule nje ya uwanja).
8. Mlinzi anatoa mpira ule (kutoka eneo la hatari).
9. (Timu ya) AFC Leopards imetiwa mkononi na (timu ya) Sofapaka, imeshatandikwa hapa (goli) mbili (kwa) nunge.

Maneno yaliyo kwenye mabano ni yale yanayopaswa kutamkwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda katika mfululizo lakini hayatamkwi, yaani yanadondoshwa. Hata hivyo, watangazaji wa mpira wanachukulia kuwa wanaeleweka na wasikilizaji wao kwa maneno hayo machache. Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa msemaji hudokeza maneno machache tu huku wakimaanisha zaidi ya kile wanachosema. Udondoshaji huu hutokana na hali ya watangazaji kutotaka kurudia maneno yasiyo muhimu katika ufikishaji wa ujumbe, hasa baada ya kuyataja kwa mara ya mwanzo wanapotangaza. Hii ina maana kuwa udondoshaji huyafanya maongezi kuepuka matumizi ya maneno ambayo yanajulikana kwa msemaji/mtangazaji na msikilizaji/shabiki katika muktadha ambamo usemi unatumiwa. Matini hizi zinaonyesha kuwa maneno yaliyo katika mabano ambayo hayatamkwi yalikwishatamkwa awali au si lazima yatamkwe kwa kuwa ujumbe umekwishawafikia wasikilizaji.

Udondoshaji hutokea pia katika lugha ya utangazaji kwa sababu ya kasi ya mchezo wenyewe na muda mchache walio nao watangazaji ambao hauwaruhusu

kukumbuka maneno fulani au baadhi ya majina ya wachezaji katika kueleza mfululizo wa matukio ya mchezo. Hata hivyo, wanatarajia kuwa wasikilizaji wao ambao ni mashabiki wa mchezo huu huelewa maana ya kauli hizi zilizodondoshwa kwa sababu wanang'amua miktadha ambamo zimetumiwa (Tazama Kiambatisho 5).

Kutokana na matini hizi zinazohusu upanguaji, uchopekaji na udondoshaji zilizochambuliwa, sifa kuu ya nadharia geuzi ambayo ni uwezo wa sheria chache kuzalisha sentensi nyingi zisizoweza kuhesabika katika lugha kutokana na umilisi wa mzawa wa lugha na ambazo zina uamilifu wa kimawasiliano hubainika.

### 3.3.2 Uwakilishaji/Urejeshi

Uwakilishaji ni dhana inayotumiwa katika isimu kumaanisha vipashio vya lugha vinavyosimamia vile visivyotajwa katika matini. Kirejeshi nacho ni neno au kiambishi katika neno kinachohusishwa na jambo fulani lililotajwa awali. Uwakilishi rejeshi hivyo basi hujitokeza kwa neno au kiambishi kinachowakilisha jambo lililokwishatajwa awali. Wanaoweza kurejelewa katika sajili ya mchezo wa kandanda kutokana na lugha ya utangazaji ni wachezaji na watangazaji. Data yetu iliwakilisha uwakilishaji huu kama ifuatavyo.

1. ...mchezaji huyu anaonyesha kuwa *yeye* si mchache, *a*namdhihirishia kocha wake kwamba alifanya busara kumchezesha.

Kipande 'yeye si mchache' ni urejeshi. Kinachorejelewa na kuwakilishwa na 'yeye' ndicho kinachorejelewa na kiambishi 'a' kinachowakilisha nafsi ya tatu umoja.

2. Naona wachezaji wa timu ya Sofapaka *wa*narejea uwanjani na kujipanga katika nafasi zao, ishara kuwa *wao wa*ko tayari kumenyana tena na wenzao katika kipindi hiki cha pili kitakachoanza wakati wowote kutoka sasa.

Kinachorejelewa na 'wao' ndicho kinachowakilishwa na kiambishi 'wa' cha nafsi ya tatu wingi. Virejelewa katika matini za (1) na (2) ni mshambulizi na wachezaji mtawalia.

3. ...*A*nachanja pale-ee go-goo-oool! *A*nasherehekea kwa kujipiga kifua na kujiambia kuwa *yeye* ndiye dume wa kufanya mambo.

Kiwakilishi 'yeye' na kiambishi 'a' vinarejelea mchezaji anayewakilishwa na nafsi ya tatu umoja.

4. Waliokuleteeni matangazo haya ya kabumbu ni *sisi* watangazaji wenu Ali Salim Manga na Jack Oyoo. *Tu*kutane tena uwanjani siku nyingine, *tu*nasema kwa herini.

'Sisi' ni nafsi ya kwanza umoja kinachowakilishwa na kiambishi 'tu'. Vinarejelea watangazaji hawa.

Matini hizi zinaonyesha urejeshi kama kipengele kinachotumika sana katika muundo wa matini kuleta muwala na uhalisia katika usemi. Aidha, urejeshi huwezesha msisitizo unaofanya ujumbe ueleweke zaidi na wasikilizaji.

### 3.3.3 Uunganishi/Uhusishi

Kapinga (1983) anaeleza viunganishi kama aina mojawapo ya maneno yanayounganisha na kuonyesha uhusiano baina ya neno na jingine au baina ya fungu moja la neno na jingine. Viunganishi huwa na dhima ya kuleta vipashio vya lugha pamoja (Mgullu 1999). Kupitia uunganishi, vipashio vya lugha vinavyohusika huwa na nguvu za mshikamano. Nguvu hizi zinadhihirika kupitia muumano wa sentensi au wa vijenzi vyake. Viunganishi hutumiwa kama daraja hivi kwamba vikikosekana basi mshikamano wa matini na uyakinifu wa ujumbe haujitokezi kikamilifu. Baadhi ya data iliyodhihirisha matumizi ya viunganishi ni ifuatayo.

a) Mpendwa msikilizaji popote ulipo tunakukaribisha katika dimba hili la leo. Hii ni mechi kali inayotazamiwa kuwa ngumu sana *kwa sababu* inahusu timu mbili hasimu tangu jadi *na* zinazotazamia kunyakua taji la ligi msimu huu.

b) *Mara ya mwisho* timu hizi maadui zilipokutana ziliweza kufanya ukatili wa kuumiza nyasi bure kwa kutoka suluhu bin suluhu, sijui leo mambo yatakuwa vile vile *au* vipi. Malango yote mawili ya timu hizi maarufu

yalilalamika *kwa sababu* ya kulazwa njaa, tusubiri tuone kama leo yatalishwa.

c) Timu zote mbili zinajivunia ubingwa wa miaka ya nyuma *na* wachezaji wakali waliosifika sana katika ligi hii *na* kanda yote ya Afrika Mashariki na Kati. Naona zimejinoa hapa katika harakati zao za kuendeleza ubabe wao.

d) Mpendwa msikilizaji ngoma inaanza pale katikati ya uwanja *baada ya* refa kupuliza kipenga chake ambacho daima huwa mdomoni mwake utadhani imepakwa asali ya nyuki.

e) Anaregesha mpira ule *hadi* kwenye safu ya ulinzi *ili* kupanga njama mpya ya kupenya ngome ya mahasimu wao ambao daima huwa thabiti kama chuma. Ulinzi wa ngome hii unaongozwa *na* mchezaji huyu mzito kama nanga mwenye miraba minne *na* aliye na tajriba kubwa ya miaka na mikaka. Ni kama itawagharimu maadui zao majasho ya damu kupangua ngome hii thabiti.

f) Ananyunyiza pale mpira juu juu *hadi* pembezoni mwa uwanja na kutulizwa maridadi na kiungo wa wingi wa kushoto nani yule -ee. Anakwenda, anakwenda na mpira, anatoa krosi rojorojo pale kwenye lango *lakini* washambulizi wanachelewa. Sijui ni wazito *au* namna gani mambo hapa.

g) Anapokea msikilizaji mpira ule mree-efu na kutuliza kwenye gamba la kifua. Anageuka nao, piga kanzu pale Agwanda, anajaribu kuingia katika ngome ile *lakini* anazidiwa ubabe *na* walinzi wa Gor waliokuwa macho. Wanaondosha hatari ile.

Kiunganishi 'kwa sababu' kimetumiwa kuonyesha mambo yaliyochangia kutokea kwa hali fulani. Yaani, jambo lililochangia mechi kuwa ngumu katika matini (a) na malango kulala njaa katika matini ya ( b). Kiunganishi 'na' kimetumiwa katika matini ya (c), na (e) kuonyesha ufafanuzi na uendelezaji wa dhana zilizotangulia ili zieleweke vyema kwa wasikilizaji. Katika matini ya (c), kiunganishi 'na' kimetumiwa kuonyesha kuwa kilichochangia ubingwa wa timu husika katika miaka ya nyuma ni wachezaji wazuri waliosifika katika eneo lote la Afrika Mashariki na Kati huku katika matini ya (e) kimetumiwa kufafanua sifa ya mchezaji anayelinda ngome kwa uthabiti. Katika matini ya (g), kiunganishi hiki kimetumiwa kutambua walinzi wa timu ya Gor waliomzidi nguvu mchezaji Agwanda. Matumizi ya maelezo haya ni muhimu katika kuwasaidia wasikilizaji kufuatilia namna mchezo huu unavyoendelea.

Kwa upande mwingine, matumizi ya kiunganishi 'lakini' kinaonyesha sababu za kutowezekana au kutokamilika kwa hali fulani ya uchezaji na mabadiliko ya mkondo wa mchezo wenyewe. Katika matini ya (f), krosi nzuri iliyoelekezwa langoni haijazalisha bao kwa sababu ya wachezaji kushindwa kuifikia. Hali kadhalika katika matini ya (g), mchezaji Agwanda anashindwa kufunga bao kwa

kuzidiwa na walinzi wa timu ya Gor Mahia. Matukio haya mawili yanabadilisha mkondo wa mchezo.

Kiunganishi 'au' nacho kimetumiwa kuleta mshikamano wa matini. Mtangazaji ametumia kiunganishi hiki kuonyesha hali ya kutokuwa na hakika kuhusu timu itakayoshinda mechi katika matini (b) na kutojua sababu iliyowafanya wachezaji wasiupate mpira katika matini ya (f) Kihusishi 'ili' nacho kimetumiwa kuonyesha kichocheo cha tukio lililotokea; yaani kurejesha mpira nyuma kunachochewa na hitaji la kupanga mikakati ya kupenya ngome ya wapinzani wao. Kwa jumla, vihusishi 'na', 'lakini', 'au' na 'ili' vimepata dhima ya kupambanua mfululizo wa matukio kama yalivyotokea mchezoni ili kueleweka na wasikilizaji.

Kihusishi 'mara ya mwisho' kimetumika katika matini ya (b) kubainisha wakati timu husika zilipokutana na kucheza dhidi ya nyingine huku 'baada ya' kikitumiwa katika matini ya (d) kuonyesha kuwa tukio moja (refa kupuliza kipenga) lilitangulia lingine (mchezo kuanza). Hivyo basi, vihusishi hivi vimedhihirisha mshikamano wa wakati.

Kihusishi 'hadi' kimepewa dhima ya kudhihirisha mshikamano wa mahali. Kimebainisha mahali mchezo ulianzia na pale ulipomalizikia. Katika matini ya (e), kihusishi 'hadi' kimetumiwa kuonyesha kuwa mpira umechezwa kuelekea safu ya ulinzi. Hali kadhalika, kihusishi hiki kimetumika katika matini ya (f) kuonyesha mpira umeelekea pembeni mwa uwanja. Matumizi ya kihusishi hiki hutoa

uelekezi unaowasaidia wasikilizaji kubaini sehemu ya uwanja ambao mchezo unafanyika kwa wakati fulani na hivyo kufuatilia matukio ya mchezo kwa urahisi.

**3.4 Hitimisho**

Sura hii imechanganua matini ili kubainisha maana zinazowasilishwa katika sajili ya mchezo wa kandanda. Uchanganuzi huu umebainisha kuwa lugha huwa na maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi. Aina hizi za maana zilizojitokeza ndizo mihimili ya nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo inayoongoza utafiti huu.

Lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda imebainisha maana dhanishi kupitia vitenzi, nomino na vivumishi. Imedhihirika kuwa si wakati wote ambapo vipashio hivi vya lugha hutumiwa kwa maana yake tambuzi katika utangazaji wa mchezo wa kandanda. Vipashio hivi vinatumiwa kwa njia inayopanua, kugeuza na kuhamisha maana yake halisi katika utoshelevu wa ujumbe na uyakinifu wa mawasiliano. Matumizi ya vipashio hivi yamefinyangwa kwa namna inayosawiri mchezo wa kandanda kama vita na uadui licha ya kuuhusisha na maswala ya ushirikina na unyumba.

Hivi ni kusema kuwa maana ya vipashio huweza kupanuka na hata kubadilika kulingana na matumizi yake katika miktadha tofauti. Uchanganuzi huu umepambanua lugha kama chombo kinachobadilika kutokana na mahitaji ya watumizi wake na kuthibitisha nadharia ya SAM inayosema kuwa lugha huwa na



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

maana dhanishi pale watumizi wake wanaposimba tajriba za ulimwengu wao kuzieleza hali zinazowazunguka. Imebainika kuwa wakati mwingine maana ya vipashio vya lugha haiwi katika viashiria vyake bali matumizi yake.

Maana tagusani imedhihirisha tendo la usemi kupitia kauli za maagizo, rai, maswali na kauli ndefu za kimaelezo. Kauli za maagizo zinasheheniwa na wasimamizi wa mchezo huu katika kuusawazisha na kuudhibiti huku kauli za rai na maswali yakitumiwa sana na wachezaji wanapojieleza kwa wasimamizi uwanjani au wanapozungumza miongoni mwao. Mazungumzo, majibizano na majibu yanayotokana na kauli hizi hujenga mahusiano miongoni mwa watumizi hawa wa lugha. Hii ni kwa sababu katika mchakato huu wote, hata wasikilizaji huwa na uwezo wa kubashiri mielekeo ya wenzao na hivyo kuhusiana nao kwa njia inayowafanya wote wakubalike katika jamii. Kauli za maelezo marefu hujitokeza kama sifa muhimu ya lugha inayotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda katika kueleza mfululizo wa matukio ya mchezo wenyewe kama unavyotokea ili kueleweka na wasikilizaji na kufikisha ujumbe kwa uwazi zaidi.

Maana matinishi imetumikisha kanuni za kisarufi na kusarifu ujumbe kutokana na ugeuzi wa upanguaji, uchopekaji na udondoshaji. Licha ya kuonyesha uhalisia wa lugha ya maongezi ya kawaida, ugeuzi huu huwawezesha watangazaji kutumia lugha kwa njia inayozalisha matini nyingi zenye dhana sawia ili kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji wao kwa njia bora zaidi bila kurudia baadhi ya vipashio vinavyoeleweka kwao wote.

Aidha maana matinishi imebainika kutokana na urejeshi unaoleta muwala na msisitizo wa ujumbe katika usemi. Pamoja na haya, maana matinishi imedhihirika kupitia matumizi ya vihusishi vinavyofaulisha mawasiliano kwa kuunganisha vipande vya maneno kuunda matini zenye mshikamano kwa njia inayowasaidia wasikilizaji kufuatilia matukio na mkondo wa mchezo kwa urahisi.

Uchanganuzi wa matini katika sura hii umeonyesha kuwa maana tagusani ambayo huwa na uamilifu husishi inatumiwa kuyakinisha maana dhanishi. Huku maana dhanishi ikiwakilisha dhati ya ujumbe, maana tagusani huangazia kaida zinazodumishwa na jamii ili kudhibiti mawasiliano kimuktadha. Maana dhanishi na maana tagusani hujitokeza kama amali za kimsingi ambazo utoshelevu wa dhima zake hutegemea amali ya maana matinishi. Hii ina maana kuwa vipashio vya lugha huunganika kuleta maana amilifu kulingana na muktadha na kaida za jamii. Kwa jumla imebainika jinsi maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi zinavyohusiana na kudhibitiana ili kusuka tanzu za sintaksia, semantiki na pragmatiki.

Katika sura inayofuata, tumechunguza taaluma na sajili mbalimbali zinazotumiwa na sajili ya mchezo wa kandanda ili kujitosheleza. Tumetambua na kuonyesha jinsi taaluma na sajili zinazohusika zinavyosukwa na kutumiwa kama msingi wa kujenga na kufuma sajili ya mchezo wa kandanda.

# SURA YA NNE

# UFUMAJI WA SAJILI YA MCHEZO WA KANDANDA

## 4.0 Utangulizi

Sura ya tatu imebainisha aina tofauti za maana zinazotokana na matumizi ya lugha katika sajili ya mchezo wa kandanda. Sura hii imeonyesha taaluma na sajili mbalimbali zinazotumiwa na sajili ya mchezo wa kandanda ili kujitosheleza. Kwa kuwa takriban lugha zote za ulimwengu huazima baadhi ya maneno machache kutoka lugha nyingine kama njia mojawapo ya kujiimarisha, hakuna lugha inayojitosheleza. Hata hivyo, sajili ya mchezo wa kandanda huonyesha utegemezi mkubwa wa taaluma na sajili nyingine katika kujisuka na kujifuma.

Tumebainisha kuwa sajili ya mchezo wa kandanda hutumikisha mno vipashio na istilahi za taaluma ya ulinzi, sajili ya biashara, sajili ya utabibu, sajili ya hoteli au taaluma ya upishi na sajili ya mapenzi katika kujitosheleza. Istilahi hizi zimejitokeza kama vitenzi, nomino, vivumishi na semi.

Hudson (1995) anaeleza kuwa kama mfumo nasibu unaowezesha mawasiliano, lugha huhitaji urudifu wa neno linaloashiria dhana fulani ili kulizoesha kwa matumizi hayo. Hali hii huzua miktadha maalum ya matumizi ya lugha. Miktadha hii mahsusi ndiyo inayozua sajili mbalimbali kutegemea shughuli na mahitaji ya wanajamii. Miktadha hii mahsusi hupambanua lugha kwa mujibu wa inakotumiwa na inavyotumiwa na kutoa mwongozo katika uteuzi wa aina fulani ya misamiati,

maudhui na miundo ya sentensi inayotumiwa kudokeza maana wakati lugha inatumiwa.

Spolsky (1998) anaeleza kwamba sajili hutambuliwa kwa misamiati na istilahi zinazojenga msingi wa taaluma husika. Hivi ni kusema kuwa lugha inayohusishwa na taaluma au sajili fulani huwa na sifa bainifu na misamiati au istilahi tambuzi. Hii inamaanisha kuwa sajili mbalimbali huwepo kwa kudhihirisha uteuzi wa misamiati mahsusi na upekee wa matumizi ya lugha kimuktadha.

Hata hivyo, hali hii haijitokezi katika sajili ya mchezo wa kandanda. Sajili hii inadhihirisha utegemezi wa istilahi, misamiati na vipashio vya sajili na taaluma tofauti kufuma sifa, kusuka na kuibua maana. Hivi ni kusema kuwa sajili ya mchezo wa kandanda haijisimamii kiistilahi wala kujitegemea kimaana. Katika hali ya kujitosheleza kimatumizi, sajili hii huchota vipashio kutoka kwingineko na kuvifinyanga ili kuibua maana. Ni kwa namna hii ambavyo upekee wa matumizi ya lugha na uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda hudhihirika. Kulingana na data yetu iliyochanganuliwa, taaluma na sajili zinazotumiwa na sajili ya mchezo wa kandanda ili kujitosheleza ni ulinzi, biashara, utabibu au hospitali, hoteli na mapenzi.

### 4.1 Taaluma ya Ulinzi

Sajili ya ulinzi hutambuliwa kwa misamiati na istilahi zinazohusiana na vita, makabiliano, uadui, maangamizi na zana za vita. Istilahi za taaluma hii

zinazotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda zinahusu vitenzi, nomino, vivumishi na semi.

### 4.1.1 Vitenzi katika Taaluma ya Ulinzi

Vitenzi ni mojawapo ya vipashio vya taaluma ya ulinzi vinavyotumiwa kufuma sajili ya mchezo wa kandanda. Vitenzi hivi hubainisha hali ya vita, uadui, maangamizi na maumivu.

**Jedwali 4.1: Vitenzi katika Taaluma ya Ulinzi**

| **Kitenzi** | **Maana** |
|---|---|
| Charaza | Piga kwa mfululizo |
| Kandamiza | Tawala kwa kutumia uonevu, dhuluma, nguvu na vitisho. |
| Winda | Vizia aghalabu mnyama msituni, kwa kumsaka na kumpiga kwa silaha. |
| Menya | Ondoa maganda ya kitu kama vile chungwa au kiazi. |
| Chapa | Piga kwa kutia adabu au kuumiza. |
| Adhibu | Kutesa, kutaabisha au kurudi |
| Lipua | Fanya kitu kifumuke au kipasuke kwa nguvu kwa sababu ya moto. |
| Tandika | Kupiga au kuchapa. |
| Umiza | Tia majeraha au sababisha kuvunjika kwa kiungo. |
| Noa | Tia makali kama vile kisu au panga ili iweze kukata. |
| Nyonga | Ua kwa kupopotoa shingo au kutia kitanzi. |
| Tisha | Kutia hofu au kuogofya. |
| Tesa | Tia kiumbe maumivu au machungu kwa muda mrefu. |
| Ua | Ondoa uhai wa kitu au mtu. |
| Vamia | Shambulia bila ya kuwa na haki ya kufanya hivyo. |
| Shambulia | Tumia kitu kama vile silaha, fimbo au ngumi ili kupiga mtu, |

| | |
|---|---|
| | aghalabu adui. |
| Pambana | Shindana kwa maneno, vitendo au vita; gongana kwa nguvu. |
| Zaba | Piga kwa kofi. |
| Nyemelea | Endea kitu kimya na polepole kama vile mwindaji afanyavyo. |
| Uma | Shika na bana kwa meno. |
| Nyanyasa | Fanyia mtu vitendo vya dharau au maonevu. |
| Twanga | Ponda kitu kama vile mahindi katika kinu ili kutoa maganda katika punje. |
| Fyeka | Kata miti au nyasi kuwa fupi. Pia ni kuua adui wakati wa vita bila kubakisha. |
| Nasa | Shika kama mtego. |
| Pokonya | Chukua kitu cha mtu kwa nguvu au kwa kumdhulumu. |
| Okoa | Toa katika hatari. |
| Vizia | Jificha mahali kungojea au kufuatia kitu au mtu taratibu ili umshike au umpige |
| Piga | Kutanisha vitu viwili kwa nguvu; chapa, tandika. |
| Komboa | Fanya mtu aliyekuwa amefungwa au kudhulumiwa au kutawaliwa awe huru. |

Hali ya klabu fulani kucheza na kupata ushindi dhidi ya nyingine katika mchezo wa kandanda unaangaliwa sawa na *kucharaza, kukandamiza, kuchapa, kuuma, kufyeka, kunyanyasa, kutwanga, kuadhibu, kulipua, kutandika, kupiga, kuumiza, kunyonga, kupokonya, kuzaba, kuvizia* na *kutesa* timu inayoshindwa.

Kwa mfano, katika matini 'Sofapaka *imeitandika* Tusker mabao manne kwa mawili' inamaanisha kuwa timu ya Sofapaka imeifunga ile ya Tusker mabao manne kwa mawili. Hali kadhalika, matini 'Katika Manchester derby second leg, City *inaichapa* United mabao matatu bila jibu baada ya *kuilipua* mabao manne kwa moja katika mkondo wa kwanza' inamaanisha kuwa klabu ya Manchester City iliishinda ile ya

Manchester United mabao manne kwa moja katika mkondo wa kwanza kabla ya kuishinda mabao matau kwa nunge katika mkondo wa pili.

Harakati za timu kujitayarisha ili kuonyesha mchezo mzuri na kupata ushindi zinafananishwa na *kujinoa*. Hali ya mchezo wa kandanda kuendelea huku kila timu ikijaribu kufunga bao inaangaliwa sawa na *kumenyana* huku hali ya klabu fulani kuonyesha mchezo wa kiwango cha juu ilifananishwa na timu *kutisha. Okoa* ni kitenzi kinachotumiwa kurejelea hali ambapo mchezaji anazuia mpira kuingia katika lango lake. Hali kadhalika, kitenzi hiki huweza kutumiwa kwa maana sawa na kitenzi *komboa* kurejelea hali ya mchezaji kufunga bao la kusawazisha ili kuepuka kushindwa.

Juhudi za timu za kufunga bao au kusajili mchezaji mpya zinalinganishwa na *kuwinda* au *kunyemelea* mchezaji huyo. Mchezaji husika anaposajiliwa, inasemekana kuwa *amenaswa*. Kwa mfano, matini 'Msikilizaji kabla ya *kunaswa* na The Gunners, nyota huyu Mjerumani ambaye amekuwa nguzo ya safu ya katikati *alinyemelewa* na timu maarufu kama vile Chelsea na Manchester United.' Inamaanisha kuwa kabla ya mchezaji Ozil kusajiliwa na timu ya Arsenal, klabu za Chelsea na Manchester United zilitafuta huduma zake.

### 4.1.2 Nomino katika Taaluma ya Ulinzi

Baadhi ya misamiati ya taaluma ya ulinzi inazotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda ni nomino zinazorejelea zana za vita, nomino zinazohusisha mchezo wa

kandanda na makabiliano au uhasama na nomino zinazohusisha mchezo wa kandanda na nguvu na mamlaka ya kiutawala.

**Jedwali 4.2: Nomino Zinazorejelea Zana za Vita**

| Nomino | Maana |
|---|---|
| Bomu | Silaha inayotengenezwa kwa vitu vinavyolipuka ambavyo husababisha maafa makubwa mahali inapolipukia. |
| Risasi | Kitu cha madini ya chuma chenye umbo la mviringo na chenye ncha mbele na kinachofyatuliwa au kulipuliwa kwa baruti kwenye mwili uliolengwa. |
| Jiwe | Kipande cha mwamba kilicho kigumu sana; mwamba. |
| Silaha | Kitu kinachotumika kupigia na ambacho kinaweza kujeruhi au kuua. |
| Mzinga | Chombo kinachotengenezwa kwa chuma chenye mwanzi mkubwa ambao hutumiwa kurusha risasi kwa nguvu zaidi kuliko bunduki. |
| Bunduki | Silaha ya kufyatulia risasi kwa nguvu. |
| Mkwaju | Fimbo ndefu ya kuchapia. |
| Kombora | Bomu linalofyatuliwa na mzinga. |
| Wembe | Kifaa kidogo cha madini chenye umbo bapa na chenye makali pande zote mbili, kinachotumiwa kwa kunyolea au kukata. |
| Ngome | Boma la mawe au la miti linalotumika kwa kujihami dhidi ya maadui hasa wakati wa vita. |
| Manowari | Chombo cha baharini kilichoundwa kwa chuma na kinachobeba silaha za kivita. |

Katika sajili ya mchezo wa kandanda, mpira unaochezwa kwa nguvu kuelekea lango ili kufunga hulinganishwa na zana za vita kama vile *bomu, risasi, mzinga, bunduki, kombora, jiwe* na *mkwaju.* Matini "Mshambulizi huyu Rooney

ameangusha *bomu* zito lililomlipua kipa" na "... Hazard anachenga moja, ...anatuma *kombora* zito pale-ee, mkwaju ule unajaajaa kimyani!" zinamaanisha kuwa wachezaji Rooney na Hazard walipiga mpira kwa nguvu nyingi na kufunga.

Nomino *silaha* na *wembe* hutumiwa kurejelea wachezaji mahiri, hasa wa safu ya mbele walio na uwezo wa kuwachenga wenzao na kufunga mabao mengi. Safu ya ulinzi au ya nyuma iliyo na jukumu la kuzuia mpira usipite wala kufunga inanasibishwa na *ngome*. Timu pinzani huangaliwa kama maadui wanaopaswa kuangamizwa kwa zana hizi za vita. Nomino *manowari* kutumiwa kitamathali kama *laliwa manowari* kurejelea hali ya mchezaji kuchezewa visivyo na mwenzake kwa kulazwa chini kwa kutumia miguu.

Hali kadhalika, baadhi ya istilahi za taaluma ya ulinzi zinazopata matumizi teule ni nomino zinazohusisha mchezo wa kandanda na makabiliano au uhasama kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali 4.3.

**Jedwali 4.3: Nomino Zinazohusisha Mchezo wa Kandanda na Makabiliano au Uhasama**

| Nomino | Maana |
|---|---|
| Mahasimu | Watu ambao wamegombana na wengine na hawasemezani. |
| Patashika | Hali ya kuwania au kugombea kitu fulani kwa nguvu na vishindo. |
| Mapinduzi | Uondoaji madarakani viongozi wa serikali, hususan kwa |

| | |
|---|---|
| | kutumia nguvu. |
| Moto | Joto kali linaloweza kuunguza. |
| Mashambulizi | Tendo la uvamizi, vamio, hujuma. |
| Mapambano | Shindano la maneno au vitendo. |
| Kizaazaa | Hali ya fujo ambapo watu hawasikilizani. |
| Kikosi | Mkusanyiko wa askari zaidi ya elfu moja. |
| Kindumbwendumbwe | Kugombea kitu; ghasia, fujo. |
| Adui | Kiumbe au mtu anayemtendea mwingine uovu. |
| Kinyang'anyiro | Mashindano makali ya kutafuta ubingwa. |
| Ukatili | Hali ya kutokuwa na huruma; udhalimu, ujahili au ubedui. |
| Mlinzi | Mtu ambaye kazi yake ni kuangalia usalama wa mahali fulani au kitu kilichohifadhiwa. |
| Mauaji | Kitendo cha kuua |

Hali ya kuendelea kwa mchezo wa kandanda hulinganishwa na *patashika, mapambano, kizaazaa, kindumbwendumbwe, kinyang'anyiro* na *mchuano.* Hii ni kwa kuwa wachezaji wa timu zozote zinazohusika katika mchezo hujizatiti kwa njia zote kupata ushindi. Mpira unaochezwa kwa nguvu kuelekea lango kwa nia ya kufunga bao hurejelewa kama *mashambulizi.* Kwa mfano, matini 'Wanang'ang'ia mpira pale, *mshambulizi* anakataa katakata kupokonywa mpira, *kizaazaa* kwenye lango, kivumbi kinatifuka, *patashika* nguo kuchanika' inarejelea hali ya wachezaji walinzi kujaribu kuzuia mpira usifunge huku wafungaji kufanya kila jitihada kupata mpira na kufunga bao.

Wachezaji wa timu fulani huwatazama wale wanaocheza nao kama *mahasimu* na *maadui* wanaopaswa kuangamizwa. Jumla ya idadi ya wachezaji wa timu fulani hurejelewa kama *kikosi* huku mchezaji wa safu ya nyuma akirejelewa kama *mlinzi.*

Nomino *mapinduzi* inatumiwa kuonyesha hali ambapo timu ambayo imeshafungwa hujibidiisha kusawazisha na hatimaye kupata bao la ushindi huku kushindwa kwa timu fulani kwenye mchezo kukinasibishwa na kufanyiwa *ukatili* au *mauaji*. Hali kadhalika, timu au mchezaji anayeonyesha mchezo wa hali ya juu hujulikana kama *moto*. Matini 'Anatuliza mpira Suarez kwenye gamba la kifua, anachenga moja...anapiga goo-goo-oool! Anafanya *mauaji* hapa. Mchezaji huyu amekuwa *moto* wa kuotea mbali' inamaanisha kuwa Suaerz ni mchezaji mzuri aliye na uwezo wa kuchenga na kufunga.

Inajitokeza kuwa baadhi ya misamiati ya taaluma ya ulinzi ni nomino zinazohusisha mchezo wa kandanda na nguvu, uwezo na mamlaka ya kiutawala. Jedwali 4.4 linaonyesha hali hii.

**Jedwali 4.4: Nomino Zinazohusisha Mchezo wa Kandanda na Nguvu na Mamlaka ya Kiutawala**

| Nomino | Maana |
|---|---|
| Vigogo | Watu wenye madaraka makubwa ya kiutawala. |
| Mibabe | Watu wakubwa wenye nguvu. |
| Majogoo | Kuku madume; majimbi. |
| Mafahali | Ng'ombe dume. |
| Farasi | Mnyama wa kufugwa wa jamii ya punda lakini mkubwa zaidi na anayetumiwa kubeba watu na kuvuta gari au kwenye mashindano ya kukimbia. |
| Punda | Mnyama wa jamii ya farasi lakini mdogo na hutumiwa kukokota magari au kubeba mizigo. |

| | |
|---|---|
| Wafalme | Watawala wanaume. |
| Miamba | Majabali au mawe makubwa yaliyo majini au nchi kavu. |

Nomino za kurejelea watu wenye nguvu, uthabiti, uwezo na mamlaka ya kiutawala kama *Vigogo, mibabe,* na *wafalme,* za kuitia wanyama kama vile *majogoo, mafahali, farasi, wafalme* na za kurejelea maumbile kama vile *miamba* hutumiwa kurejelea klabu zenye historia ndefu ya kushinda mechi nyingi au kutwaa mataji kadha. Hivi ni kusema kuwa klabu husika huzitawala nyingine zinazoonekana dhaifu kwa kutosajili matokeo mazuri katika mchezo huu. Klabu hizi zinazoshindwa na kupata matokeo mabaya huangaliwa sawa na *punda.*

Matini '...Kumbuka kwamba *miamba* hawa wa soka AFC na Gor wanapokutana huwa ni derby hapa Nairobi, kila timu ikijaribu kufanya mapinduzi na kuonyesha *ubabe* wake na *'Vigogo* hawa Liverpool wanapigiwa upatu wa kutwaa taji la ligi ya Uingereza mwaka huu baada ya kuonyesha makali katika safu ya mashambulizi' zinamaanisha kuwa AFC Leopards, Gor Mahia na Liverpool ni klabu maarufu, zenye nguvu na uwezo wa kutwaa mataji mengi.

### 4.1.3 Vivumishi katika Taaluma ya Ulinzi

Kipashio kingine kinachotumiwa kusuka sajili ya mchezo wa kandanda kama tukio la kivita na uhasama ni vivumishi vya sifa kama vile *butu* na *kali* na vivumishi vya nomino kama vile *matata* na *hatari.*

**Jedwali 4.5: Vivumishi katika Taaluma ya Ulinzi**

| Kivumishi | Maana |
|---|---|
| Butu | Isiyo kali au isiyokata; gutu. |
| -kali | Yenye ncha iliyochongeka au inayokata sana. |
| Matata | Mvurugiko wa mambo, hali ya vurugu. |
| Hatari | Hali ya kutokuwa katika usalama; hali ya kuleta maafa. |

Kivumishi *butu* kinatumiwa kurejelea mchezaji au timu isiyo na uwezo wa kushinda mechi au mchezaji asiye na uhodari wa kufunga mabao kwa kupoteza nafasi nyingi za kufunga. Kwa upande mwingine, *-kali* ni kivumishi kitumiwacho kumaanisha mchezaji au timu yenye uwezo wa kushinda mechi zake au mchezaji mwenye uwezo wa kufunga mabao kila apatapo nafasi.

Kwa mfano, matini 'Wanaingia pale Arsenal, Carzola kwake Wilshire, Wilshire anamtilia Giroud, anakwenda-aa nje! Anakosa nafasi ya tatu ya wazi huyu Giroud, amekuwa *butu* hapa' hutoa dhana kwamba mchezaji Giroud hana makini ya kulenga lango ili kufunga bao kutokana na pasi nzuri aliyoandaliwa na Wilshire. Kwa upande mwingine, matini '...Msikilizaji, Odhiambo anaingia uwanjani and just in his second touch on the ball, anafunga bao maridadi. Kweli mshambulizi huyu ni *mkali* sana' inaonyesha kuwa Odhiambo ni mchezaji makini anayetumia nafasi ya kwanza anayopata kufungia timu yake bao.

*Matata* na *hatari* ni nomino zinazopewa uamilifu wa kivumishi katika sajili ya mchezo wa kandanda. Maneno haya hurejelea mchezaji hodari na aliyesifika kwa kufunga mabao mengi kama alivyo Odhiambo katika mfano ulio hapo juu.

#### 4.1.4 Semi katika Taaluma ya Ulinzi

Hali kadhalika, semi hujitokeza kama kipashio kingine kinachotumiwa katika ufumaji wa sajili ya mchezo wa kandanda. Semi hizi ni zile zinazohusiana na maswala ya vita, uadui na uhasama.

**Jedwali 4.6 Semi katika Taaluma ya Ulinzi**

| **Semi** | **Maana** |
|---|---|
| Piga risasi | Piga kwa bunduki au bastola. |
| Piga pembe | Sukuma kwa nguvu kwa pembe kama afanyavyo ng'ombe mkali. |
| Kulipiza kisasi | Lipiza uovu kwa uovu uliotendewa. |
| Haribu sura | Umiza mtu vibaya usoni. |
| Tia mkononi | Piga au tesa. |
| Kaba koo | Shika au binya mtu kooni kwa kujaribu kumnyonga. |
| Teka nyara | Kamata na vizia mtu kwa nguvu kwa kumshinda katika vita. |
| Shika mateka | Chukua mtu kwa nguvu na kumdhibiti kama mtumwa ili akupatie kitu unachotaka. |
| Kodoa macho | Kodoa macho sana kwa kushangaa au kwa kukasirika. |
| Nyoshea kidole | Ashiria mtu kwa kidole kwa lawama au hasira. |
| Tifua kivumbi | Shikana na kusukumana kama ilivyo katika vita. |
| Pora mpira | Shindana na kumnyang'anya mtu mpira. |
| Umiza nyasi | Kanyaga nyasi kwa nguvu na mfululizo. |
| Panga njama | Afikiana kufanya jambo baya dhidi ya mtu au watu wengine. |

Katika utoshelevu wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda, watangazaji wa hutumia misemo *piga risasi, piga pembe, tia mkononi, kaba koo, teka nyara* na *shika mateka* na msimu *haribu sura* kurejelea hali ya timu fulani kushinda nyingine katika mchezo wa kandanda, aghalabu kwa kuifunga mabao mengi. Kwa mfano, matini 'Klabu ya Ulinzi *yaiharibu sura* Bandari kwa kuinyuka hapa goli mbili bila' na 'AFC Leopards *imetiwa mkononi* na Sofapaka, imeshatandikwa hapa mbili nunge' zinamaanisha kuwa timu ya Ulinzi na ya Sofapaka zimepata ushindi wa mabao mawili kwa bila dhidi ya timu ya Bandari na AFC Leopards mtawalia.

Msemo *kulipiza kisasi* inatumiwa kurejelea hali ya klabu fulani kudhamiria kuishinda klabu nyingine iliyoishinda katika mechi iliyotangulia huku msemo panga njama ukitumiwa kurejelea mikakati na mbinu inazotumiwa na klabu fulani ili kupata ushindi dhidi ya nyingine. *Nyoshea kidole* ni msemo unaotumiwa kwa maana ya wachezaji wa timu fulani kutoa habari zinazoonyesha kuwa wako tayari kukabiliana na kuwashinda wale wa timu nyingine katika mchezo utakaofuata.

Hali kadhalika, msimu *tifua kivumbi* hutumiwa kurejelea hali ya mchezo kuwa mgumu na wachezaji wa timu zote mbili kukabiliana kiasi cha kutojulikana timu itakayoweza kuibuka washindi. Aidha, *kupora mpira* ni msimu wenye maana ya mchezaji fulani kumpokonya mwingine mpira huku *umiza nyasi* ukipewa matumizi ya timu mbili kucheza kwa nguvu bila timu yoyote kuibuka washindi. 'Wanang'ang'ana pale katikati ya uwanja, Arteta *anampora mwenzake mpira* na

kuucheza mbele' ni matini inayomaanisha kuwa mchezaji Arteta amempokonya mwenzake mpira na kuucheza mbele.

## 4.2 Sajili ya Biashara

Sajili ya biashara hutambuliwa kwa istilahi zinazohusiana na soko, mnada, bidhaa, huduma na shughuli za uuzaji na ununuzi. Istilahi hizi zimejitokeza kama vitenzi, nomino na semi. Zifuatazo ni baadhi ya istilahi na misamiati ya sajili ya biashara inayotumiwa kuibua maana katika sajili ya mchezo wa kandanda.

**Jedwali 4.7: Istilahi za Sajili ya Biashara**

| **Istilahi** | **Maana** |
|---|---|
| Uza | Badilisha kitu kwa fedha au kwa kitu. |
| Nunua | Toa fedha ili kupata kitu kinachouzwa. |
| Lipa | Toa ada inayolingana na thamani ya kitu kinachouzwa. |
| Piga bei | Pendekeza kiasi cha fedha zinazohitajika kwa bidhaa. |
| Weka sokoni | Kubali kuuza bidhaa kulingana na thamani yake. |
| Peleka mnadani | Wasilisha bidhaa ili kutafuta wanunuzi wanaoweza kuzishindania bei. |
| Vunja benki | Tumia nguvu kuiba fedha kutoka kwenye benki. |
| Soko la Uhamisho | Mahali uhamisho wa wachezaji kutoka klabu moja hadi nyingine hufanyika. |
| Mchezaji wa Mkopo | Mchezaji kutoka timu nyingine. |
| Ofa | Kiasi cha fedha ambazo klabu fulani huwa tayari kutoa na kulipa kwa klabu nyingine ili kupata huduma za mchezaji mpya. |

| | |
|---|---|
| Dili | Makubaliano ya kiasi cha fedha ambazo klabu moja inalipa kwa nyingine kwa uhamisho wa mchezaji. |
| Mauzo | Fedha zinazopatikana katika biashara; mapato. |
| Mteja | Mtu anayekwenda kupata bidhaa au mahali fulani kama vile dukani. |

Katika sajili ya mchezo wa kandanda, harakati za klabu fulani kusajili au kupata huduma za mchezaji fulani hurejelewa kama *kununua* mchezaji. Wasimamizi wa klabu fulani wanapokubali kuruhusu mchezaji fulani kuhamia timu fulani, inasemekana kuwa *wamemuuza.* Hii ni kwa sababu usimamizi wa klabu hiyo hupokea kiasi fulani cha fedha na kuonekana kama *inalipwa.* Kwa upande mwingine, kitenzi *uza* kinatumiwa kurejelea hali ya mchezaji fulani kusababisha timu yake kushindwa kutokana kukosa makini kwenye mchezo. Klabu ambayo huduma za mchezaji wake huhitajika na klabu nyingine husemekana *kumpiga bei.* Klabu isiyohitaji tena huduma za mchezaji wake hasa kwa kushuka kiwango cha ubora wake husemekana *kumweka sokoni au kupelekwa mnadani.* Klabu inayotumia fedha nyingi kumsajili mchezaji mahiri husemekana *kuvunja benki.*

Matini 'Msikilizaji huyu Mata, kiungo matata kutoka Hispania *aliyenunuliwa* na Man United kutoka Chelsea kwa *dili* ya kitita cha pauni milioni ishirini na saba, aliingia kurutubisha *midfield* na baada ya dakika tano tu uwanjani, alipachika bao la tatu kimyani na sasa anaongeza la nne dhidi ya Norwich City. Si ajabu Chelsea *ilimuuza* shingo upande' inamaanisha kuwa klabu ya Manchester United ilipata huduma za mchezaji Mata baada ya kukubali na kutoa ada ya pauni milioni ishirini na saba kwa klabu ya Chelsea.

Klabu inayotaka kumsajili mchezaji husemekana *kutoa ofa* inapotangaza kiasi cha fedha inayoweza kulipia huduma za mchezaji husika. Hali kadhalika, klabu husika zinapokubaliana kuhusu uuzaji na ununuzi wa mchezaji inasemekana kuwa zimefikia *dili*. Mchezaji kutoka timu nyingine na anayeruhusiwa kuichezea timu tofauti kwa muda fulani kabla ya kurejea katika timu inayommliki hurejelewa kama *mchezaji wa mkopo*. Shughuli zote za usajili wa wachezaji kutoka klabu moja hadi nyingine hufanyika katika *soko la uhamisho*. Matumizi ya istilahi hizi za sajili ya biashara kwa namna hii husawiri wachezaji kama bidhaa au huduma zinazoweza kufanyiwa biashara sokoni.

*Mauzo* ni neno linalotumiwa kurejelea mchezaji yeyote anayechangia timu yake kushindwa na hivyo kulaumiwa kwa unyonge au kutomakinika uwanjani. Aidha, timu ambayo aghalabu hushindwa sana na nyingine hurejelewa kama *mteja* wake.

**4.3 Sajili ya Utabibu/Hospitali**

Hii ni sajili inayopambanuliwa na kutambuliwa kwa misamiati inayorejelea wagonjwa, wahudumu wa afya, dawa na vifaa vya utabibu. Data ifuatayo inaonyesha baadhi ya istilahi za sajili ya hospitali zinazohusishwa katika ufumaji wa sajili ya mchezo wa kandanda.

**Jedwali 4.8: Istilahi za Sajili ya Utabibu**

| Istilahi | Maana |
|---|---|
| Dawa | Kitu anachopewa mgonjwa aghalabu huwa cha vidonge, unga au majimaji ili kumtibu. |
| Hoi | -enye kuchoka sana au kutojiweza. |
| Ahueni | Nafuu aipatayo mgonjwa baada ya kuugua. |
| Mchawi | Mtu anayesadikika kuwa na uwezo wa kuwadhuru watu kwa kuwaroga. |
| Maiti | Mfu, mzoga au kimba. |
| Matanga | Mkusanyiko wa watu kuliko na msiba ili kuomboleza na kuwaliwaza wafiwa. |
| Pagawa | Ingiwa au pandwa na pepo mbaya kichwani. |
| Roga | Dhuru kwa uchawi. |
| Zika | Weka au fukia kitu, mzoga au maiti ndani ya shimo au kaburi. |
| Piga bao | Kujulishwa yaliyopita au kutabiriwa yajayo na mganga. |
| Kufa na kupona | Kupata kitu kwa namna au nguvu zote. |
| Machela | Kitu kama kitanda, aghalabu hutumiwa kubeba mtu aliye mgonjwa au maiti. |

Mchezaji au klabu iliyo na mazoea ya kufunga au kupata ushindi dhidi ya nyingine hurejelewa kama *dawa* yake. Klabu inayoonyesha mchezo dhaifu na matokeo duni hurejelewa kuwa *hoi*. Neno hilo hutumiwa kurejelea hali ambapo timu inazidiwa katika mchezo na kuelekea kushindwa. Kuzidiwa na kushindwa huku mchezoni ndiko kunakonasibishwa na *kuzikwa*. Timu inayojimudu kusajili matokeo mazuri baada ya msururu wa matokeo duni husemekana kuwa imepata *ahueni*. Aidha, neno hili hutumiwa kurejelea hali ya timu kuponea kufungwa bao au kushindwa katika mchezo. *Mchawi* ni nomino inayotumiwa katika sajili ya mchezo wa

kandanda kurejelea mchezaji mahiri aliye na uwezo wa kuwachenga wenzake na kufunga mabao ya kupendeza kiajabu.

*Pagawa* na *roga* ni vitenzi vinavyotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kurejelea hali ya mchezaji bora kuwashangaza na kuwachachawiza wenzake wa timu pinzani kwa kuonyesha mchezo wa hali ya juu na kufunga. Kwa mfano, matini 'Mpenzi msikilizaji tangu mshambulizi huyu van Persie kutua Man United baada ya kuwindwa na timu hii kwa misimu miwili amekuwa *akiwapagawa* waajiri wake hawa wa zamani. Leo amerudi uga wa Emirates *kuwaroga* tena Arsenal, anafunga bao maridadi la kusawazisha. Huyu ni *mchawi* kweli' inamaanisha kuwa tangu mshambulizi van Persie kuihama klabu ya Arsenal, amekuwa akiwashangaza kwa kufunga mabao na kusababisha klabu hiyo kushindwa kila anapocheza dhidi yao. Timu yenye kushindwa katika mechi hunasibishwa na *maiti* huku hali ya timu fulani kutazamia mechi ngumu au kushishwa katika mchezo ikiiangaliwa sawa na *matanga.*

*Piga bao* ni msemo unaotumiwa kusimamia juhudi na mikakati ya mkufunzi wa timu fulani kupata ushindi katika mechi ambayo imeratibishwa kuchezwa huku msemo kufa na kupona ukimaanisha hali ya wachezaji kucheza kwa nguvu na ujuzi wao wote ili kushinda mechi. Matini 'Msikilizaji wangu mechi hii ya fainali itakuwa ya *kufa na kupona,* hakuna timu itakayokubali kushindwa' inamaanisha kuwa wachezaji wa timu zote mbili wamejitayarisha kucheza kwa nguvu, juhudi

na ujuzi wao wote katika mechi hiyo ngumu ili kuibuka washindi wa taji. Aidha *machela* ni kitanda kitumiwacho kubeba wachezaji waliojeruhiwa.

### 4.4 Sajili ya Hoteli/ Taaluma ya Upishi

Istilahi bainifu za sajili hii ni zile zinazohusu wahudumu, wateja, aina ya vyakula, vifaa vya upishi na namna ya ulaji. Uchanganuzi wa data yetu umeonyesha matumizi ya vitenzi, nomino, vivumishi na semi zifuatayo katika uibuaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda.

**Jedwali 4.9: Istilahi za Sajili ya Hoteli**

| **Istilahi** | **Maana** |
|---|---|
| Iva | Kuwa mbivu, pevuka kama vile tunda au pikika kwa chakula na kuwa tayari kwa ajili ya kuliwa. |
| Kaanga | Choma au pika chakula kwa mafuta. |
| Chemka | Pata joto kwa kitu cha majimaji kiasi cha kuanza kugeuka mvuke. |
| Kula njano | Hali ya mtu kula kadi ya njano. |
| Kula nyekundu | Hali ya mtu kula kadi nyekundu. |
| -tamu | -enye ladha ya sukari au ya kuridhisha kinywani. |
| -bichi | -sio bivu, -siopikwa na kuiva vizuri, -siyopevuka. |
| -bivu | Iva au pevuka kwa tunda. |
| Krosi rojorojo | Mpira wa juu juu uliopigwa kuelekea lango. |
| Moto | Joto kali linaloweza kuunguza au kuivisha. |
| Pika bao | Andaa nafasi ya kufunga bao. |
| Nawa mpira | Kushika mpira kwa mkono. |
| Mezea mate | Kutamani kitu kama vile chakula kitamu. |
| Mega mpira | Kupiga pasi nzuri. |

| | |
|---|---|
| Lala njaa | Kupitisha usiku wote bila kula. |
| Kula na kutapika | Kutapika baada ya kula kuzidi kiasi. |

Mchezaji au klabu iliyoimarika na kuoyesha mchezo wa hali ya juu na kushinda mechi zake inarejelewa kuwa *imeiva* na wakati mwingine kuwa *tamu* au *moto*. Kivumishi *mbichi* hutumiwa hurejelea timu hafifu huku *mbivu* kikitumiwa kumaanisha timu pevu yenye kuonyesha mchezo wa kupendeza. Matini "Msikilizaji wangu, wadadisi wengi wa kabumbu wanatabiri kuwa leo hii Jumapili ndio siku ambayo wafalme wapya wa EPL watajulikana hapa ugani Anfield. *Mbivu* na *mbichi* itajulikana kati ya wenyeji Liverpool na Chelsea" imetumiwa kumaanisha kuwa matokeo ya mechi hii ndiyo itakayoamua timu nzuri itakayoshinda na hivyo kutawazwa mabingwa na ile dhaifu itakayoshindwa na hivyo kukosa taji.

Klabu moja inaposhinda timu nyingine, inasemekana *kuikaanga*. Hali ya mchezaji kutoa pasi nzuri inayochangia kupatikana kwa bao inarejelewa kama *kupika bao* huku hali ya mchezo kuendelea kwa muda mrefu bila bao kupatikana hurejelewa kama *malango kulala njaa*. Matini "...Mara ya mwisho timu hizi maadui zilipokutana ziliweza kufanya ukatili wa kuumiza nyasi bure kwa kutoka sare tasa, sijui leo mambo yatakuwa vile vile au vipi. Malango yote mawili ya timu hizi maarufu yalilalamika kwa sababu ya *kulazwa njaa*, haya tusubiri tuone kama leo *yatapikiwa mabao* na kulishwa" inamaanisha kuwa hakuna bao lililofungwa katika mechi hiyo kwa sababu ya ukosefu wa pasi au nafasi nzuri za kufunga.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Mpira unaochezwa juu juu kutoka pembeni mwa uwanja kuelekea lango hurejelewa kama *krosi rojorojo* huku hali ya kupiga pasi nzuri ikirejelewa kama *kumega mpira*. Mchezaji mwenye uwezo wa kutoa pasi nzuri na kuonyesha mchezo wa hali ya juu aghalabu huwapendeza wengi. Mchezaji kama huyo husemekana *kumezewa mate* na mashabiki au wasimamizi wa klabu mbalimbali. 'Mchezaji huyu matata ni mtamu kweli, si ajabu *anamezewa mate* na klabu nyingi za ligi kuu' ni matini inayoonyesha kuwa mchezaji anayerejelewa anawapendeza wasimamizi wa klabu nyingi za ligi kuu. Hali kadhalika, hali ya mchezaji kushika au kugusa mpira kwa mkono unaelezwa kama *kunawa mpira*. Matini 'Hatari hii, difenda *amenawa mpira* ndani ya box, ni penalty' inarejelea hali ya timu fulani kupewa adhabu ya penalti kutokana na mchezaji wa safu ya nyuma kushika mpira katika eneo la lango.

Hali ya uwanja kujaa sana mashabiki wanaoshuhudia na kushangilia mechi hurejelewa kama *uwanja kula na kutapika*. Adhabu ya onyo anayopewa mchezaji kwa kuonyesha mchezo mbaya au utovu wa nidhamu inarejelewa kama *kulishwa njano* huku adhabu ya kuondolewa uwanjani anayopewa mchezaji kwa kuonyesha mchezo mbaya au utovu wa nidhamu hurejelewa kama *kulishwa nyekundu*.

### 4.5 Sajili ya Mapenzi

Hii ni sajili inayotambuliwa kwa istilahi zinazorejelea harakati za kupata wachumba, uhusiano katika uchumba na kati ya wanandoa na maneno ya kuonyesha hisia za mapenzi. Uchanganuzi wa data yetu umeonyesha matumizi ya

istilahi zifuatazo za sajili ya mapenzi katika uibuaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda.

**Jedwali 4.10: Istilahi za Sajili ya Mapenzi**

| Istilahi | Maana |
|---|---|
| Mpenzi | Mtu anayependwa sana na watu au mtu. |
| Kipenzi | Mtu anayependwa sana na watu au mtu. |
| Zawadi | Kitu atunukiwacho mtu kuwa ni ishara ya mapenzi au wema. |
| Chumbia | Peleka maombi kwa wazazi wa binti kutaka kumwoa. |
| Tongoza | Shawishi mtu akubaliane na matamanio yako, aghalabu ya kimapenzi. |
| Posa | Peleka maombi kwa wazazi wa binti kutaka kumwoa. |
| Chanua | Fumbuka kwa maua. |
| Najisi | Jamiiana na mtu bila ya hiari yake. |
| Tahiri | Kata govi la mboo ili kichwa chake kiwe wazi; kata kinembe. |
| Tasa | Kiumbe yeyote wa kike asiyeweza kuzaa. |
| Oana | Kubaliana kuishi kama mke na mume kwa mujibu wa desturi zilizokubalika. |

Nomino *mpenzi* inatumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda kutambulisha na kujinasibisha na wasikilizaji wao huku *kipenzi* ikitumiwa kurejelea mchezaji anayeenziwa na wasikilizaji wengi kutokana na mchezo wake mzuri. Vitenzi *chumbia, posa* na *tongoza* hutumiwa kurejelea harakati za klabu fulani kurairai na kushawishi mchezaji wa klabu tofauti kuichezea. Kwa mfano, matini "...Mchezaji huyu Suarez anawika kweli, amekuwa moto wa kuotea mbali, huyu ni mtambo wa kufunga mabao na si ajabu *alichumbiwa* sana na timu kadha kama Arsenal na Real


Madrid katika dirisha la uhamisho wa msimu uliopita" inarejelea harakati za klabu ya Arsenal na Real Madrid kumsawishi mchezaji Suarez kuzichezea.

Timu inayoshindwa kufunga au kupata matokeo mazuri hurejelewa kama *tasa*. Neno hili pia hutumiwa kurejelea hali ya mchezo wa kandanda kumalizika bila timu husika kufungana bao lolote. Kwa mfano, matini "...Mara ya mwisho timu hizi maadui zilipokutana ziliweza kufanya ukatili wa kuumiza nyasi bure kwa kutoka *sare tasa,* sijui leo mambo yatakuwa vile vile au vipi" inamaanisha kuwa mchezo ulimalizika bila timu husika kufungana bao lolote. Hali ya kutofungana katika mchezo pia hurejelewa kama timu husika *kuoana* katika mchezo. Aidha kitenzi hiki pia hutumiwa kurejelea hali ya wachezaji fulani kufanana katika umbo au namna ya kucheza. Mpira unaofungwa kwa njia rahisi kutokana na uzembe au kutomakinika kwa mlinda lango au walinzi hurejelewa kama *zawadi*. Klabu au mchezaji anayeimarika katika mchezo wake anasemekana kuwa *amechanua.*

Matumizi ya istilahi na misamiati taaluma ya ulinzi, sajili ya biashara, sajili ya utabibu au hospitali, sajili ya hoteli au taaluma ya upishi na sajili ya mapenzi kusuka maana yanaonyesha utegemezi wa sajili ya mchezo wa kandanda kwa sajili nyingine. Hivi ni kusema kuwa sajili na taaluma hizi ndizo msingi wa ufumaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda. Hata hivyo, imebainika kuwa taaluma au sajili hizi huchangia kwa kiwango tofauti katika ufumaji na uibuaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda. Kulingana na takwimu za data tulizochanganua, taaluma au sajili hizi zote zimechangia vipashio au istilahi 132.

Taaluma ya ulinzi imechangia istilahi 80 ambazo ndizo nyingi zaidi. Idadi hii inawakilisha 60.61%. Sajili ya hoteli au taaluma ya upishi inafuata kwa kuchangia istilahi 16 inayowakilisha 12.12%. huku sajili ya biashara ikichangia istilahi 13 inayowakilisha 9.85%. sajili ya utabibu au hospitali imechangia istilahi 12 inayowakilisha 9.09% huku sajili ya mapenzi ikichangia istilahi 11 ambayo ni kiwango cha chini zaidi. Kiwango hiki kinawakilisha 8.33%. Mchango huu wa kila taaluma au sajili kitakwimu umeonyeshwa kwa kutumia chati ya viwango kama ifuatavyo.

**Mchango wa Sajili/Taaluma Mbalimbali katika Ufumaji wa Sajili ya Mchezo wa Kandanda**






KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Sababu kuu inayosababisha taaluma ya ulinzi kuchangia asilimia kubwa zaidi ya istilahi zinazojenga sajili ya mchezo wa kandanda ni kuwa licha ya timu zinazohusika katika mchezo kunuia kuwafurahisha na kuwachangamsha mashabiki na hata kujifurahisha wenyewe, kila timu hulenga kuibuka washindi wa mechi na taji. Mintarafu ya haya, mchezo wa kandanda hugeuka kuwa makabiliano kama yanavyotokea katika vita vya kawaida kati ya maadui halisi. Hali kadhalika, huku mashabiki, wachezaji na wakufunzi wa timu inayoibuka washindi wakifurahia na kushangilia, wale wa timu inayopoteza mechi huweza kukasirika, kuhuzunika na hata kulia. Hali hii wakati mwingine huweza kuleta uhasama wa kweli kati ya wachezaji, mashabiki na wakufunzi wa timu husika. Hali hii ndiyo inayoeleza mchango mdogo zaidi wa sajili ya mapenzi kwa kuwa inatawaliwa na lugha nyoofu, yenye rai, unyenyekevu na upole.

Matumizi ya vipashio na istilahi za taaluma au sajili hizi ili kufuma sajili ya mchezo wa kandanda yamepambanua lugha kama chombo kinachobadilika kulingana na mahitaji ya watumiaji wake na kuthibitisha nadharia ya SAM inayosema kuwa lugha huwa na maana dhanishi pale watumiaji wake wanaposimba tajriba za ulimwengu wao kuzieleza hali zinazowazunguka. Mbali na kutumiwa kwa maana yake tambuzi, vipashio hivi pia hutumiwa kwa njia inayogeuza na kupanua maana yake ili kufuma sajili ya mchezo wa kandanda. Hivi ni kusema kuwa maana dhanishi imejitokeza kama msingi wa kufinyanga vipashio hivi ili kutoa vivuli vya maana inayotosheleza uwiano wa ujumbe na uyakinifu wa kipragmatiki katika sajili ya mchezo wa kandanda.

### 4.6 Hitimisho

Katika sura hii, tumechanganua matini ili kubainisha taaluma na sajili tofauti zinazotumiwa na sajili ya mchezo wa kandanda katika kujifuma na kujitosheleza. Imebainika kuwa sajili ya mchezo wa kandanda huchota malighafi na vipashio vyake kutoka taaluma na sajili mbalimbali kama vile ulinzi, biashara, hospitali, hoteli na mapenzi.

Istilahi za taaluma ya ulinzi zimebainika kama vitenzi, vivumishi, semi, nomino zinazohusu zana za vita, nomino zinazohusisha mchezo wa kandanda na makabiliano au uhasama na nomino zinazohusisha mchezo wa kandanda na nguvu, uthabiti au mamlaka ya kiutawala.

Istilahi za sajili ya biashara zinazotumiwa kusuka sajili ya mchezo wa kandanda hubainika kupitia vitenzi na misimu huku sajili ya hospitali ikiwakilishwa na vitenzi, nomino, vivumishi na misemo. Istilahi za sajili ya hoteli zimebainika kutokana na matumizi ya vitenzi, vivumishi, misemo na misimu huku sajili ya mapenzi ikijitokeza kupitia matumizi ya vitenzi na nomino.

Matumizi ya istilahi na misamiati ya sajili au taaluma hizi kusuka maana zinaonyesha utegemezi wa sajili ya mchezo wa kandanda kwa sajili nyingine. Istilahi hizi ndizo zilizofinyangwa kimatumizi ili kupanua na kutoa vivuli tofauti vya maana. Ni kwa namna hii ambavyo uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda hujitokeza na kuwezesha sajili hii kujifuma na kujitosheleza.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii ni muhtasari wa yaliyoshughulikiwa katika tasnifu nzima. Sura hii imegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni matokeo ya utafiti, mahitimisho ya utafiti na mapendekezo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yameeleza kwa ufupi yaliyoangaziwa katika sura ya pili, sura ya tatu na sura ya nne. Sehemu ya mahitimisho ya utafiti inahusu maamuzi yaliyofanywa na mtafiti kutokana na uchanganuzi wa data. Aidha sura hii inatoa mapendekezo ya mtafiti kuhusu utafiti zaidi unaoweza kufanywa kuhusiana na eneo hili la utafiti.

Utafiti huu umetekelezwa kwa madhumuni ya kubainisha jinsi lugha ya utangazaji inavyotumiwa kufuma maana na kufanikisha mawasiliano katika sajili ya mchezo wa kandanda. Mbinu muhimu za utafiti zilikuwa usomaji wa maktabani uliomwezesha mtafiti kung'amua mambo muhimu na kujenga msingi na usuli wa utafiti huu kama ilivyoonyeshwa katika sura ya kwanza. Aidha, mtafiti alihusisha usikilizaji wa matangazo ya moja kwa moja ya mchezo wa kandanda redioni na taarifa zinazohusu mchezo huu kwenye redio na runinga ambapo data iliyochanganuliwa ilikusanywa.

Utafiti huu uliegemezwa katika nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo. Nadharia hii inatambua aina tatu za maana: maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa ili kubainisha aina hizi za maana

kama zinavyojitokeza katika sajili ya mchezo wa kandanda. Utafiti huu ulifanikiwa kutimiza malengo yafuatayo:

- Kutambua mbinu za mawasiliano zinazotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda.
- Kubainisha msimbo wa maana unaoibuliwa kutokana na matumizi ya lugha katika sajili ya mchezo wa kandanda.
- Kubainisha taaluma na sajili zinazotumiwa na sajili ya mchezo wa kandanda ili kujitosheleza.

Malengo haya yalitimizwa kama inavyodhihirika katika muhtasari ufuatao wa matokeo ya utafiti.

## 5.1 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yameangaziwa katika sura ya pili, sura ya tatu na sura ya nne. Mbinu za mawasiliano zinazotumiwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda zimebainishwa katika sura ya pili. Imebainika kuwa watangazaji wa mchezo wa kandanda hutegemea mbinu hizi kuwasiliana na kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji wao. Kwa sababu watangazaji wa mchezo wa kandanda hutumia lugha ya uneni, wanahusisha mbinu za kiisimu. Miongoni mwa mbinu zilizobainika ni utohozi, uchanganyaji msimbo, ubadilishaji msimbo, maswali ya balagha, tafsiri sisisi na tamathali za usemi kama vile urudiaji, tashbihi, tashihisi, misemo, misimu na methali.

Utohozi uliobainika ni wa maneno ya lugha ya Kiingereza katika Kiswahili. Baadhi ya maneno ya Kiingereza yaliyotoholewa katika lugha ya Kiswahili ni kama vile *super star, defender, referee, league, coach, offer, penalty* na *finals.* Mbinu ya utohozi imejitokeza kama chambo cha kuteka nadhari ya msikilizaji ili amakinike kupokea ujumbe na kama mbinu ya ukuzaji na upanuzi wa msamiati wa lugha usio na visawe vyake katika lugha pokezi au iwapo visawe vilivyopo havijazoeleka wala kueleweka na wengi. Vile vile, utohozi umejitokeza kama mbinu itumiwayo na watangazaji wa mchezo wa kandanda kurahisisha mawasiliano na wasikilizaji wao na katika kujitambulisha nao.

Uambatishaji kiungo, uchopekaji wa maneno ya kigeni kati ya sentensi na uchopekaji wa maneno ya kigeni mwishoni mwa sentensi ni aina za uchanganyaji msimbo na ubadilishaji msimbo zilizobainika. "*Defender* anaondoa mpira katika eneo la hatari", "Mkufunzi wa timu ya Tusker analazimika kufanya *substitution* ya mapema baada ya mlinzi wa safu ya kulia kuumia" na "Kona hiyo itapigwa kuelekea lango la Tusker. Anaruka pale na kupiga mpira kwa kichwa, la, la, la! *That was a free header, and he misses a very clear chance!"* ni baadhi ya matini za uchanganyaji msimbo na ubadilishaji msimbo zilizobainika. Katika utangazaji wa mchezo wa kandanda, uchanganyaji msimbo na ubadilishaji msimbo umeonyesha dhima ya kurejelea, kufafanua, kusisitiza, kupendeza na kujitambulisha na kuonyesha hisia.

Imebainika kuwa lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda hutumia misemo na misimu kama mbinu ya kuwachangamsha wasikilizaji, kujitambulisha na mashabiki na kunogeza zaidi lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda. Misimu inayotumiwa na watangazaji ni kama vile *angusha bomu, ingia jehanamu, vunja benki, pika bao, pora mpira, sugua benchi, jenga kibanda* na *cheka na wavu* hutambuliwa na kueleweka na wasikilizaji bila utata wowote. Hali kadhalika, tafsiri sisisi inayohusishwa na watangazaji haitatizi mawasiliano kati yao na wasikilizaji kwa sababu wanaelewa muktadha wa matumizi yake. Tafsiri sisisi zilizojtokeza kama vile *golden boot, dirisha la uhamisho, Mashetani Wekundu, Wanabunduki* na *Paka Weusi* zilihusu hali ya mchezo, usajili wa wachezaji, na lakabu za klabu mbalimbali.

Aina za takriri zilizobainika ni takriri-vitenzi na takriri-nomino. Takriri imejitokeza kama mbinu inayotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda kusisitiza ujumbe na kueleza mfululizo wa mchezo wa kandanda. Matumizi ya mbinu hizi kwa uchangamano hufaulisha mawasiliano kati ya watangazaji wa mchezo wa kandanda na wasikilizaji wao.

Sura ya tatu imechanganua matini ili kubainisha maana zinazowasilishwa katika sajili ya mchezo wa kandanda. Uchanganuzi huu umebainisha kuwa lugha huwa na maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi. Lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda imebainisha maana dhanishi kupitia vitenzi kama vile *adhibu, tandika, kaanga, lipua, nyanyasa, winda* na *wika*; nomino kama vile *bomu,*

*risasi, mahasimu, miamba, kombora,* na *mapinduzi* na vivumishi. *Butu, -kali, bivu, -bichi, -tamu* na *-baya* ni mifano ya vivumishi vilivyochanganuliwa.

Imedhihirika kuwa si wakati wote ambapo vipashio hivi vya lugha hutumiwa kwa maana yake tambuzi katika utangazaji wa mchezo wa kandanda. Vipashio hivi vinatumiwa kwa njia inayopanua, kugeuza na kuhamisha maana yake halisi katika uyakinifu wa ujumbe na utoshelevu wa mawasiliano katika sajili hii. Kwa mfano, matini 'Sofapaka *imeitandika* Tusker mabao manne kwa mawili' inamaanisha kuwa timu ya Sofapaka imeifunga ile ya Tusker mabao manne kwa mawili. Matumizi ya vipashio hivi yamefinyangwa kwa namna inayosawiri mchezo wa kandanda kama vita na uadui licha ya kuuhusisha na maswala ya biashara, upishi, ushirikina na unyumba.

Hivi ni kusema kuwa maana ya vipashio huweza kupanuka na hata kubadilika kulingana na matumizi yake katika miktadha tofauti. Hivyo basi, maana dhanishi hujitokeza kama msingi wa vivuli vya maana kulingana na muktadha wa matumzi katika sajili ya mchezo wa kandanda. Uchanganuzi huu umepambanua lugha kama chombo kinachobadilika kutokana na mahitaji ya watumizi wake na hivyo kuthibitisha nadharia ya SAM inayosema kuwa lugha huwa na maana dhanishi pale watumizi wake wanaposimba tajriba za ulimwengu wao kuzieleza hali zinazowazunguka. Imebainika kuwa wakati mwingine maana ya vipashio vya lugha haiwi katika viashiria vyake bali matumizi yake.

Maana tagusani imedhihirisha tendo la usemi kupitia kauli za maagizo, rai, maswali na kauli ndefu za kimaelezo. Kauli za maagizo zinasheheniwa na wasimamizi wa mchezo huu katika kuusawazisha na kuudhibiti huku kauli za rai na maswali yakitumiwa sana na wachezaji wanapojieleza kwa wasimamizi uwanjani au wanapozungumza miongoni mwao.

Wachezaji hutumia kauli za rai kuwaomba radhi waamuzi kwa kukiuka sheria zinazodhibiti mchezo huu na wenzao wanaowachezea visivyo huku wakitumia maswali kuulizia maamuzi yasiyowaridhisha na wanapochezewa visivyo na wenzao. Kwa mfano, "...Terry anamwambia *pole ndugu yangu, hii ni hali ya game"* ni maneno yanayomhakikishia mchezaji Aguero kuwa mwenzake hakudhamiria kumwangusha au kumuumiza. Mazungumzo, majibizano na majibu yanayotokana na kauli hizi hujenga mahusiano thabiti miongoni mwa watumizi hawa wa lugha na hivyo kufanikisha mawasiliano. Hii ni kwa sababu katika mchakato huu wote, hata wasikilizaji huwa na uwezo wa kutabiri mielekeo ya wenzao na hivyo kuhusiana nao kwa njia inayowafanya wote wakubalike katika jamii yao.

Kauli ndefu za maelezo marefu hujitokeza kama sifa muhimu ya lugha inayotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda katika kueleza mfululizo wa matukio ya mchezo wenyewe kama unavyotokea ili kueleweka na wasikilizaji na kufikisha ujumbe kwa uwazi zaidi.

Maana matinishi imetumikisha kanuni za kisarufi na kusarifu ujumbe kutokana na ugeuzi wa upanguaji, uchopekaji na udondoshaji. Ugeuzi huu huwawezesha watangazaji kutumia lugha kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji wao kwa njia bora zaidi bila kurudia baadhi ya vipashio vinavyoeleweka kwao wote. Kupitia udondoshaji, watangazaji wa mchezo wa kandanda huepuka kupoteza wakati. Hii ni kwa sababu mchezo wa kandanda huchezwa kwa kasi na mfululizo usioweza kuwaruhusu watangazaji kuelezea matukio yote kama yanavyotokea. Mbali na kuonyesha uhalisia wa maongezi ya kawaida, upanguaji umedhihirisha uwezo wa msemaji kubuni tungo nyingi zinazomwezesha kueleweka kwa uangavu zaidi kutokana na vipashio vya lugha yake.

Aidha, maana matinishi imebainika kutokana na urejeshi unaoleta muwala na msisitizo wa ujumbe katika usemi. Wakati mwingine urejeshi na uwakilishaji hutumiwa kutokana na kasi ya mchezo na kauli kuwa si rahisi kwa watangazaji kuwajua au kuwataja wachezaji wote kwa majina yao mchezo unapoendelea. Pamoja na haya, maana matinishi imedhihirika kupitia matumizi ya vihusishi vinavyofaulisha mawasiliano kwa kuunganisha vipande vya vipashio vya lugha ili kuunda matini zenye mshikamano kwa njia inayowasaidia wasikilizaji kufuatilia matukio ya mchezo kwa urahisi.

Uchanganuzi wa matini katika sura hii umeonyesha kuwa maana tagusani ambayo huwa na uamilifu husishi inatumiwa kuyakinisha maana dhanishi. Huku maana dhanishi ikiwakilisha dhati ya ujumbe, maana tagusani huangazia kaida



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

zinazodumishwa na jamii ili kudhibiti mawasiliano kimuktadha. Maana dhanishi na maana tagusani hujitokeza kama amali za kimsingi ambazo utoshelevu wa dhima zake hutegemea amali ya maana matinishi. Hii ina maana kuwa vipashio vya lugha huunganika kuleta maana amilifu kulingana na muktadha na kaida za jamii. Kwa jumla, imebainika jinsi maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi zinavyohusiana na kudhibitiana ili kusuka tanzu za sintaksia, semantiki na pragmatiki katika uyakinifu wa maana, udokezi wa ujumbe na ukamilishaji wa mawasiliano.

Uchanganuzi wa matini ili kubainisha taaluma na sajili tofauti zinazotumiwa na sajili ya mchezo wa kandanda katika kujifuma na kujitosheleza umefanywa katika sura ya nne. Imebainika kuwa sajili ya mchezo wa kandanda huchota malighafi na vipashio vyake kutoka taaluma na sajili mbalimbali kama vile ulinzi, biashara, hospitali, hoteli na mapenzi.

Istilahi za taaluma ya ulinzi zimebainika kama vitenzi, vivumishi, semi, nomino zinazohusu zana za vita, nomino zinazohusisha mchezo wa kandanda na makabiliano au uhasama na nomino zinazohusisha mchezo wa kandanda na nguvu, uthabiti au mamlaka ya kiutawala. Mifano ya vitenzi katika taaluma ya ulinzi ni kama vile *charaza, lipua, tandika, tesa, vamia, vizia, zaba, pora* na *shambulia. Bomu, risasi, kombora, mahasimu, mapambano, mapinduzi, kikosi, vigogo* na *mibabe* ni baadhi ya nomino zilizojitokeza huku *butu* na *–kali* ikiwa mifano ya vivumishi vilivyotumika katika taaluma ya ulinzi. Semi zilizobainika ni kama vile

*piga risasi, lipiza kisasi, tia mkononi* na *teka nyara* Matumizi ya istilahi za ulinzi yamesawiri sajili ya mchezo wa kandanda kama vita, uadui na maangamizi.

Istilahi za sajili ya hospitali zimewakilishwa na vitenzi na nomino kama vile *roga, dawa, ahueni, machela, mchawi* na semi kama vile *piga bao* na *kufa na kupona* huku istilahi za sajili ya biashara zinazotumiwa kusuka sajili ya mchezo wa kandanda zikibainika kupitia vitenzi kama vile *uza, lipa, nunua, mauzo,* na misimu kama vile *vunja benki* na *peleka mnadani*. Maana zinazotokana na matumizi ya istilahi za biashara hujenga wachezaji wa mchezo wa kandanda kama bidhaa na huduma zinazofanyiwa biashara sokoni.

Istilahi za sajili ya hoteli zimebainika kutokana na matumizi ya vitenzi kama vile *iva, kaanga*. Sajili hii vilevile imebainishwa kupitia vivumishi kama vile *–tamu, -bivu* na *-bichi,* misemo na misimu kama vile *lala njaa, pika bao* na *kula na kutapika* huku sajili ya mapenzi ikijitokeza kupitia matumizi ya vitenzi kama vile *chumbia* na *najisi,* na nomino kama vile *mpenzi* na *tasa* miongoni mwa nyingine.

Matumizi ya misamiati ya sajili ya hoteli huwaangalia wachezaji wazuri sawa na vyakula vilivyoiva vizuri na vitamu huku matumizi ya istilahi za sajili ya mapenzi zikinasibisha wachezaji mahiri na mabinti warembo. Hali kadhalika, harakati zote za kutafuta na kusajili wachezaji wapya huangaliwa sawa na shughuli za unyumba kama vile uchumba na posa.

Matumizi ya misamiati ya hospitali hunasibisha mchezo wa kandanda na ushirikina na utabibu. Wachezaji wakakamavu wananasibishwa na *waganga, wachawi* na *dawa* huku mchezo wa kuvutia unaosababisha ushindi ukiangaliwa sawa na urogi.

Matumizi ya misamiati ya sajili au taaluma hizi kusuka na kuibua maana zinaonyesha utegemezi wa sajili ya mchezo wa kandanda kwa nyingine. Istilahi hizi ndizo zilizofinyangwa kimatumizi ili kutoa vivuli tofauti vya maana. Hivi ni kusema kuwa matumizi ya lugha ili kuibua maana katika sajili ya mchezo wa kandanda huwa na msingi wake katika kufinyanga vipashio vya taaluma na sajili nyingine. Ni kwa namna hii ambavyo upekee wa matumizi ya lugha na uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda hujitokeza na hivyo kuwezesha sajili hii kujifuma na kujitosheleza.

**5.2 Mahitimisho ya Utafiti**

Lugha hutumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda kwa minajili ya kupitisha ujumbe na kuwasiliana na wasikilizaji wao. Mawasiliano haya yanafanikishwa kupitia mbinu kama vile utohozi, uchanganyaji msimbo, ubadilishaji msimbo, takriri, tashbihi, tashihisi, misemo, misimu, methali, maswali ya balagha na tafsiri sisisi.

Utafiti huu umebainisha kuwa mawasiliano haya yanakamilishwa kutokana na upekee wa matumizi ya lugha katika sajili hii. Upekee huu wa matumizi ya lugha

huzua hali ambapo maana tambuzi ya vipashio vya lugha huwa msingi wa kutoa vivuli vya maana nyingine, yaani maana ya vipashio vya lugha hupanuliwa, hugeuzwa na kuhamishwa katika sajili ya mchezo wa kandanda kulingana na matumizi yake. Hivi ni kusema kuwa watumizi wa lugha katika sajili hii husimba tajriba za ulimwengu wao katika kueleza hali zinazowazunguka. Ni kwa njia hii ambapo uyakinifu wa ujumbe na utoshelevu wa mawasiliano huwezeshwa katika sajili hii.

Katika kusuka na kufuma maana, sajili ya mchezo wa kandanda imeonyesha utegemezi wa istilahi za taaluma na sajili nyingine kama vile hoteli, ulinzi, hospitali, biashara na mapenzi. Uchanganuzi wetu wa data umeonyesha kuwa taaluma ya ulinzi imetoa mchango mkubwa zaidi wa 60.61% ikifuatwa na sajili ya hoteli ambayo imechangia 12.12%. Sajili ya biashara imechangia 9.85% huku sajili ya utabibu au hospitali ikichangia 9.09%. Hali kadhalika, sajili ya mapenzi imechangia 8.33%. Hivyo basi, imebainika kuwa sajili hii hujijenga na kujitosheleza kutokana na mfinyango wa vipashio vya sajili nyingine.

Upekuzi wa kiusomi wa mada hii umeweza kuongeza hazina katika tafiti zilizofanywa kuhusu uchanganuzi wa matini na kuwezesha kuiorodhesha miongoni mwa tafiti zinazohusu maana katika isimujamii. Waaidha, utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika ukuzaji wa taaluma ya isimujamii na tagaa la pragmatiki.

## 5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu umebainisha uhamishaji wa maana kutokana na upekee wa matumizi ya lugha katika sajili ya mchezo wa kandanda. Utafiti huu ulijikita katika matini za uneni. Hivyo basi, pana hitaji la kufanya utafiti zaidi kuhusu matini andishi ili kutambua aina ya miundo na msimbo unaoweza kujitokeza. Aidha, utafiti wa kubainisha lugha ya malumbano miongoni mwa mashabiki wa mchezo huu pamoja na nyimbo wanazotumia kushangilia timu zao hasa mchezo huu unapoendelea unaweza kutupa mwanga zaidi kuhusu matumizi ya lugha katika sajili hii.

Lakabu mbalimbali za kurejelea klabu, viwanja, wachezaji na wakufunzi zinapaswa kupewa uchunguzi zaidi wa kitaaluma ili kubaini jazanda zinazohusishwa nazo. Hali kadhalika, utafiti unaweza kufanyiwa mada hii kwa uzingativu wa michezo mingine ili kumulika jinsi matumizi ya lugha na uibuaji wa maana unavyoshabihiana au kutofautiana katika sajili ya michezo kwa jumla.

# MAREJELEO


Adero, M. C. (2005). 'Uwezo wa Lugha katika Matini za Siasa Nchini Kenya kuanzia Mwaka wa 2002 hadi 2005'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haïjachapishwa).

Aloo, S. N. (2002). 'Uchanganuzi wa Matangazo ya Biashara katika Redio na Televisheni: Mtazamo wa Kipragmatiki.' Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Alter, R. (1981). *The Art of Biblical Narrative*. New York: Basic Books Publishers.

Appel, R. na Muysken, P. (1987). *Language Contact and Bilingualism*. London: Edward Arnold.

Austin, J. L. (1962). *How to Do Things with Words*. Clarendon: Oxford.

Beeman, W. (1977). *The Dictionary of Anthropology*. Oxford: Blackwell.

Berelson, B. na Steiner, G. (1969). *Human Behaviour*. New York: Harcourt Brace.

Berk-Seligson, S. (1986). 'A Linguistic Constraints on Intra-Sentential Code-Switching: A Study of Spanish/Hebrew Bilingualism.' *Language in Society* 15: 313-348.

Bolinger, D. na Sears, D. (1981). *Aspects of Language*. (3rd edition). New York: Harcourt Brace Javanorich Inc.

Brierly, S. (1995). *The Advertising Handbook*. London: Routledge.

Brown, G. na Yule, G. N. (1983). *Discourse Analysis.* Cambridge: Cambridge University Press.

Buliba, A., Njogu, K. na Mwihaki, A. (2006). *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Butchavarov, P. (1960). *Philosophy.* London: Cambridge University Press.

Cartford, J. C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation.* New York: Oxford University Press.

Chapman, R. (1989). *Linguistics and Literature: An Introduction to Literary Studies.* London: Edward Arnold.

Cook, A. B. (1969). *Introduction to English Language: Structure and History.* New York: The Ronald Press Company.

Cook, G. (2000). *The Discourse of Advertising.* 2nd Edition. London: Routledge

Cook, V na Nelson, M. (1996). *Chomsky's Universal Grammar.* Oxford: Blackwell

Crystal, D. na Davy, D. (1969). *Investigating English Style.* London: Longman Group Limited.

Deuchar, M na Quay, S. (2000). *Bilingual Acquisition: Theoritical Implications of A Case Study.* New York: Oxford University Press.

Falk, J. S. (1973). *Linguistics and Language: A Survey of Basic Concepts and Implication.* New York: John Wiley and Sons.

Fromkin, V. na Rodman, R. (1978). *An Introduction to Language*. New York: Rinehart and Winston.

Gichohi, W. na Kagwa, M. ( 2007) . *Kamusi Changanuzi ya Methali*. Nairobi: Moran.

Goody, E. N. (1978). *Towards a Theory of Questions: Questions and Politeness Strategies in Social Interactions.* Cambridge: Cambridge University Press.

Gumperz, J. (1982). *Discourse Strategies.* Cambridge: Cambridge University Press.

Habwe, J. (1989). 'Elements of Pragmatic Discourse among Mvita People'. M. A Thesis, University of Nairobi (Unpublished).

Habwe, J. (1999). 'Discourse Analysis of Swahili Political Speeches'. Ph.D Thesis, University of Nairobi (Unpublished).

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Habwe, J., Matei, A. K., na Nyonje, J. (2010). *Darubini ya Isimujamii kwa Shule na Vyuo.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Halliday, M. A. K. (2004, 1994, 1985,). *An Introduction to Functional Grammar.* London: Edward Arnold.

Halliday, M. A. K. na Hasan, R. (1989). *Langauge, Context and Text: Aspects of Language in a Social-Semiotic Perspective*. Oxford: Oxford University Press.

Halliday, M. A. K., McIntosh, A. na Strevens, P. (1964). *The Linguistic Science and Language Teaching*. London: Longman.

Ho, J. W. Y. (2007). Code-mixing: Linguistic Form and Socio-cultural Meaning. *The International Journal of Language Society and Culture 21*. (http://www.educ.utas.edu.au/users/tle/JOURNAL/issues/2007/21-2.pdf)

Hudson, R. (1995). *Word Meaning*. London: Routledge.

Hymes, D. H. (1974). *Foundations in Sociolinguistics: An Ethnographic Approach*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Ipara, I. O. na Maina, G. (2008). *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford University Press.

Jefwa, G. M. (2010). *Utangulizi wa Isimu*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Kiai, A. (1999). 'A Discourse Analysis of Education Radio Programs to Farmers: Adaptation Register'. M. A Thesis, University of Nairobi. (Unpublished).

Kihara, D. K. (2006). 'Uchambuzi wa Matini: Matumizi ya Lugha katika Sajili ya Matatu'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

King'ei, K. na Kisovi, C. (2005) . *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kombo, D. K. na Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Pauline Publications Africa.

Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. (2nd edition). New Delhi: New Age International Publishers.

Leech, G. (1966). *English in Advertising: A Linguistic Study of Advertising in Great Britain*. London: Longman.

Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to Poetry*. London: Longman.

Leech, G. (1983). *Principles of Pragmatics*. London: Longman Publishers.

Lehman, W. (1972). *Descriptive Linguistics: An Introduction*. New York: Rand House.

Levinson, S. C (1983). *Pragmatics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Longhorn Publishers (K) Ltd. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Lucas, F. L. (1955). *Style*. London: Cassell & Company.

Lyons, J. (1968). *Introduction to Theoritical Lingustics.* Great Britain: Cambridge University Press.

Lyons, J. (1977). *Semantics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Lyons, J. (1981). *Language and Linguistics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Maina, R. W. (2011). 'Mbinu za Mawasiliano katika Matangazo ya Runinga Nchini Kenya'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Massamba, D. P. B. (1987). 'The impact of politics in language development in Tanzania', *Kiswahili* 54, 1 and 54.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. na Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA). Dar es Saalam: TUKI.

Matei, K. A. (2011) . *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili.* Nairobi : Oxford University Press.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Michira, J. (1993). 'Uchanganuzi wa Kimtindo wa Lugha ya Matangazo ya Biashara Redioni'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Morreale, S. P. (2004). *Introduction to Human Communication.* Belmont: Wadsworth.

Mugenda, O. M. na Mugenda, A. G. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Munyasa, A. T. (2012). 'Upekee wa Lugha katika Mikahawa ya Eastlands'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Musau, P. (2000). 'The Development of Swahili Styles: The Use of Metaphor in the Language of Football Commentary.' Katika Njogu, K., Momanyi, C., King'ei, K. na Musau, Paul. (Wah). *Kiswahili Katika Karne ya Ishirini na Moja.* Nairobi: Twaweza Communications Ltd. 243-250.

Muysken, P. (2000). *Bilingual speech. A typology of code-switching.* Cambridge: Cambridge University Press.

Naseh, L. (1997). Codeswitching between Persian and Swedish, Eurosla 7 Proceedings: 201-211.

Ndalu, A. na King'ei, K. (1988). *Kamusi ya Semi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Ndalu, A. na King'ei, K. (1989). *Kamusi ya Methali za Kiswahili.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Ndung'u, V. (2001). 'Uchanganuzi wa Usemi katika Sajili ya Dini: Sifa Bainifu za Lugha ya Mahubiri'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K., King'ei, K., Momanyi, C. na Musau, P. (Wah) (2000). *Kiswahili Katika Karne ya Ishirini na Moja.* Nairobi: Twaweza Communications Ltd.

Njogu, K., Mwihaki, A. na Buliba, A. (2006). *Sarufi ya Kiswahili: Uchanganuzi na Matumizi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Norwich, P. (1998). *Meaning.* London: Oxford University Press.

Orodho, J. A. (2005). *Elements of Education and Social Science Research Methods.* Nairobi: Masola Publishers.

Pfaff, C. W. (1979). 'Constraints In Language Mixing' in *Language* 55. pp 291-318.

Poplack, S. (1980). 'Sometimes I will start a Sentense in Spanish y termino en Espanol: Toward a Typology of Code Switching.' *Linguistics 18.* pp 58-618.

Richards, J., Platt, J. and Weber, H. (1985). *A Longman Dictionary of Applied Linguistics*. London: Longman.

Romaine, S. (1989). *Bilingualism*. Oxford: Basil Blackwell.

Spolsky, B. (1998). *Sociolinguistics*. New York: Oxford University Press.

Tanaka, K. (1994). *Advertising Language: A Pragmatic Approach to Advertisements in Britain and Japan*. London: Routledge.

Tannen, D. (1984). *Conversational Style*. New Jersey: Ablex Publishing Corporation. The Jomo Kenyatta Foundation.

Todd, C. (1987). *An Introduction to Linguistics*. London: Longman.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la Tatu. Dar-es-Salaam: Oxford University Press, East Africa Ltd.

TUKI. (1999). *Kamusi ya Isimu na Lugha*. Dar es Saalam. TUKI.

Ullmann, S. (1972). *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Basil Blackwell.

Vestergaard, T. and Shroder, K . (1985). *The Language of Advertising*. Oxford: Blackwell.

Walya, E. (1996). 'Kenyan Banking Discourse: Structure, Strategies and their Effect on Banking Interaction'. M. A Thesis, Kenyatta University. (Unpublished).

Wamitila, K. W. (2001). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K. W. (2003a). *Kamusi ya Tashbihi, Vitendawili, Milio na Mishangao*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K. W. (2003b). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Wendell, V. H. (1992). *Dictionary of Concepts in Literary Criticism and Theory.* New York: Greenwood Press.

Yule, G. N. (1996). *The Study of Language*. (2nd edition). Cambridge: Cambridge University Press.

**Kiambatisho 1: Matini za Misimu**

| Msimu | Matini |
|---|---|
| Ona/ tifua kivumbi | Mchezo unamalizika na Sofapaka imeonyeshwa kivumbi na timu ya Chemelil. |
| Aga mashindano | Thika United yaaga mashindano haya ya GoTv baada ya kushindwa na Sofapaka. |
| Kuwa na miguu ya glasi | Mchezaji huyu mwenye miguu ya glasi ametolewa uwanjani baada ya kulaliwa manwari |
| Tuliza mzuka | Mchezaji huyu Torres sasa ametuliza mzuka Chelsea baada ya kupata nafasi nyingi za kucheza. |
| Beba mikoba | Mchezaji Keli anatazamiwa kubeba mikoba ya timu yake mpya. |
| Chimba mkwara | Mkufunzi huyu mpya bwana Kimanzi anaendelea kuchimba kwara Tusker. |
| Bahati kusimama | Wanaendelea kufyatua *risasi* kali hapa ili kukomboa timu lakini bahati haijasimama. |
| Jenga ukuta | Naona wachezaji wanajenga ukuta pale kabla ya foul hiyo kuchezwa. |
| Tingisha/ tetemesha wavu. | Sserenkuma anaingia pale katika eneo la hatari, hatari pale-ee anatingisha wavu tena! |
| Soma gazeti | Msikilizaji Arsenal inaonyesha mchezo mzuri na kumiliki mpira, naona kipa wao anasoma tu gazeti. |
| Shuka dimbani | Mpenzi msikilizaji ikiwa unajiunga nasi sasa nakufahamisha kwamba timu hizi zilishuka dimbani saa kumi jioni. Hadi sasa dakika ishirini na saba zimechezwa. |
| Pachika bao | Anakwenda na mpira, anapiga pale-ee go-oool. Msikilizaji Sserenkuma anapachika bao kimyani, Gor moja, Sofapaka sufuri. |
| Kupigwa kiatu | Valencia anakwenda na mpira, anachenga moja, mbili, lakini anapigwa kiatu na ankubali kwenda chini |

| | |
|---|---|
| Kusakata ngozi | Wanacheza pale, sasa wanasakata ngozi ile kurudi nyuma. Wanaanza kwao tena hawa. |
| Weka kibindoni | AFC Leopards ilimweka mshambulizi huyu Keli kibindoni punde tu kabla ya msimu huu kuanza na sasa ameanza kuonyesha makali yake. |
| Nyoshea kidole | Tusker imekuwa ikimnyoshea Ulinzi kidole na leo zinakutana ana kwa ana, haya msikilizaji... |
| Ota mbawa | Msikilizaji mechi hii kati ya Gor Mahia na AFC Leopards yaota mbawa baada ya mashabiki kuzua vurugu. |
| Kuficha mpira | Sikiliza penalty hiyo. Anajivuta Gerrard na kucheza mpira goo-oool! Msikilizaji kiungo huyu alificha mpira huu kushota na kumbwaga kipa aliyelala kulia. |
| Chonga kona | Anaweka mpira karibu na kijibendera kile na kujivuta. Anachonga kona rojorojo katika eneo la hatari-iii anaondosha kwa kichwa pale Terry. |
| Kupatiwa namba | Anachenga moja, anachenga mbili, tatu, anavurumisha kombora nzito-oo go go –ooo l...mchezaji huyu anamdhihirishia kocha wake kwamba alifanya busara *kumpatia namba.* |
| Kupangua ngome | Anaregesha mpira ule Wanyonyi hadi safu ya ulinzi ili kupanga njama ya *kupangua ngome* ya mahasimu wao... |



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**Kiambatisho 2: Matini za Vitenzi**

| **Kitenzi** | **Matini** |
|---|---|
| Kamua;<br>Uma | Mpenzi msikilizaji tunakukaribisha katika kipindi cha pili cha mchezo huu. Timu hizi *zilizoumana* bila mafanikio katika kipindi cha kwanza zinaendelea *kukamuana* hapa... |
| Kwaruza;<br>Vaa;<br>Bwaga | Naona wachezaji wa timu zote mbili wakiingia uwanjani tayari *Kukwaruzana* hapa. Mwenzangu ananiambia kuwa msimu uliopita timu hizi *zilipovaana* hapa hapa, Sofapaka *iliwabwaga* Tusker magoli tatu kwa moja. |
| Garagaza | Msikilizaji timu zote mbili zinarudi kwenye uwanjani zikiwa tayari kuendelea *kugaragazana* baada ya muda wa mapumziko kuisha. |
| Pagawa;<br>Roga | Mpenzi msikilizaji tangu mshambulizi huyu van Persie kutua Man United baada ya kuwindwa na timu hii kwa misimu miwili amekuwa *akiwapagawa* waajiri wake hawa wa zamani. Leo amerudi hapa uga wa Emirates *kuwaroga* tena Arsenal, anafunga bao maridadi la kusawazisha. Huyu ni mchawi kweli. |
| Nyakua | Kufika leo bado haijulikani ni timu gani *itanyakua* taji la mwaka huu kwa sababu timu ya Liverpool, Chelsea na Manchester City zimetengwa na pointi nne tu na bado zimebaki mechi tano. |
| Ng'ang'ania;<br>Menya;<br>Pokonya | *Wanang'ang'ania* mpira ule, *wanamenyana* vikali, mshambulizi yule anakataa *kupokonywa* mpira, kizaazaa kwenye lango. |
| Tawala;<br>Ng'aa | Wanachukua mpira pale katikati ya uwanja, wanatambariza, anamgawia pasi nzuri, anamtilia tena mwenzake, *wanang'ara* msikilizaji, wanacheza hapa pasi za kuonana hawa, mchezo wa nipe nikupe, wanaendelea *kutawala* mchezo huu. |
| Tuma;<br>Chambua | Anakwenda pale na mpira, anakwenda, anakwenda, *anatuma* chuma nzito pale-ee la la la bado! Mshambulizi huyu |

| | |
|---|---|
| | Aguero *anawachambua* madifenda hawa wa Manchester United lakini anakosa bao. La! |
| Alika | Katika mchezo wa leo Ulinzi *inawaalika* Gor Mahia katika uwanja wao wa Manispaa ya Nakuru. |
| Achilia; Pangua | Anakwenda, anaingia pale Rama Salim, hatari, hatari pale, *anaachilia* goo go bado! Kipa anaruka kama nyani na *kupangua* kombora hiyo. |
| Nyata; Poteza; Okoa; Tisha | Haya, sikiliza penalty hii. *Ananyatia* mpira ule Collison, anapiga-aa *anapoteza.* Fabianski *anaokoa* tena jamani. Hakika kipa huyu *anatisha. Anaokoa* penalty ya pili hapa. Ananikumbusha *alivyookoa* penalty ya Bayern kule Ujerumani. |
| Tema | Mlinzi huyu *aliyetemwa* na Tusker amekuwa nguzo katika timu yake mpya ya AFC Leopards. |
| Lisha | Anakwenda, anakwenda, anangia pale, analaliwa manowari mshambulizi wa Ulinzi. Naona refa anafikia mfuko wake *anamlisha* nyekundu mlinzi huyu. |
| Bisha | Wanaingia pale tena wanasamawi kwenye eneo la hatari, Oscar, Oscar kwake nani- ii Hazard, anatuma chuma kwa nguvu-u kipa anapangua. Hee he! Wanaendelea kubisha lango hili vijana wa Mourihno. |

**Kiambatisho 3: Matini za Nomino**

| Nomino | Matini |
|---|---|
| Dimba; Mchuano | Popote ulipo msikilizaji, tunakukaribisha katika *dimba* hili la leo. *Mchuano* huu ni kati ya vigogo hawa Sofapaka na Tusker inatazamiwa kuwa mgumu. |
| Ngozi | Wanachukua mpira pale kwenye wingi wa kulia, wanatambariza, anamtilia mwenzake pasi, wanasakata *ngozi* kweli kweli hawa wachezaji wa Ulinzi. |
| Hoi; Ahueni; Kifaa; Kindumbwe-ndumbwe | Anachanja kona maridadi juu juu Carzola, anapiga kichwa Mertersarker go-oool! Katika dakika ya themanini na sita, Arsenal inakomboa bao dhidi ya Wigan kwenye *kindumbwendumbwe* cha nusu fainali ya kombe la FA. Kocha wao Wenger na wachezaji waliokuwa *hoi* wanapata *ahueni* . Dakika zilikuwa zinayoyoma hapa msikilizaji. Mertersarker kwa mara nyingine anaonyesha kuwa yeye ni *kifaa* cha kutegemewa, analinda na anafunga. |
| Jiwe; Kinda; Dawa; | Msikilizaji usione wembamba wa reli, *kinda* huyu Janujaz ambaye aliingia dakika tano tu zilizopita, anarusha *jiwe* zito hadi kimyani, kijana huyu anafanya mauaji hapa, amekuwa *dawa* ya maadui za Man U, leo ni kama mara yake ya tatu kutoka bench na kuokoa timu yake. |
| Mteja; Mzinga; Maembe; Zawadi | Wanasonga na mpira pale katikati ya uwanja, anachukua Rooney, anaangalia acheze wapi, anatuma *mzinga* mrefu kwenye lango-oo, anafunga. Salaale! Anapata *zawadi* hapa bila jasho, kipa alikuwa *mteja.* Msikilizaji kipa huyu *maembe* atajilaumu kwa kuuza timu yake. |
| Risasi | Katika dakika ya sabini na tatu, Sofapaka wanapata hapa bao la nne, Tusker bado ina bao mbili. Tusker ina mtihani mgumu kushinda mechi hii. Wanaendelea kufyatua *risasi* kali hapa ili kukomboa timu yao lakini bahati |

| | |
|---|---|
| | haijasimama. |
| Maiti | Katika Manchester derby second leg, Ciy inaichapa United mabao matatu bila jibu baada ya kuilipua mabao manne kwa moja katika mkondo wa kwanza. Tangu Moyes kuchukua ukufunzi, Manchester United imekuwa *maiti* wa kuzikwa na timu yoyote. |
| Kipenzi;<br>Nyota;<br>Nguzo | Naona anatoka Ramsey anaingia Ozil. Msikilizaji *kipenzi* huyu wa mashabiki kabla ya kunaswa na Arsenal, *nyota* huyu Mjerumani ambaye amekuwa *nguzo* ya safu ya katikati alinyemelewa na timu kadha kama vile Chelsea na Manchester United. |
| Mauaji;<br>Moto;<br>Mtambo;<br>Mchawi | Anatuliza mpira Suarez kwenye gamba la kifua, anachenga moja, anachenga tena, anatoa pasi ya back heel kwake Sturridge, anachukua tena, anapiga go-goo-oool! Anafanya *mauaji* hapa. Anafunga bao lake la thelathini msimu huu na kuvunja rekodi ya ufungaji wa mabao Liverpool. Mchezaji huyu anawika kweli, amekuwa *moto* wa kuotea mbali. Huyu ni *mtambo* wa kufunga na si ajabu alichumbiwa na timu kadha katika dirisha la uhamisho msimu uliopita. Huyu ni *mchawi* kweli kweli. |

**Kiambatisho 4: Matini za Kauli za Maelezo**

1. *Ananyunyiza pale mpira juu juu hadi pembezoni mwa uwanja na kutulizwa maridadi na kiungo wa wingi wa kushoto nani yule. Anakwenda, anakwenda na mpira, anatoa krosi rojorojo pale kwenye lango lakini washambulizi wanachelewa. Sijui ni wazito au namna gani mambo hapa.*

2. *Anapokea msikilizaji mpira ule mree-efu na kutuliza kwenye gamba la kifua. Anageuka nao, piga kanzu pale Agwanda, anajaribu kuingia katika ngome ile lakini anazidiwa ubabe na walinzi wa Gor waliokuwa macho. Wanaondosha hatari ile.*

3. *Anamegewa pale pasi ya mwaka na kuituliza. Anakwenda, anakwenda Nasri, anakwenda na mpira, anakwenda nao, hatari, hatari katika lango, hatari katika lango-oo anapiga nje! Salaale! Ajabu gani hii, alikuwa na mpira peke yake lakini anajaza nje. La!*

**Kiambatisho 5: Matini za Udondoshaji**

| **Kauli/matini zilizodondoshwa/fupishwa** | **Kauli/matini kamili** |
|---|---|
| Anacheza mbele | Anacheza mpira mbele |
| Anarudisha nyuma | Anarudisha mpira nyuma |
| Wamemkaba yule hatari | Wamemkaba mchezaji yule hatari |
| Huyu hapa anakula njano | Mchezaji huyu hapa anakula kadi ya njano |
| Wale wanakwenda mbele | Wachezaji wale wanakwenda mbele |
| Wanarudi mbio | Walinzi wanarudi mbio katika eneo lao |
| Mchezaji yule amechezewa visivyo na kuumizwa. Inabidi atolewe nje | Mchezaji yule amachezewa visivyo na kuumizwa. Inabidi atolewe nje kwa machela |
| Anakwenda, anakwenda, anakwenda... | Anakwenda na mpira, anakwenda na mpira, anakwenda na mpira |
| Anapanda, anapanda kule-ee | Anapanda, anapanda kule-ee kwenye wingi wa kulia |
| Anatoa haraka haraka | Anatoa mpira harakata haraka |
| Mpendwa msikilizaji tunakukaribisha katika mechi hii ya Liverpool na Chelsea. | Msikilizaji tunakukaribisha katika kusikiliza matangazo ya mechi kati ya Liverpool na Chelsea. |
| Anachukua mpira pale mchezaji Wanga, anakwenda, anakwenda, anakwenda... | Anachukua mpira pale mchezaji Wanga, anakwenda Wanga, anakwenda Wanga, anakwenda na mpira... |
| Anachanja kona maridadi juu juu Carzola, anapiga kichwa Mertersarker go-oool! | Anachanja kona maridadi juu juu Carzola, anapiga mpira kwa kichwa mchezaji Mertersarker go-oool! |



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY